Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 10 Julai, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama kawaida yetu leo tena ni siku ya Alhamisi ya Maswali kwa Waziri Mkuu. Kwanza, kuna Taarifa za kuwasilisha mezani. Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:-**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:-**

Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2008/2009.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF (K.n.y. MAGDALENA H. SAKAYA - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII):-**

Taarifa ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

## TAARIFA YA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, katika eneo la kwanza la taarifa kweli kulikuwepo na Taarifa ya Spika, ambayo imetolewa chini ya Kanuni 33(1) ya Kanuni za Bunge. Katika Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge unaoendelea Bunge lilipitisha Muswada wa Sheria wa Serikali uitwao *the Public Audit Bill, 2008* na sasa ni Sheria Namba 11 ya mwaka 2008.

Muswada huo ulipelekwa kwa Rais ili upate kibali chake baada ya kupitia katika hatua zake zote za uchapishwaji. Tayari Mheshimiwa Rais ametoa kibali chake na sasa Muswada huo ni Sheria ya Nchi. Kwa hiyo, hongera Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ni Muswada ambao kwa kweli uliingia *fast track* na ni *fast track* kwa kweli. Kwa hiyo, tunaendelea na shughuli za leo, Katibu. (*Makofi)*

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kufuatana na utaratibu wetu maswali ni ya papo kwa papo. Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni ndiye atakayeuliza swali la kwanza. Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MHE. HAMAD R. MOHEMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa mnamo tarehe 8 Julai, 2008 Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar alitoa ufafanuzi au maelezo ya kwamba Zanzibar ni nchi au *source* nchi. Ni nini kauli ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kutokana na maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli anachokisema, nilitoa maelezo hapa kuhusiana na suala hilo ambalo nimeona limezua mjadala mzuri tu upande wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Lakini kwa hili labda nitende haki pengine ngoja ninukuu vifungu vya Katiba vinasema nini katika kujaribu kuliweka jambo hili vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema: “Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano.” *(Makofi)*

Ibara ya 2(1) ya Katiba hiyo inasema: “Eneo la Jamhuri ya Muungano ni eneo lote la Tanzania Bara na eneo lote la Tanzania Zanzibar na ni pamoja na sehemu yake ya bahari ambayo Tanzania inapakana nayo.” *(Makofi)*

Sasa kwa sababu nilimsikiliza Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa Zanzibar akisema kwamba Zanzibar ni nchi na akatumia maneno kwamba ni *State*. Ngoja niseme Kiingereza kinasemaje kwenye Katiba. Ibara ya Kwanza ya Katiba kwa Kiingereza inasema: "*Tanzania is one State and is sovereignty United Republic*." *(Makofi)*

Ibara ya 2, Ibara ndogo inasema: "*The Territory of the United Republic consist of the all of the area of Mainland Tanzania and all of the area of Tanzania Zanzibar and includes territory waters.*" *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ndiyo maelezo ya Kikatiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Baada ya kufanya utafiti baada ya kuona mjadala mkali nikataka kuona chimbuko hasa linatokana na nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar ina Katiba yake na ninukuu baadhi tu ya maeneo muone tatizo liko wapi, na kwa hiyo, wote tuseme tunafanyaje?

Katika Ibara ya Kwanza ya Katiba ya Zanzibar inasema: "Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania." Ibara ya 2 Ibara ndogo inasema:-

"Eneo la Zanzibar ni eneo lote la Visiwa vya Unguja na Pemba na Visiwa vidogo vidogo vilivyozungukwa na bahari yake ambayo kabla ya Muungano ikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar." Nikaona bado haitoshi ukienda Ibara ya 9 ya Katiba ya Zanzibar inasema, nafikiri nisome zote mbili. Ibara ndogo ya kwanza inasema:-

"Zanzibar itakuwa nchi ya Kidemokrasia na haki za jamii." Ibara ndogo ya pili inasema: Kwa hivyo, hapa inaelezwa rasmi kwamba akaendelea kufafanua mamlaka yanayotokana na madaraka ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unachoweza kukiona hapa katika kujaribu kumjibu Mheshimiwa rafiki yangu Hamad Rashid Mahomed ni kwamba Katiba zote mbili zina *make reference* kwa maneno nchi, na nadhani ndiyo maana unakuta Zanzibar kidogo waliona kama vile Mheshimiwa Waziri Mkuu kama kateleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa maana ya msingi wa Katiba ya Jamhuri ambayo ndiyo inayotuunganisha sisi wote wawili ambayo mimi ninaamini ndiyo Katiba Mama kwa maana hiyo ndiyo maana nikasema hakuna nilichoteleza.

Lakini kama lipo tatizo pengine la tafsiri ya mambo haya, hili pengine tutamwaachia Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wakae watazame lugha hii katika Katiba mbili inatupa tafsiri gani ili pengine tuweze kuwa waangalifu tunapotoa kauli mbalimbali. Ndiyo maana nikasema sitakuwa na jibu la moja kwa moja, ninaloweza kusema sana sana ni hilo. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD R. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, imeonekana kama lipo tatizo la tafsiri, na mahali peke yake kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ni Mahakama ya Katiba ndiyo inaweza kutupa tafsiri ya hayo mambo mawili. Kwa nini suala hili tusilipeleke kwenye Mahakama ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kupata tafsiri sahihi?

**NAIBU SPIKA:** Lazima kwanza kuwepo mgogoro jamani. Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nimesema ukishafika kwenye masuala ya tafsiri sasa ya kipi ni sahihi. Maana hapa nadhani maneno *Sovereignty State* na neno nchi ni kama yanaleta kidogo hali ya kutoeleweka vizuri. Zanzibar ni *Sovereignty State.*

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo

**WAZIRI MKUU:** Wamejibu haraka haraka mno, ndiyo maana nimesema si langu. Mimi nadhani tuwaachie Wanasheria hao wawili waangalie na kama hapana budi wanaweza kupeleka jambo hili Mahakamani tukapata *interpretation* ambayo ni nzuri zaidi. *(Makofi)*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu nitamuuliza swali kuhusu *Bio fuels*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na *statement* ambazo zimekuwa zikitolewa na Serikali na Waheshimiwa Wabunge humu Bungeni, lakini na wananchi mbalimbali vilevile huko nje ya Bunge kuhusu faida na hasara za Kilimo cha Mimea ya Kuzalisha *Bio fuel* ambayo ni *energy*. Ni dhahiri kwamba wengi wetu Watanzania tunaelewa hasara ya kulima mazao haya kama michikichi, jetrofa na kadhalika hasa kuwaathiri bionwai, mazingira, masuala ya jamii pamoja pengine hata masuala ya kiuchumi? Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu tumeendelea kuruhusu watu kushika maeneo makubwa na kulima mazao kama jetrofa hapa nchini. Hatuna mwongozo bado, hatuna sera, hatuna sheria wala hakuna mkakati tunajikanganya.

Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa nini tunasingoje tusimamishe shughuli zote hizi kuwapa watu vibali vya kuanza kulima mpaka sheria, mkakati na sera ziwe tayari na zifanyiwe *Strategic Environmental Assessment* ili kujihakikishia kwamba haitatuletea matatizo mbele ya safari? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu. Naomba maswali yenu yawe *directed focus* siyo kuwa marefu

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu ndugu yangu Mheshimiwa Raphael Mwalyosi kama ifuatavyo:- Kilimo cha mazao ambayo baadaye yanakuja kutoa mafuta ni dhahiri kimezungumzwa sana katika nyanja mbalimbali.

Sina hakika kama suala hapa ni la *Environmental Impact Assessment* kwa maana ya kwamba mazao hayo yanaweza kuwa na madhara gani kwenye mazingira yetu au ile *product* yake hasa nadhani ndiyo pengine ingeangaliwa zaidi. Kwa hiyo, nadhani ni jambo njema tutalifikiria haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka niseme tu Serikali ilichofanya haraka haraka. Tumewaandikia Wakuu wa Mikoa wote, tumewapa maagizo ya kiutawala kwamba jambo hili linalohusiana na kilimo hiki kwanza tumesema ni vizuri Wakuu wa Mikoa wakahakikisha kwamba maeneo hayatolewi kiholela kwa sababu hiyo ni *danger* ya kwanza. Tukasisitiza kwamba maeneo kwa uelewa wetu ambayo yangeweza kutolewa pengine bila madhara makubwa kwa maana ya ardhi ni yale ambayo yanaonekana hayafai kwa kilimo cha mazao ya chakula na mazao mengine ya biashara. Sasa naamini Wakuu wa Mikoa jambo hilo watakuwa wameanza kulizingatia na tuliona tufanye hivyo haraka wakati Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika inaandaa sasa mwongozo dhabiti. Lakini kubwa zaidi kwa kweli sheria kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge na jitihada zinafanyika sasa hivi. Nadhani haitachukua muda mrefu kabla hatujaleta.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesita kusema tusimamishe kwa sababu wengine tayari wapo huko, lakini tumeona tujihami kwa kuhakikisha kwamba hili jambo linawekwa katika mfumo ambao utakuwa kidogo wa manufaa kwetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi swali la nyongeza liwe fupi.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa maelezo mazuri. Lakini ukiangalia maeneo mengi ambayo yamechukuliwa sasa hivi kwa mfano, Kusini mwa Tanzania, wamechukua tayari *very plain land* ambayo kibionwai ni maeneo ambayo yako karibu na Selou kwa mfano. Maeneo ya Ukanda huu wa Kusini Kilwa na wapi, wamechukua maeneo makubwa *up to more than eighteen thousand hectors*. Maeneo makubwa sana tayari yamechukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilichokuwa nasema yale maeneo ambayo hawajaanza kuyalima kwa nini tusiwasimamishe mpaka wangoje sheria ipite kwanza. Kwa nini tunaendelea kuwaruhusu watu wengine wanaanza kufika kwenye maeneo hayo kule?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, haya tunakubali tutapeleka maagizo hayo. Nadhani ni jambo jema tu. (*Makofi*)

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa kuwa, Serikali mbili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, imeunda Kamati mbili za pande zote

mbili kwa ajili ya kupitia mapitio ya mgawanyo wa fedha zinazotoka kwenye michango ya faida ya BOT na misaada inayotoka nje. Sasa hivi Kamati hiyo ni mwaka wa pili sasa kutoa mapendekezo yake kwa ajili ya Serikali kwa ajili ya gawio la 4.5. Serikali imekaa kimya kwa muda wa miaka miwili bila kupata maelezo yoyote, Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu anaeleza nini kwenye Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya mapato hayo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu ndugu yangu Mheshimiwa Mbunge, kuhusiana na hili suala. Suala hili limekuwa linazungumzwa sana, linaulizwa sana hapa Bungeni, lakini vikao vingine nje ya Bunge najua limekuwa likiulizwa sana na maelezo ambayo yamekuwa yakitolewa jumla ni kwamba ni kweli si jambo ambalo Serikali imelifumbia macho.

Tunaelewa uzito wake na ndiyo tulilazimika vile vile kufika mahali na kujaribu kutafuta utaratibu wa kupata mtalaam tushauriane tuweze kuona namna bora ambayo tunaweza tukafikia muafaka ambao utatusaidia sana.

Lakini mimi baada ya kuwa nimelisikia mara kwa mara niliamua kwamba pengine jambo hili katika kikao kinachokuja ambacho kinaongozwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais anayeshughulikia masuala mbalimbali. Nimeona jambo hili ni vizuri niliweke katika *one of the agenda* pale pengine lipate msukumo kutoka pande zote mbili ndani ya uongozi wa Makamu wa Rais wakati Kamati hizo mbili nazo zinaendelea kwa upande wake, pengine tutaharakisha zoezi hili liweze kukamilika haraka.

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu toka tumepata uhuru watoto wa shule wa kike walikuwa wakipata mimba wanafukuzwa shule. Mpaka sasa hivi Serikali ina mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba watoto wote wanakwenda shule.

Lakini tatizo la kupata mimba bado lipo mashuleni na tafiti zimeonyesha kwamba nchi mbalimbali hapa Afrika ikiwemo Kenya, Zambia, Malawi, wamepunguza tatizo hilo kuhakikisha kwamba watoto wale wa kike wanaopata mimba huwa wanarudi mashuleni. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba tatizo hilo linapungua hapa nchini? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu dada yangu Mheshimiwa Suzan Lyimo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sina hakika kama nina jibu la moja kwa moja la uhakika la namna ya kudhibiti jambo hili. Kwa sababu ni jambo letu sisi Watanzania wenyewe na linafanyika miongoni mwetu ndani ya jamii, wazazi wakiwemo, walimu wakiwemo. Kwa hiyo, kwa kweli changamoto kubwa ninayoiona mimi kwanza ni kwa

jamii yenyewe kutambua kwamba jambo hili ni jambo ovu na halitakiwi kufanywa. *(Makofi)*

Lakini kama ni maelekezo Mheshimiwa Mbunge, tumejitahidi sana. Tumekuwa tukikemea, Rais amekemea sana. Lakini juzi nilikuwa Mbeya pale mtakumbuka nilichokiona watoto zaidi ya 700 wamebebeshwa mimba ndani ya kipindi cha miaka miwili *is a big figure*.

Lakini sasa tumekubaliana pale ofisini tunataka kufanya sensa ya nchi nzima, tunataka kujua hasa ukubwa wa tatizo ukoje. Baada ya pale pengine tujaribu kujadiliana wenyewe ndani kwa ndani, tuone tunakabiliana vipi na jambo hili. Kama sheria pengine zitaonekana ni laini labda tuzirekebishe ziweze kuwa kali zaidi kama njia ya kujaribu kutahadharisha jambo hili. Lakini kwa sehemu kubwa ni jamii yenyewe tukitambua wajibu wetu nadhani litatusaidia vizuri zaidi.

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nina swali dogo moja la nyongeza. Kwa kuwa wastani wa watoto wa kike kukua *inverted comers* ni miaka 13 tafiti zinaonyesha hivyo; na kwa kuwa watoto wa darasa la kwanza wanaanza na miaka 7 na kuendelea.

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba watoto wa kike wanaanza shule wakiwa na umri wa miaka mitano ili wanapomaliza darasa la saba wawe angalau na miaka 12 muda ambao bado wengi hawajakua na hivyo wale wanaume wanaowanyemelea washindwe? *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahaa! Sina hakika kama utakuwa umetatua tatizo Mheshimiwa Mbunge. Mimi naomba nirudie tu kwa sababu nilipokwenda Mbeya juzi nimekuta idadi kubwa ya watoto waliopata mimba ni wa shule za msingi. Kwa hiyo, ni udhaifu/uovu tu wanadamu kwamba baadhi ya watoto wale ambao wanapata mimba ni wadogo sana. Kwa hiyo, ukirudisha miaka nyuma ukadhani umesogeza mbele, pengine utahamisha tatizo kutoka shule za msingi kwenda sekondari. Bado tatizo litakuwa ni pale pale. Kwa hiyo, mimi nadhani kubwa kwa kweli tuondokane na tabia hizo ambazo siyo nzuri. (*Makofi*)

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kukuuliza mkutano wa nchi matajiri duniani maarufu kama G8 umemalizika hivi jana huko Japan. Lakini pamoja na kuwa nchi hizo matajiri walikuwa wamekutana, lakini pia nchi maskini zilikuwepo pale ikiwemo nchi yetu ya Tanzania kuhudhuria mkutano huo. Kwa kuwa, sasa dunia inakabiliwa na hali ya mfumko wa bei uliosababishwa na ongezeko la bei ya mafuta katika soko la dunia. Je, tutarajie nini mara baada ya mkutano huo ambao umemalizika hiyo siku ya jana? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina hakika kabisa Mheshimiwa Juma Killimbah hata Waheshimiwa Wabunge wengi mmekuwa mkifuatilia mkutano ule ulivyoendelea na kauli zilizokuwa zinatoka katika maeneo mbalimbali.

Mimi ninachokiona kikubwa tu kilichojitokeza kwanza ni *appreciation* tu kwamba tatizo lipo na ni kubwa sana.

Lakini sikuona mimi kama wametoka pale na kitu ambacho unaweza ukasema nchi maskini tutakuwa na manufaa makubwa sana hata kidogo. Sasa nilichokuwa natarajia mimi pengine ilikuwa ni kwa sababu ni watu wenye nguvu nyingi nilidhani wangesema kuanzia sasa tunataka nchi zinazozalisha mafuta zifanye *A, B, C*, lakini wapi na wao inaonekana wanaogelea katika tatizo hili na pengine huwezi ukajua *behind it* kuna nini.

Lakini kusema kweli mimi sidhani kama nimefarijika sana na matokeo ya mkutano ule. Kwa hiyo, nilitaka tu niseme Mheshimiwa Juma Killimbah bado lazima tuendelee kama Tanzania kutazama sisi wenyewe hapa ndani na na-*appriciate* sana baadhi ya mawazo yalitoka hasa kwenye matumizi ya gesi, tuone ni hatua zipi tunaweza tukachukua pengine kwa kutumia gesi yetu tuweze kupunguza baadhi ya matatizo ambayo yanajitokeza. Sitegemei maajabu kutoka kwenye vikao hivyo. (*Makofi*)

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu Jimbo la Vunjo hususan eneo la tambarare linalohusisha kata tatu za Kilua Kusini, Kahe Magharibi, Kahe Mashariki zinakumbwa na mafuriko makubwa kila mwaka ambayo yanaleta uharibifu mkubwa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu je, Serikali yako iko tayari kuunda mkakati maalum wa kujenga miundombinu ya kuelekeza maji yaende Mto Ruvu badala ya kusambaa kwenye mashamba ya wananchi wa Kata hizo na kuleta maafa kila mwaka? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli anachokisema Mheshimiwa Kimaro kwamba eneo lake mara nyingi sana limekuwa likikumbwa na mafuriko ya maji kwa sababu ya *element* ya tambarare na kuna milima inayozunguka maeneo yale.

Kwa hiyo, pengine niseme tu sina jibu moja kwa moja kwamba nimshauri.

Lakini nadhani, kinachoweza kufanyika niishauri Halmashauri yake pale itengeneze mradi ijaribu kuweka vile vigezo ambavyo tunafikiri vinaweza vikasaidia kupunguza sana tatizo hili, viwasilishwe Serikalini rasmi tuliangalie, tuone kama kuna namna ya kuweza kusaidia kupunguza matatizo yale yanayotokana na mafuriko ya mara kwa mara. (*Makofi*)

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu tatizo hilo ni kubwa kwa sababu wakati mwingine hata maisha ya watu hupotea.

Je, anaweza kunipa uhakika hapa kwamba Halmashauri ikileta mchanganuo wa kujenga hiyo miundombinu Serikali itatoa fedha kwa wakati unaofaa?

**NAIBU SPIKA:** Kwanza watengeneze, halafu wataona kutakuwa na uzito kiasi gani. Naomba tuendelee na swali linalofuata. *(Makofi)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, kwa kuwa hivi sasa kuna pengo kubwa sana kati ya mapato na matumizi ya Watanzania hasa wale wa kipato cha chini, jambo ambalo limesababisha umaskini mkubwa sana miongoni mwa wananchi kiasi kwamba Watanzania wengi leo wanaishi kwa mlo mmoja tu kwa siku.

Je, Serikali ina mkakati gani kuwaondoa Watanzania hapa walipo leo ili angalau watakapofika mwaka 2010 waweze kuishi maisha bora? Ahsante. (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijaribu kutoa maelezo kuhusiana na swali la Mheshimiwa Salim Khamis kuhusiana na hali ya umaskini hapa Tanzania.

Si siri wala si jambo ambalo mtu unaweza ukasema halifahamiki. Ni kweli kwamba Taifa letu ni moja kati ya mataifa ambayo bado ni maskini na ni kweli vile vile kwamba Watanzania walio wengi bado maisha yao yako duni ukilinganisha pengine na nchi zilizoendelea.

Sasa nikisema hivi sina maana kwamba hakuna nyingine katika Bara la Afrika, au Mabara mengine yapo, lakini huko ni kukiri ukweli.

Sasa Serikali inafanya nini ndiyo maana umeona katika jitihada za Serikali tumejaribu kuja na aina mbalimbali za sera, mikakati mbali mbali ya kujaribu kumsaidia mwananchi wa Tanzania aweze kutoka hapa alipo na kupiga hatua moja mbele.

Tunachoweza kusema ni kwamba pamoja na jitihada zote hizi ambazo tumeziona hasa katika kuimarisha uchumi mpana bado watalaam wanasema pamoja na mafanikio yote tuliyoyapata kutahitajika miaka 10 mpaka 20 tukiwa chini ya kiwango cha *GDP* isiyopungua asilimia 10 ili tuweze kuona matokeo ya haya mafanikio unayoyaona. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni dhahiri kabisa kwamba kazi iliyopo ni kubwa na mimi ninachoweza kusema tu Mheshimiwa Khamis ni kwamba tushirikiane wote, jitihada zilizopo

zitatusaidia pole pole tuweze kusonga mbele lakini kwa maana ya mwaka 2010 kwamba tuwe tumeshafikia huko hapana tusikudanganye. Lakini hatua hizo zitatupeleka hatua moja lakini tutakuwa bado hatujafika mwisho wa safari. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wa maswali kwa Waziri Mkuu umekwisha. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru sana nadhani tumeridhika na utaratibu wa maswali unaojibu.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 187

### Mihadi ya Serikali Isiyoshughulikiwa

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA** aliuliza:-

Kwa kuwa, taarifa ya *CAG* ya mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2007 imeonyesha kuwa, mihadi ya Serikali ya thamani ya Tsh. 131,897,754,514/= haikuwa imeshughulikiwa hali ambayo inazidi kuwa mbaya siku hadi siku kwani mwaka 2005/2006 mihadi ambayo haikushughulikiwa ilikuwa ni Tsh. 18,874,596,840/= na mwaka 2006/2007 ilikuwa Tsh. 131,897,754,514/= ongezeko la asilimia 598.8:-

(a) Je, hali hiyo imesababishwa na nini, kwa nini imepanda ghafla kiasi hicho?

(b) Je, ni nini athari za kiuchumi na kijamii kitaifa za mihadi isiyotekelezwa ndani ya mwaka mmoja wa fedha?

(c) Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na hali hiyo hasa ikitiliwa maanani kauli mbiu ya Serikali ya Kasi mpya, Nguvu mpya na Ari mpya?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI** (**MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa, Mbunge wa Jimbo la Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Fedha, Afisa Mhasibu anapaswa kuonyesha kwenye hesabu za fedha anazozisimamia, mihadi yote ambayo

mikataba kati ya Wizara/Idara/Mkoa husika imekamilika lakini utekelezaji wa shughuli kwa maana ya utoaji wa vifaa au huduma hadi kufikia tarehe 30 Juni, ulikuwa haujafikia hatua ya kulipwa.

Uonyeshaji huo ni kwa madhumuni ya kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kutokana na wajibu huo, katika mwaka wa fedha 2006/2007, taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilionyesha mihadi ya Tshs. 131,897,754,514/= ukilinganisha na Tshs. 18,874,596,840/= mwaka 2005/2006.

Hali hii imesababishwa na Wizara mbalimbali ikiongozwa na Miundombinu ambayo ilikuwa na sehemu kubwa ya mihadi ya Barabara ambayo utekelezaji wake haukuwa umefikia hatua ya kulipiwa ilipofika tarehe 30 Juni, 2007.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sehemu kubwa ya mihadi inayoripotiwa ndani ya taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ni ile inayotoka kwenye Bajeti ya Maendeleo, ambayo mara nyingi utekelezaji wa miradi huchukua zaidi ya mwaka mmoja, haitakuwa rahisi kukadiria athari za kiuchumi, kijamii na kitaifa kwa kuchelewa kutekeleza kwa kipindi hicho. Hata hivyo, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba athari zingeweza kuonekana kama tungechelewa zaidi.

(c )Mheshimiwa Naibu Spika, kauli ya Serikali ni kuhakikisha kuwa tunajitegemea hatua kwa hatua katika kugharamia matumizi yetu ya kawaida na ya maendeleo. Pia kufanya manunuzi kwa kufuata Sheria na Kanuni za Manunuzi.

Aidha, ni vyema kwa kila mradi kuandaliwa vipindi vya utekelezaji na mahitaji ya fedha kwa nia ya kuondokana na tatizo la ucheleweshaji wa malipo.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Bajeti na malengo yake yanapitishwa mwaka hadi mwaka na Bunge. Na kwa kuwa utekelezaji unategemewa kuwa ndani ya mwaka husika jambo ambalo linasaidia pia kwa usimamizi na udhibiti kwa upande wa Mkaguzi Mkuu.

Je, kwa kuwa hali hii inaendelea kuongezeka na sababu kubwa ni kucheleweshwa fedha na wafadhili Serikali iko tayari kukaa na wafadhili kuwa na mpango rasmi wa lini fedha zitolewe ili bajeti ya Serikali iliyopitishwa na Bunge isiathirike?

Swali la pili, kwa kuwa kwa kawaida *quotations* yaani tenda inapotolewa kandarasi zinapotolewa bei zinakuwa kwa muda usiozidi siku 90 na kwa kuwa Jaji Warioba katika taarifa yake ya Rushwa alisema kwamba mwanya mmoja mkubwa ni katika kandarasi za ujenzi hasa wa barabara. Suala hili la kuzidishiwa kwa kiwango hiki inaonyesha inatengeneza mwanya wa rushwa.

Je, Serikali inafanya nini sasa ili mwanya huu uweze kuzibwa kwa sababu katika taarifa za Mkaguzi imeonekana pia kuna mianya mingi hapa ya matumizi mabaya?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka niseme Serikali inakaa na wafadhili kila mwaka, sasa hivi tunakaa takriban mara nne.

Lakini wazo la Mheshimiwa Slaa la kukaa nao na kujadili jinsi ya fedha kutolewa kwa wakati ni wazo zuri na tutalifanyia kazi zaidi.

Lakini la pili, ni suala la mwanya ambalo linatokana na zabuni, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Dr. Slaa avute subira hivi sasa tunalifanyia marekebisho Sheria ya Manunuzi tutaleta marekebisho haya Bungeni na marekebisho haya yanalenga zaidi katika kuthibiti hiyo mianya isiweze kutokea.

Na. 188

**Huduma ya Kuongeza Wagonjwa Damu Katika Kituo cha Afya cha Mwamashimba**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Kituo cha Afya cha Mwamashimba kinahudumia wananchi wengi wanaotoka kwenye Kata za Kikubiji, Bupamwa, Fukalo, Mhande, Mwamala na Mwamashimba; na kwa kuwa, hakuna huduma ya wagonjwa kuongezewa damu kwenye kituo hicho:-

Je, Serikali itapeleka lini huduma hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanzisha Mpango wa Taifa wa Damu Salama kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji endelevu wa Damu iliyo salama na ya kutosha katika vituo vyetu vya kutolea huduma inapohitajika.

Hadi sasa Serikali yetu kwa kushirikiana na Serikali ya Marekani imejenga vituo sita vya kanda vya damu salama katika kanda za Kaskazini (Moshi), Ziwa (Mwanza), Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), Mashariki (Dar es Salaam), Magharibi (Tabora) na

Kusini (Mtwara). Kazi zinazofanywa na vituo hivi ni pamoja na uhamasishaji, ukusanyaji, upimaji, uhifadhi na usambazaji wa damu salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya kumpatia mgonjwa damu kama tiba inahitaji umakini na utaalam wa hali ya juu. Kituo chochote cha Afya kinaweza kuruhusiwa kutoa huduma ya kuongeza damu baada ya kuthibitika kuwa kinakidhi vigezo kwa viwango vinavyokubalika.

Vigezo hivyo ni pamoja na kuwepo jengo, wataalam na vifaa vya kupima damu (*Cross-Matching and Blood Grouping*) na jokofu ambalo linapata umeme wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia mpango wa damu salama itakuwa tayari kutoa huduma ya damu na ushauri wa kitaalam kwa vituo vyote vinavyokidhi vigezo vya utoaji wa huduma kuongeza damu vinginevyo itabidi wapate damu kutoka Kanda ya Ziwa kwa Mheshimiwa Nyawazwa kama alivyoomba.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii niulize maswali madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba ili kukidhi haja ya kuwekewa huduma hii kuwe na jokofu na bajeti ya jana ya Nishati na Madini tayari eneo hili litawekewa umeme kwa mwaka huu. Je, Serikali inasemaje sasa kupeleka huduma hizo baada ya umeme kupelekwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili watu wa tarafa hiyo ya kituo hiki kuna kata sita ambazo zinatakiwa zihudumiwe na Wilaya ya Kwimba ina gari moja tu la wagonjwa ambalo ni jumla ya kata 25. Je, Serikali sasa haioni umuhimu kupeleka gari la wagonjwa lingine la pili ili liweze kuwahudumia Kata zote 25 na watu wa Kwimba wapate huduma nzuri kama hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII**: Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza kama nilivyosema katika jibu langu la msingi nimesema moja ya kigezo kuweza kukidhi ni kuwepo na jokofu.

Lakini vile vile nimesema ni lazima kuwepo na wataalamu na vifaa vya kuweza kutibia kwa sababu tunafahamu kabisa damu lazima upime kuhakikisha kwamba huwezi kuambukiza magonjwa mengine kwa mgonjwa ambaye anahitaji damu. Kwa hiyo, kama watakidhi kama nilivyosema basi wataweza kupatiwa zile huduma zinaweza zikatolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, suala la usafiri. Ni kweli kabisa kama anavyosema Kwimba ina kata 25 ningependa kumshauri kwamba kama Halmashauri likae katika Bajeti zao ili iweze kuona kwamba wanatenga fedha kupitia TAMISEMI ili waweze kununua gari la wagonjwa liweze kukidhi mahitaji ya Wilaya ya Kwimba na hususan katika Kata hizi 25 ambazo zinahitaji huduma za usafiri.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana. Aidha, napenda nimpongeze dada yangu Esther Nyawazwa kwa swali lake zuri sana ambalo linagusa hisia za wapiga kura wangu wa Jimbo la Kwimba hasa wanaotumia Kituo cha Afya cha Mwamashimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nimwulize swali moja. Kwa kuwa uwezo wa Halmashauri zetu kupata wataalam pamoja na vifaa unazidiwa kidogo kama umeme ukipatikana katika Kituo cha Afya hapa kama tulivyoahidiwa. Je, Serikali itakuwa tayari kutuma wataalam pamoja na vifaa ambavyo vitakavyokuwa vinahitajika ikiwa pamoja na *X-ray*?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Mwamashimba watapata umeme na suala la wataalam kama nilivyokuwa nikizungumzia tukae na Mheshimiwa Sakila pamoja na Mheshimiwa Nyawazwa ili tuweze kuona kwamba kipindi hiki tutaweza kuwasaidia namna gani ili kuongeza wataalam na vile vile kuongea na TAMISEMI tuweze kuona kwamba tutawasaidia namna gani ili kuweza kuongezea waweze kupata vifaa tiba ambavyo vitawatolea huduma watu wa Mwamashimba na jimboni kwake Kwimba.

Na. 189

### Uchunguzi wa Matukio ya Watu Wanaojinyonga

**MHE. JAMES D. LEMBELI** aliuliza:-

Kwa kuwa, ni jukumu la kisheria la Polisi kuchunguza matukio yote ya watu wanaojinyonga kabla ya mazishi kufanyika na Jeshi la Polisi huwajibika moja kwa moja na gharama husika.

Je, ni sababu gani za msingi zinazowafanya Polisi wa Kahama kwa kushirikiana na Watendaji wa kata na vijiji kuwalazimisha wananchi kwenye maeneo yalikotokea matatizo ya mauaji au mtu kujinyonga kuchangia fedha kwa ajili ya mafuta ya magari yao na kusababisha usumbufu na malalamiko mengi toka kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi ndilo lenye jukumu kisheria kuchunguza matukio yote ya jinai yakiwemo ya mauaji na linawajibika moja kwa moja na gharama husika. Hivyo hakuna sababu zozote za msingi zinazoweza kuwafanya Polisi Kahama kwa kushirikiana na Watendaji wa Kata na Vijiji kuwalazimisha wananchi kwenye maeneo yaliyotokea matatizo ya mauaji au mtu kujinyonga kuchangia fedha kwa ajili ya mafuta ya magari ya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchunguzi wetu hatukufanikiwa kupata ushahidi wa Polisi kudai fedha kutoka kwa wananchi kwa ajili ya kugharamia mafuta ya magari ya Polisi. Aidha, bado uchunguzi unaendelea kubaini endapo kuna watendaji wa Kata na vijiji wanaodai fedha kwa kisingizio cha kugharamia mafuta ya magari ya Polisi na kusababisha usumbufu kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, iwapo Mheshimiwa Mbunge anayo taarifa kwamba askari wa Wilaya ya Kahama wanashirikiana na watendaji wa Serikali za Kata na vijiji kuwadai wananchi fedha kwa ajili ya kugharamia huduma za Polisi tunaomba atufahamishe ili Jeshi la Polisi liweze kuchukua hatua zinazostahili.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa katika Wilaya ya Kahama matukio ya vifo vya aina hii ni mengi. Na kwa kuwa Polisi Wilaya ya Kahama hupata mgao mdogo wa mafuta sawa na Wilaya ambazo hazina matatizo mengi hivyo mara nyingi kuwa na upungufu wa mafuta kufuatilia matukio kama haya yanapojitokeza.

Je, Serikali iko tayari kuongeza mgao wa mafuta kwa Wilaya hii ya Kahama ili kuondoa kabisa tatizo la watu kutumia ujanja, kuchangisha wananchi fedha kinyume cha utaratibu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema sisi hatuna ushahidi kuhusu matukio ya askari kuwafanya wananchi wachange kuhusu shughuli za kutafuta wahalifu. Nimesema hivi na naomba kama upo ushahidi wa kutosha na Mheshimiwa Lembeli anayo taarifa kuhusu hiyo atuletee tuweze kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mgao wa mafuta itakuwa nasema uongo nikiweza kuahidi hapa kwamba mafuta yatagawiwa kwa sababu mafuta yanakwenda kwa mujibu wa Bajeti ambayo tunakuwa nayo kama Wizara.

Kwa mujibu wa fedha ambazo tunazozipata au Kasma ambayo tulikuwa nayo tutaendelea kwa utaratibu huo mpaka tutakapopata fursa ya kuweza kupata fedha za kutosha ambazo kwa kweli hili tatizo la ufinyu wa mafuta sio kwamba ni la hapo tu lakini ni tatizo ambalo linakabili nchi nzima lakini askari wetu wanajitahidi kadri wawezavyoBajeti tunayazingatia.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi na mimi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo hili ambalo lipo katika Wilaya ya Kahama ni tatizo la nchi nzima pamoja na kwamba Naibu Waziri anasema hana taarifa lakini ni tatizo la nchi nzima. Je, Serikali iko tayari kufanya utafiti na kuona jinsi watu wanavyosumbuliwa wakati wanapopata kesi kama ya mauaji?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utafiti, utafiti tutafanya lakini naomba pawepo na ushirikiano. Ushirikiano kati ya sisi katika vyombo vyetu na wananchi husika. Wananchi ndio wanaoathirika au ndio wanapata matatizo haya kama yapo kama wanavyosema Waheshimiwa Wabunge.

Kwa hiyo, ningeomba tuwe na ushirikiano wa karibu watuletee taarifa kama hivi tuko hapa ili tuweze kujua tuweze kuyafanyia kazi na bado nitasema kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwamba jukumu la kugharamia matatizo kama haya pote nchini si jukumu la wananchi na wananchi wasibughudhiwe ni jukumu la Jeshi la Polisi.

Na. 190

**Sheria ya Ndoa, Mirathi na Sheria Zinazohusu Watoto**

**MHE. MWAJUMA HASSAN KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa, Waziri wa Katiba na Sheria alipokuwa akijibu hoja ya Mheshimiwa Shoka Khamis Juma kwenye Mkutano wa Nane wa Bunge kuhusu marekebisho ya Sheria ya Ndoa, Mirathi na Sheria zinazohusu watoto aliliambia Bunge kuwa, Sheria hizo ziko kwenye mchakato na kwamba, zitaletwa Bungeni; na kwa kuwa, sasa ni muda mrefu umepita na Sheria hizo hazijaletwa Bungeni kama alivyoahidi.

Je, ni sababu zipi za msingi zinazosababisha Sheria hizo kuchelewa kuletwa Bungeni ili zifanyiwe marekebisho?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Wizara imewahi kutoa ahadi ya kuleta marekebisho ya Sheria za Ndoa, Urithi na Mirathi ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa uamuzi wa sasa wa Serikali kuhusu sheria hizi, ni kuandaa Waraka wa Serikali *(White Paper*) ili kupata na kukusanya maoni ya wananchi kuhusu sheria hizi. Hii ni kwa sababu maeneo mbalimbali ya sheria hizi yanagusa imani, mila na desturi za wananchi wengi na ambao busara inahitaji washirikishwe kwa ukamilifu ili mabadiliko yatakayofanywa yawe na manufaa zaidi kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya zoezi hili kukamilika, mapendekezo ya mabadiliko au utunzi wa sheria mpya yataletwa ndani ya Bunge lako Tukufu.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho yalioombwa kwa muda mrefu yalikwisha kufanyiwa kazi na Tume ya Kurekebisha Sheria. Tume hiyo ilishazunguka nchi nzima. Leo inarudi tena kuzunguka nchi nzima kukusanya maoni ya watu. Lakini wakati huo huo kuna matatizo ya msingi kwa mfano malezi ya mtoto aliyepatikana nje ya ndoa ni shilingi 100/= kama ilivyokuwa miaka ya 1960. Je, Serikali haioni kwamba kuna uharaka wa kushughulikia maeneo ya haraka wakati wanaendelea kukusanya maoni katika mambo mengine?

**NAIBU SPIKA:** Hii ya shililngi 100/= kwa kweli hapana!! (*Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze kwanza hili la malezi. Hili la malezi halihusiani na Sheria ya ndoa wala Sheria ya watoto ni sheria nyingine tofauti inayohusu mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa si mtoto aliyoko ndani ya ndoa. Lakini nizungumze sasa kuhusu sheria hizi za ndoa na kwa nini tunafanya *white paper*. Mwaka 1969 tulikuwa tunaangalia tena sheria hii hasa ya ndoa. Tulifanya *white paper* ambayo iliongozwa na Jaji Suply wakati ule na matokeo yake tukapata sheria ya ndoa ya mwaka 1971. Umuhimu wa jambo hili kulifikisha kwa wananchi ni kwamba tukikaa hapa hata watu kumi tu hatutaelewana wala kukubaliana kuhusu jambo hili. Lazima tupate maoni ya wengi linahusiana na mila, dini, desturi za watu na sasa hivi kuna mambo kwamba tunahusika na dunia kwa ujumla, mambo mapya. Lazima tukae tupate muafaka wa wananchi. Tulifanya hivyo mwaka 1969 tunadhani tutafanya tena mwaka huu tukimaliza mwaka ujao pengine hili zoezi litachukua mwaka tukimaliza tutaleta sheria ambayo inakubalika na inajumuisha maoni na matakwa ya wengi itakuwa rahisi kuitekeleza sheria ya namna hiyo.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Majibu ya Mheshimiwa Waziri yanaonyesha kwamba kuna tatizo la mila mambo ya dini lakini hili jambo ni jambo la msingi sana kubadilisha kwa hizo sheria ambazo zinaonyesha zinamkandamiza mtoto au mwanamke.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu kwa nini Serikali isifanye haraka kutoa elimu kwa jamii hizo ili hiyo sheria iletwe mara moja Bungeni tuweze kubadilisha kwa sababu kuna watoto wadogo sana wanaoolewa wakiwa na umri mdogo ambao wanatakiwa wawepo shuleni na wanakuwa na watoto na ni madhara makubwa kwa mtoto mdogo kupata mtoto katika umri mdogo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la umri wa kuolewa ndio suala la msingi katika sheria hii ya ndoa kwa mfano. Sasa hivi sheria hii inasema mtoto wa kike anaweza kuolewa akiwa na miaka 15, mtoto wa kiume anaweza kuoa akiwa na 18. Sheria hii ilitungwa baada ya kupata maoni ya wananchi wengi sana, huo ndio ukweli wenyewe ulivyo.

Tulifikia sheria hii ya miaka 15 baada ya kuzunguka nchi nzima chini ya Jaji Suply mwaka 1969, kama tunaona sasa miaka 15 sio umri muafaka, basi tutakuja tutaleta mapendekezo tutabadilisha. Lakini lazima tupate muafaka lazima tupate *consensus* ya wananchi kwa ujumla na ndiyo maana tunafanya zoezi hili.

Sasa hivi Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoka kuongea hapa kuhusu tatizo la mimba linalowapata vijana wetu wa kike chini ya miaka 15. Ni tatizo la jamii, ni tatizo kubwa sana katika jamii, sasa kama Mheshimiwa Mbunge analeta mapendekezo tufanye elimu ili watu wengi walielewe hili ni jambo zuri lakini nafikiri ni katika mila zetu na ndiyo maana nasema mila zetu wenyewe lazima tuzibadilishe.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa baadhi ya dini suala la ndoa na suala la mirathi ziko sheria zao ambazo toka enzi na enzi katika vitabu zimo hivyo inaonesha wazi kwamba sheria hizi hazitokidhi kutokana na huko nyuma zinakotoka taratibu zao. Je, Serikali kwa wale ambao hata ikitungwa sheria haihusiki kutokana na dini zao inazungumza nini Serikali? (*Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapotunga sheria inakuwa inaweka *standard* ya nchi. Lakini inatambua kwamba zipo sheria za kimila na kwamba zipo sheria za kidini na inaziheshimu.

Kwa hiyo, endapo mtu atakuwa anatawaliwa na sheria za kidini basi hizo ndizo sheria zitakazomtawala katika maisha yake na endapo yuko mtu hana sheria za kidini

basi Serikali imeweka sheria ambazo zitamtawala yule ambaye hahusiki na sheria hizo za kidini au za kimila.

Na. 191

**Msisitizo wa Kulima Mazao ya Chakula**

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwepo na msukumo mkubwa wa kilimo cha kuzalisha mazao ya mafuta *(oil crops)* kama jatrofa nk; na hivyo kufanya uzalishaji wa mazao ya chakula kupungua kwa kiasi kikubwa:-

(a)Je, Serikali haioni kuwa, kwa kufanya hivyo wakulima watakosa chakula hasa pale mazao hayo ya mafuta yatakapokosa soko?

(b)Je, Serikali haioni kuwa mazao hayo ya mafuta hayataweza kushindana na *natural oil*, hasa ikitiliwa maanani kuwa Tanzania ina gesi asilia na pia mafuta yamegundulika sehemu nyingi duniani ikiwemo nchi jirani ya Uganda na kuwa popote penye gesi asilia pana mafuta?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Jerome Lyimo (Viti Maalum) lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme pasipo na utata wa aina yoyote kwamba uzalishaji wa kilimo kwa malengo ya kuzalisha chakula utapewa kipaumbele na Serikali itaendelea kuhimiza wakulima kwanza kujiwekea usalama wa vyakula (*food security)* halafu kutenga ziada kwa malengo ya biashara. Mtazamo huu wa mkulima mmoja mmoja ukijumuishwa, unatoa msimamo wa taifa kuhusu suala la *biofuel.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli uzalishaji wa mazao ya *biofuel* usiporatibiwa kwa ufanisi unaweza kuwa na ushindani mkubwa na uzalishaji wa chakula, kitu ambacho kinaweza kusababisha uhaba wa chakula nchini. Serikali kupitia Kamati Maalum ya *Biofuel* tayari imeandaa rasimu ya mwongozo wa masuala ya biofuel ambapo unaelekeza kuwepo uwiano kati ya uzalishaji wa mazao kwa ajili ya chakula na kwa ajili ya nishati *(biofuel).*

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia vipaumbele vya kitaifa, utekelezaji wa mwongozo huu utasimamiwa kwa makini na Serikali ili kuhakikisha maelekezo yaliyopo yanazingatiwa.

Pamoja na kwamba biashara ya *biofuel* ni huria kama ilivyo kwenye bidhaa za mafuta ya petroli; na kwa vile biofuel inawakilisha chanzo cha nishati mbadala, ni jukumu la Serikali kuhakikisha masuala ya kuendeleza *biofuel* yanatekelezwa kwa kuzingatia maslahi ya nchi, wakiwemo wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha uwepo wa soko la kudumu la biofuel, Serikali itasisitiza uzalishaji nishati hiyo kwa ajili ya soko la ndani ikiwa ni pamoja na kutumia katika magari mashine na viwanda vya hapa nchini. Hata hivyo fursa za soko la nje ya nchi zitaangaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutathimini masuala mbalimbali ya kiuchumi, kijamii na kimazingira, Serikali kwa kutumia vyombo vyake vya uchumi itaamua ni chanzo kipi cha mafuta kitumike kulingana na hali ya soko la nje na la ndani kwa wakati huo.

Mfano mzuri ni nchi ya Brazil ambayo inazalisha mafuta ya petroli, gesi asilia na mafuta ya mimea kwa wingi ambapo huamua kiwango cha uzalishaji kwa kuzingatia hali halisi ya soko na hivyo kuifanya nchi kuwa na uhakika wa upatikanaji wa nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua kuwa mafuta ya petroli yana ukomo, upo umuhimu kwa Tanzania kuandaa mikakati itakayohakikisha kuwa mafuta yatokanayo na mimea yanatumika kwa pamoja na yale ya petroli kwa kuruhusu viwango muafaka vya uchanganyaji *(blending*).

Serikali kupitia Kamati niliyoitaja inazingatia masuala yote ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyagusia.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Waziri Mkuu amejibu swali la namna hii leo kwa ufasaha mkubwa naomba niulize swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imeandaa rasimu ya mwongozo wa masuala ya *biofuel* ambayo itaelekeza uwiano kati ya mazao ya chakula na mazao ya *biofuel*. Naomba kuiuliza Serikali kama itakuwa na mpango wa kuleta rasimu hiyo hapa Bungeni ili tuweze kuiona na kujua huo uwiano.

Je, Waziri anaweza kutuletea rasimu hiyo ili Wabunge tuione?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kujibu maswali ya biofuel ambayo kusema kweli yamepunguza kwa kiasi kikubwa majibu niliyokuwanayo hapa. Nadhani ni jambo la msingi, tunalikubali kwamba Kamati ya Kitaifa ya *Biofuel* inaendelea na kazi na tutakapokamilisha rasimu hiyo tutaileta Bungeni kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda umekisha. Sasa matangazo ya wageni. Leo katika Ukumbi wetu wa Bunge leo hii tuna Wabunge wenzetu kutoka Bunge la Jamhuri ya Nigeria ambao ni Makamishna Wabunge. Hao ni Mheshimiwa Saada Aminu, Kamishna na Kiongozi wa Msafara, *can you please stand up.* Mwingine ni Mheshimiwa Kamishna Anochia, wameongozana na *Assistant Director, Administration and Personnel* Al Haji Maaj. *We are very happy to meet you and I am sure we are going to share your experience on the Commission of The Parliament because we have also something to learn from you*. (*Makofi*)

Baada ya hapo tuna mgeni mwingine katika Ukumbi wa Spika huyu ni Bwana Mark Ashust yeye ni Mkurugenzi kutoka *Africa Research Institute*. *You are welcome*. *(Makofi)*

Wageni wa Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, kwanza kabisa ni Bwana Patrick Mwangunga ambaye ndiye mume wake Mheshimiwa Waziri ambaye anawasilisha hotuba yake leo. Pia kuna Daudi Mwangunga ni Ndugu yake Bwana Patrick. (*Makofi*)

Napenda kuwataja wageni wengine kwa sababu muwafahamu maana yake ndiyo mtakuwa mna-*network* nao. Kwanza kabisa ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii Bi. Blandina Nyoni, mwingine ni Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Hifadhi za Taifa *TANAPA* Bwana Modestus Ilungulu. Mwingine ni Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Utalii wa Wanyamapori Profesa Gabriel Mbasa, mwingine ni Mkurugenzi wa Sera na Mipango Bwana Tadeus Kilenga huyu alikuwa Msaidizi wangu nilipokuwa Waziri.

Mwingine ni Mkurugenzi wa Mambo ya Kale Bwana Donatius Kamamba na mwingine ni Mkurugenzi wa Misitu na Nyuki Dr. Felician Kilahama, mwingine ni Mkurugenzi wa Wanyamapori Bwana Erasmus Tarimo. Mwingine ni Mkurugenzi wa Utalii Bi. Maria Mmari na mwingine ni Kaimu Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Bi. Edita Beda, (*Makofi*)

Mwingine ni Mkurugenzi Mkuu Shirika la Hifadhi za Taifa Bwana Gerald Digurube, mwingine ni Mkurugenzi Mtendaji Bodi ya Utalii Bwana Peter Mwinguo, mwingine ni Mtendaji Mkuu Wakala wa Chuo cha Utalii cha Taifa Bi. Agnes Mziray, mwingine ni Mkurugenzi Mkuu Makumbusho ya Taifa Dr. Nobert Kayombo, mwingine ni Kaimu Mkurugenzi Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori *TANAPA* Dr. Saimon Mduma, mwingine Mkurugenzi Mkuu Taasisi ya Utafiti wa Misitu *TAFORI* Dr. Ladislau

Ishubemki na Kaimu Mhifadhi Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro Bwana Benard Mrunya. (*Makofi*)

Wengine ni Mtendaji Mkuu Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania, Ndugu Heriel Petro Msanga na Mkuu wa Chuo cha Wanyamapori Mweka Bwana Emmanuel Savere.(*Makofi*)

Kwa niaba ya Wabunge naomba kuwapa pole kwa msiba uliowapata wiki iliyopita.

Halafu tunawageni wengine kutoka Ubalozi wa Uholanzi hapa yupo *First Secretary* Hesen Samsen, tuna *Policy Officer Governance* Joseph Kitama na Afisa mwingine ni Erick Rock. *Am sure I couldn't pronounce your names properly*. (*Makofi*)

Halafu tuna mgeni wa Mheshimiwa Faida Mohamed Bakari ni mdogo wake Bi Riziki Abdallah Ali. Tuna wageni wa Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya Ndugu Said Mkesha na Dalia Mkesha ambao ni watoto wa kaka yake.

Halafu tuna wageni wa Mheshimiwa Sevelina Mwijage ni Mama Catherine Mwijage ambaye ni mama yake mzazi; yupo wapo mama? Yule pale hongera sana na Stella Silvanus na Halima Silvanus watoto wake. Karibuni sana hasa mama maana yake kufika hapa ni jambo zuri. (*Makofi*)

Tunao Wanafunzi 50 kutoka *City Secondary* pamoja na Walimu wao; hii shule ipo Dodoma ahsateni. Tunao wanafunzi 50 kutoka Dodoma Sekondari na wenyewe wasimame na Walimu wao. Tunao wanafunzi kutoka *DCT Mvumi Secondary* na wenyewe wasimame. Tunawashukuru wanafunzi wote kwa sababu ni sehemu ya masomo yenu. *(Makofi)*

Halafu tuna wageni 15 kutoka Kanisa la Biblia Dodoma wote wasimame walipo. *Oky* hawajafika. Halafu wanafunzi 30 na Walimu sita kutoka *Retreewood Nursery and Primary School* kutoka Dar es Salaam wako wapi? Nadhani hawajafika labda kesho. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tuna shughuli za kazi; kwanza kabisa kutakuwa na Kikao cha pamoja kati ya Kamati ya Uongozi na Tume ya Huduma za Bunge leo saa saba na nusu mchana katika Ukumbi wa Mikutano wa Spika.

Mheshimiwa Gideon Cheyo,  Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji anaomba niwatangazie Wajumbe wake kwamba leo saa tano na nusu wakutane katika ukumbi Namba 231.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Wilson Masilingi anaomba niwatangazie Wajumbe wake kwamba saa tano asubuhi hii wakutane katika ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge baada  ya hapo tunaendelea na kazi. Katibu  endelea na *Order  Paper.*

## KAULI   ZA   MAWAZIRI

### Ununuzi wa Pamba Msimu Mwaka 2008/2009

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kauli ya Serikali kuhusu msimu wa ununuzi wa pamba mwaka 2008/2009. Kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2007, Kanuni namba 49, naomba kutoa Kauli ya Serikali kuhusu msimu wa ununuzi wa pamba mwaka 2008/2009 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nitoe taarifa fupi kuhusiana na ununuzi wa zao la pamba unaoendelea hivi sasa hususan katika Mikoa ya Ziwa, ile ya Kati na Magharibi. Kama wote tunavyojua, zao la pamba ni moja ya mazao makubwa ya kilimo ambayo huchangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi na pia katika kulileteа taifa fedha za kigeni.

Pamoja na ukweli huo ununuzi wa zao la pamba msimu huu umekuwa wa kusuasua sana ukilinganisha na hali ilivyokuwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na bei nzuri ya pamba kwa mkulima mwaka 2007/2008 iliyotokana hasa na ushindani wa haki katika soko la pamba wakulima wa pamba wameitikia wito na kuongeza uzalishaji  wa  zao hilo.

Msimu uliopita soko lilianza na bei ya shilingi 350/- kwa kilo na kuongezeka hadi shilingi 500 mpaka 550/- kwa kilo ya pamba ya mbegu. Kutokana na motisha wa bei uzalishaji wa pamba msimu wa 2008/2009 umeongezeka kutoka tani 262,000 zilizozalishwa msimu wa 2007/2008 hadi tani 432,000 au mara mbili.

Waheshimiwa Wabunge mtaungana nami katika kuwapongeza sana wakulima wa pamba kwa mafanikio hayo.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia mafanikio yaliyopatikana msimu wa 2007/2008 maandalizi ya msimu huu yalianza kwa Bodi ya Pamba kuitisha mkutano wa wadau ambao ulifanyika tarehe 7 Juni, 2008 Mjini Shinyanga.

Mkutano huo uliitishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bodi ya Pamba namba 2 ya mwaka 2001 kifungu 5 (1) (f) ambacho kinasema *"To ensure competition fair trade and to set, monitor and indicative prices as established market forces."* Sheria hii inatoa fursa kwa wadau wa pamba kushauriana na kukubaliana kuhusu bei dira ya ya kuanzia msimu. Wadau waliokutana ni kutoka *Tanzania Cotton Growers Association TACOGA, Tanzania Cotton Association* huu ni Ushirika wa Wanunuzi, Bodi ya Pamba pamoja na uwakilishi wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Katika Mkutano huo mapendekezo ya bei ya kuanza msimu huu yalikuwa kama ifuatavyo:-

*Tanzania Cotton Association* walipendekeza shilingi 362/- kwa kilo. *Tanzania Cotton Growers* walipendekeza shilingi 400/- na Bodi ya Pamba ilipendekeza shilingi 470/- kwa kilo/-

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majadiliano marefu wadau walikubaliana bei ya dira iwe shilingi 400 kwa kilo ya kuanzia. Hata hivyo mchanganuo wa bei ya pamba katika Masoko ya Dunia ulionyesha kuwa bei ya Mkulima kwa pamba ya mbegu ingeweza kufikia shilingi 455.35/- kwa kilo kwa kutumia bei ya *cent 60* kwa ratili kwa dola za Marekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msimu wa ununuzi wa pamba 2008/2009 jumla ya makampuni 39 yamesajiliwa kununua pamba ikilinganishwa na makampuni 43 yaliyonunua pamba msimu wa 2007/2008. Tangu msimu uzinduliwe rasmi takriban wiki tatu zilizopita bei ya pamba imebakia kuwa shilingi 400/- kwa kilo ya pamba mbegu iliyokubaliwa kufungua msimu kwa makampuni yote 39 katika maeneo yote ya Kanda ya Magharibi yanayolima pamba nchini.

Hali hii ni pamoja na ukweli kwamba bei ya pamba kwenye soko la kimataifa imekuwa zaidi ya senti 60 za dola ya Kimarekani kwa ratili ya pamba nyuzi iliyotumika kukokotoa bei ya kuanzia msimu wa 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika kwa hakika mwenendo huu wa bei unatia shaka kwani kwa miaka yote ya nyuma ambapo utaratibu huu ulitumika kulikuwepo bei zilizotofautiana baina ya wanunuzi na baina ya maeneo. Wasiwasi wetu unatokana na sababu za msingi zifuatazo.

Kabla na baada ya Kikao cha tarehe 7 Juni, 2008 ambapo shilingi 400/- ilikubaliwa kuwa bei dira ya kuanzia bei ya pamba katika soko la kimataifa imeendelea kuwa juu ya senti 60 za dola ya Kimarekani kwa ratili ya pamba nyuzi. Hii ina maana kwamba wakulima wanastahili kulipwa zaidi ya shilingi 400/- kwa kilo ya pamba mbegu.

Haiyumkiniki kwamba makampuni yote 39 yaliyosajiliwa kununua pamba yana gharama sawa za uendeshaji na yanauza pamba kwa mkataba mmoja na hivyo kulipa shilingi 400/- tu. Ukweli ni kwamba kila kampuni huuza pamba peke yake na yapo makampuni ambayo yameuza pamba kwa bei kubwa kuliko senti 60 za dola za Kimarekani kwa ratili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kutoonekana kabisa kwa hali ya ushindani katika soko la pamba tangu msimu uanze Bodi ya Pamba iliitisha tena Mkutano wa wadau tarehe 7 Julai, 2008. Mkutano huo ulihudhuriwa na Wajumbe wa *TCA*, *TACOGA* Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika pamoja na Bodi ya Pamba. Matokeo ya Mkutano huu wa pili yanaonyesha kuwa kimsingi Wajumbe bado wanakubaliana na vigezo vilivyotumika katika kukokotoa bei ya mkulima ya shilingi 400/- kwa kilo na kuafiki bei hiyo iendelee kutumika katika ushindani wa soko.

Hii ina maanisha kwamba mkulima anaweza kulipwa zaidi ya shilingi 400/- kwa kilo ya pamba mpaka sasa. Hata hivyo Chama cha Wafanyabiashara wa Pamba kilieleza sababu kubwa ambazo zinasababisha bei kutoongezeka kuwa ni Halmashauri za Wilaya kuweka masharti mengi na magumu kwa wanunuzi wa pamba. Baadhi ya masharti hayo ni pamoja na baadhi ya Wilaya kama ifutavyo:-

(i) Kurejeshwa kwa ushuru wa elimu ambao ulifutwa. Kwa mfano Meatu wanadai shilingi 10/- kwa kila kilo ya pamba wakati Maswa wanadai shilingi 5/-.

(ii)Kuanzishwa kwa ada za leseni za vituo vya kununulia pamba. Kwa mfano Wilaya ya Bukombe inahitaji kulipwa shilingi 10,000/- kwa kila kituo wakati Wilaya ya Kahama inatoza shilingi 2,500/- kwa kila kituo. Hili linafanyika pamoja na kuwepo na leseni kutoka Bodi ya Pamba ambayo hailipiwi.

(iii)Halmashauri za Wilaya zinadai ushuru wa Pamba ulipwe kabla ya kununua pamba; na kwamba pamba hairuhusiwi kutoka vijijini bila ya kulipa fedha za ushuru. Aidha Wilaya ya Maswa haipokei hundi wanataka malipo yote wanataka yawe kwa fedha taslimu.

(iv)Baadhi ya Wilaya kuzuia baadhi ya wanunuzi kununua pamba katika Wilaya husika bila sababu za msingi. Mfano Wilaya ya Bariadi imezuia baadhi ya wanunuzi kuanza kununua pamba.

(v)Wilaya ya Kishapu kuamua kuongeza ushuru wa vyama vya msingi hadi kufikia shilingi 25, 000/- bila sababu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na sababu hizi katika maeneo mengi wanunuzi walioruhusiwa na ambao ndiyo wameanza kununua pamba ni wachache sana hali ambayo inaathihiri ushindani. Kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kutamka

kuwa Halmashauri haziruhusiwi kutoza ushuru wa mazao ambao ni zaidi ya asilimia 5 ya bei ya Mkulima ambayo ina ruhusiwa na Sheria. (Makofi)

Aidha Halmashauri zisitishe taratibu na masharti yote yaliyopo hivi sasa na ambayo yanadhoofisha nguvu ya ushindani wa soko. Pia ninapenda kutoa wito kwa makampuni na vyama vya ushirika vinavyonunua pamba kuwa watumie vizuri fursa ya ushindani wa soko kulipa wakulima bei nzuri zaidi kwa sababu takwimu za bei ya soko la pamba zinaonyesha kuwa hilo linawezekana.

Bei waliyokubaliana wadau ya shilingi 400/- kwa kilo ya pamba mbegu ni ya kufungua msimu na sio bei ya kudumu kwa msimu mzima. Serikali inaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa bei wanazolipwa wakulima ili kuhakikisha kuwa wakulima wanalipwa bei ya haki kwa jasho lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendelea kuwalipa bei ya chini wakulima kunawapunguzia ari na motisha na kurudisha nyuma shabaha ya Serikali ya kuongeza uzalishaji ili kufikia marobota milioni moja na nusu ifikapo mwaka 2010. Serikali inatambua kuwa wanunuzi ni wadau katika Maendeleo ya wakulima. Kudhoofisha uzalishaji kunafanya hata biashara zao kutokuwa endelevu.

Kwa msingi huo narudia kuwataka washindane katika bei badala ya kushirikiana kuweka bei. Aidha wanunuzi wanapaswa wawalipe wakulima bei nzuri ili zao la pamba liwe endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa taarifa hiyo na nina hakika Mheshimiwa Mzee Cheyo amefurahi. Katibu kwa shughuli inayofuata kwenye *Order Paper*.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009
### Wizara ya Maliasili na Utalii.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira iliyowasilishwa leo juu ya makadirio na matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka 2008/2009; naomba kutoa Hoja kuwa Bunge lako Tukufu sasa likubali na

kujadili na kupitisha Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Job Ndugai Mbunge kwa ushirikiano walioutoa kwa Wizara katika kutekeleza majukumu yake. Wizara imezingatia mapendekezo yaliyotolewa na Kamati, na itazingatia pia yale yatakayotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa kuchangia hoja ninayoiwasilisha katika Bunge hili.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani aliyonayo kwangu  kwa kuniteua na kunikabidhi dhamana ya kuongoza Wizara ya Maliasili na Utalii.

Naomba pia kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika. Ni dhahiri kuwa uteuzi wake ni kielelezo cha imani kubwa waliyonayo kwake viongozi wa Bara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Mizingo Kayanza Pinda Mbunge wa Mpanda Mashariki na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuteuliwa kwake na Mheshimiwa Rais na baadaye kuthibitshwa kwa kura za kishindo na Bunge letu Tukufu kushika wadhifa huu mkubwa. Kuteuliwa kwake na baadae kuthibitishwa na Waheshimiwa Wabunge kunadhihirisha imani kubwa waliyonayo Mheshimiwa Rais na wananchi juu ya uwezo wake na utendaji kazi katika kusimamia majukumu ya Serikali. Namtakia mafanikio katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matukio muhimu. Kabla sijatoa matukio muhimu yaliyotokea katika mwaka wa fedha 2007/2008, kwa masikitiko makubwa ninaomba kutoa taarifa kwa Bunge lako Tukufu kuwa Mnamo tarehe 3/7/2008 kwenye majira ya kati saa sita na nusu na saa saba mchana Wizara yangu ilipoteza Maafisa Wakuu watatu wa wa Idara ya Wanyamapori akiwemo Mkurugenzi  Msaidizi katika ajali mbaya ya ndege ndogo ya Wizara iliyotokea maeneo ya Mlima Monduli Mkoani Arusha.

Maafisa hao walikuwa wanaelekea Loliondo Wilayani Ngorongoro kikazi. Wizara yangu itawakumbuka watumishi hao kwa kazi kubwa waliyoifanya hususani katika sekta ndogo ya wanyamapori. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi amina.

Mheshimiwa Naibu Spika,  Katika mwaka 2007/2008 matukio muhimu katika Wizara ni kama yafuatayo:-

(i) Wizara ilifanya mabadiliko katika ngazi za Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi na maafisa mbalimbali waandamizi ikiwa ni pamoja na kuwahamisha watumishi ambao wamekaa kwenye kituo kimoja kwa muda mrefu ili kuboresha utendaji na kuongeza ufanisi wa kazi.

(ii) Tanzania iligombea na kuchaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Kituo cha Kimataifa cha Mafunzo ya Urithi wa Utamaduni kilichopo Roma-Italia. Nafasi hii itasaidia Tanzania kunufaika katika uhifadhi wa urithi wa utamaduni kwa kuwezeshwa kifedha na kitaalam.

(iii) Nchi yetu ilikuwa mwenyeji wa mkutano wa 33 wa Chama cha Wakala wa Usafirishaji Watalii *(Africa Travel Association - ATA).* Mkutano huo ulifanyika Arusha mwezi Mei, 2008 na kuhudhuriwa na wajumbe wapatao 400 kutoka Bara la Amerika, Ulaya, Asia, na Afrika. Katika Mkutano huo Tanzania ilichaguliwa kuwa Rais wa Chama hicho na mjumbe wa Bodi ya Kamati ya Utendaji ya *ATA* kwa kipindi cha miaka miwili ijayo. Mkutano uliambatana na maonyesho ya utalii na sanaa za mikono ambapo kampuni 45 zilishiriki. Manufaa yaliyopatikana kutokana na Mkutano huo ni pamoja na Tanzania kukuza utalii wake kupitia Wakala wa Wasafirishaji Watalii na Wanahabari waliohudhuria, kuanzisha na kuimarisha mikataba ya kibiashara baina ya wafanyabiashara wa Tanzania na wenzao wa Marekani na kufungua rasmi tawi la *ATA* hapa nchini *(ATA Tanzania Chapter*) ili kuimarisha uhusiano ulioanzishwa baina ya Wakala wa Utalii wa Marekani na Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya Utekelezaji kwa Mwaka 2007/2008 na Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2008/2009. Naomba kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kwa mwaka 2007/2008 na mpango wa maendeleo na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2008/2009 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ndogo ya Wanyamapori . Wizara iliendelea na jukumu la kuhifadhi na kulinda wanyamapori na mazingira yao pamoja na kusimamia matumizi endelevu. Jukumu hili lilitekelezwa kwa kushirikisha wadau mbalimbali, wakiwemo washirika wa maendeleo, wananchi waishio kandokando ya maeneo ya hifadhi, mashirika yasiyo ya kiserikali na sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera na Sheria. Katika mwaka 2007/2008, Wizara ilipanga kuwasilisha muswada wa Sheria ya Wanyamapori. Hata hivyo, muswada huu haukuweza kuwasilishwa kama ilivyokusudiwa kutokana na hatua zilizochukuliwa za kuwashirikisha wadau wengi zaidi katika mchakato wake.

Sasa napenda kuliarifu Bunge lako kwamba muswada huo utawasilishwa katika mwaka huu wa fedha wa 2008/2009. Aidha, ili kuratibu utalii wa wanyamapori nje ya Hifadhi za Taifa na eneo la Hifadhi la Ngorongoro, Wizara iliandaa Kanuni za matumizi ya wanyamapori yasiyo ya uvunaji, zitakazotumika katika maeneo hayo kuanzia mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Usimamizi na Matumizi Endelevu ya Rasilimali . Katika kuongeza mchango wa sekta kwenye pato la taifa, Wizara ilifanya marekebisho

kwa kuongeza viwango vya ada mbalimbali katika tasnia ya uwindaji wa kitalii. Makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2007/2008, yalikuwa Shilingi 48,694,840,000.

Pamoja na makadirio hayo, ilidhihirika kuwa viwango vipya vya ada za uwindaji wa kitalii havikuweza kuhimili ushindani katika soko. Kutokana na hali hiyo, Wizara ililazimika kufanya marekebisho ili kuendana na hali halisi. Marekebisho hayo yalipunguza makadirio ya mapato ya awali kwa asilimia 38. Katika kujenga mazingira mazuri zaidi ya kuongeza kiwango cha mapato yatokanayo na tasnia ya uwindaji wa kitalii, Wizara yangu inafanya tathmini ya vitalu vya uwindaji wa kitalii kwa ajili ya kupata takwimu za rasilimali iliyopo, kujua thamani halisi kulingana na soko na kuweka utaratibu bora zaidi wa kugawa vitalu mara muda wa ukodishaji utakapomalizika Desemba, 2009. Matokeo ya zoezi hili yataiwezesha Wizara kupata thamani halisi ya vitalu katika maeneo yenye madaraja mbalimbali ya uhifadhi ili kuwezesha kupanga viwango stahili vya ada katika tasnia hii ya uwindaji wa kitalii.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ulinzi wa Wanyamapori. Jukumu la ulinzi wa wanyamapori lilitekelezwa na Wizara kwa kuendesha doria ya jumla ya siku za doria 132,884 ndani na nje ya mapori ya hifadhi. Katika kuimarisha doria na kuifanya iwe endelevu; watumishi 236 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi kwa mpangilio ufuatao: Intelijensia (22), matumizi ya "*Geographical Information System*" (23), nidhamu na ukakamavu (165), uendeshaji wa mashtaka (18), utunzaji wa ghala na uhasibu (8).

Aidha, ndege mpya aina ya *Cessna Grand Caravan* yenye uwezo wa kubeba askari 13 kwa wakati mmoja imenunuliwa na imeanza kutumika mwezi Mei, 2008. Ni matumaini ya Wizara kuwa ndege hii itasaidia sana katika shughuli za uhifadhi, kama kitendea kazi muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwaka 2007/2008, Wizara ilikamata watuhumiwa 4,653 wa ujangili na makosa mbalimbali ya ukiukaji Sheria. Kesi 1,393 zilifunguliwa katika mahakama mbalimbali na kati ya hizo, kesi 390 zilimalizika kwa watuhumiwa 811 kukiri makosa na kulipa faini ya jumla ya Shilingi milioni 55.9. Watuhumiwa 119 walifungwa jela kwa jumla ya miezi 1,250 na watuhumiwa 20 waliachiwa huru.

Aidha, silaha mbalimbali zilikamatwa ikiwa ni pamoja na bunduki 202, risasi 594 na silaha nyinginezo (mitego, nyaya, panga, mishale na kadhalika.) 126,260.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vifaa na mali nyingine zilizokamatwa ni pamoja na magari 65, ng'ombe 36,158, baiskeli 239 na mbao 113,495. (*Makofi*)

Kazi ya ulinzi wa wanyamapori inakabiliwa na changamoto kubwa kama vile, majangili kutumia silaha mbalimbali, zikiwemo za kivita. Matumizi ya silaha hizo

yamesababisha kujeruhi na hata kuwaua watumishi waliokuwa katika majukumu yao ya kulinda rasilimali ya wanyamapori.

Katika kipindi cha Januari hadi Aprili, 2008, watumishi wanne waliuawa na wengine watatu kujeruhiwa katika Mapori ya Selous, Moyowosi, Mkungunero na Ikorongo.

Kwa niaba ya Wizara, napenda kutoa pole kwa familia za watumishi hao na Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ulinzi wa Maisha ya Watu na Mali. Katika mwaka 2007/2008, Wizara iliendesha doria za msako wa wanyamapori wakali na waharibifu katika Wilaya za Karagwe, Pangani, Rombo, Manyoni, Nzega, Tunduru, Nachingwea, Masasi, Nanyumbu, Serengeti, Bunda na Kondoa. Doria hizo zilihusisha maeneo ambayo tulipokea taarifa za matukio ya simba wala watu. *(Makofi)*

Maeneo hayo ni Wilaya za Singida Vijijini, Manyoni, Tunduru, Mpanda, Sikonge, Simanjiro, Rufiji na Kilwa. Aidha, matukio ya tembo kuharibu mazao yalitolewa taarifa katika wilaya za Karagwe, Bunda, Serengeti, Rombo na Pangani. Kufuatia taarifa hizo, Wizara iliendesha doria za msako na kuua tembo sita (6) na simba saba (7).

Katika kuimarisha uwezo wa kukabili tatizo la wanyamapori wakali na waharibifu, mwaka 2008/2009, Wizara itajenga vituo kwenye maeneo yenye matatizo makubwa, ili kuwezesha kukabiliana na matatizo hayo mapema kabla uharibifu mkubwa haujatokea. Kwa kuanzia, vituo hivyo vitajengwa katika Wilaya za Rombo, Simanjiro na Bunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamba wamekuwa tatizo sugu katika baadhi ya mito na maeneo ya ardhioevu nchini kwa kutishia maisha ya binadamu na mifugo.

Hatua za kukabiliana na tatizo hilo zilichukuliwa kwa kutoa vibali vya kuwinda mamba 1,500 katika Mito ya Ruvuma, Songwe, Ruvu, Rufiji, Malagarasi, Pangani, Ruhuhu, Luhombero, Mara na Kilombero.

Vilevile, vibali vilitolewa kwa ajili ya kuwinda mamba kwenye Maziwa ya Nyasa na Rukwa pamoja na mabwawa ya Nyumba ya Mungu na Mtera.

Katika kipindi cha 2008/2009, Wizara inakusudia kutoa vibali vya kuwinda mamba 1,500 katika maeneo yenye matatizo sugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika kukabiliana na kero ya kuenea kwa Kunguru Weusi hususan katika Jiji la Dar es Salaam, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Manispaa za Wilaya za Dar es Salaam ambazo ni Kinondoni, Ilala na Temeke, Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu katika Nchi za Tropiki (*Tropical Pestcides Research Institute);* Kituo cha Kudhibiti Panya Morogoro *(Rodent Control Centre, Morogoro)* na Shirika lisilo la Kiserikali la Kuhifadhi Maliasili na Mazingira Tanzania (*Wildlife Conservation Society of Tanzania)*, imeendesha zoezi la kuwauwa kunguru weusi kwa kutumia sumu maalum ya aina ya *DRC-1339* na pia kwa kutumia mitengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Mei 2008, jumla ya kunguru 160,231 waliuawa kwa kutumia mitego na sumu. Katika mwaka 2008/2009, Wizara kwa kushirikiana na wadau, inakusudia kuendeleza zoezi la kupunguza idadi ya kunguru weusi, hususan katika Jiji la Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhifadhi Ardhioevu. Katika kuhifadhi ardhioevu, Wizara inatekeleza programu ya usimamizi endelevu wa ardhioevu katika Wilaya 14 za Mikoa ya Mbeya, Kigoma, Arusha, Tabora na Iringa. Mapori ya Akiba ya Mpanga – Kipengele, Ugalla, Moyowosi, Kigosi, Rukwa na Lukwati, pamoja na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ipo katika programu hiyo.

Katika kushirikisha wananchi kwenye utekelezaji wa programu hiyo, Mwaka 2007/2008, vikundi 600 katika Wilaya 10 za Mikoa ya Iringa na Mbeya vilipatiwa mafunzo ya ujasiriamali na kuanzisha miradi 31. Miradi hii inalenga kuongeza kipato na kuhifadhi mazingira ya ardhioevu. Mpango wa usimamizi wa ardhioevu ya Maragalasi - Muyovozi iliyoko Mikoa ya Tabora na Kigoma ulikamilishwa.

Aidha, maeneo ya ardhioevu ya Kilombero na Ziwa Natron yaliendelezwa kwa kukusanya taarifa za msingi za kuwezesha kuandaa mipango ya usimamizi wa maeneo hayo. Katika mwaka 2008/2009, Wizara itaendeleza programu ya kuhifadhi mazingira ya ardhioevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uendeshaji na Usimamizi wa Mapori ya Akiba. Wizara kupitia Idara ya Wanyamapori, inalo jukumu la kusimamia uhifadhi wa mapori ya akiba, kujenga na kuimarisha miundombinu kwenye mapori hayo kwa ajili ya kuendeleza utalii na uhifadhi. Katika mwaka 2007/2008, uhifadhi na uendelezaji wa miundombinu uliathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na ufinyu wa bajeti. Hata hivyo, Wizara iliweza kukarabati kilomita 200 za barabara na viwanja vinne vya ndege katika Mapori ya Akiba ya *Selous* (viwanja vya Mtemere, Kingupira na Matambwe) na Rungwa. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau iliweza kufanya ukarabati wa viwanja vya Maswa, Rukwa – Lukwati, Lukwika – Lumesule na Ugalla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuweka mazingira mazuri ya kazi kwa watumishi walioko katika Mapori ya Akiba. Tumejenga nyumba za kuishi watumishi kwenye Mapori ya Akiba ya Rungwa, Liparamba na zile zinazotumika na Kikosi Dhidi Ujangili katika miji ya Iringa, Mwanza, Bunda, Songea na Tabora. Aidha, ukarabati wa nyumba ulifanywa katika Pori la Akiba la Burigi-Biharamulo na Chuo cha Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara inatarajia kukarabati barabara zenye urefu wa kilomita 900 ndani ya mapori ya akiba, na kukarabati viwanja nane vya ndege kwenye Mapori ya *Selous*, Rungwa – Kizigo – Muhesi na Muyowosi – Kigosi ikiwa ni mkakati wa kupanua na kuboresha shughuli za utalii na kuwezesha ulinzi ndani ya mapori haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara iliahidi kuandaa Mpango wa Usimamizi na Uendeshaji wa Pori la Akiba Maswa. Rasimu ya kwanza ya mpango huo imekamilika.

Katika kipindi cha 2008/2009, Mpango wa Usimamizi na Uendeshaji wa mapori ya Maswa, Ikorongo na Gurumeti utakamilishwa. Aidha, mipango ya mapori ya Ugalla, Rungwa na Mpanga/Kipengele itafanyiwa mapitio.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushirikishaji Jamii na Elimu kwa Umma. Moja ya madhumuni ya Sera ya Wanyamapori ni kujenga uwezo wa wananchi kuhifadhi na kunufaika na rasilimali za wanyamapori waliopo kwenye maeneo ya vijiji. Katika kutekeleza madhumuni haya, mwaka 2007/2008, maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori *(Wildlife Management Areas-WMAs)* na Jumuiya kumi za kusimamia maeneo hayo zilitangazwa. Jumuiya hizo zilipatiwa haki ya matumizi ya wanyamapori hivyo kuziwezesha kuingia mikataba na wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, washiriki 162 kutoka Jumuiya nne walipata mafunzo ya ujasiriamali katika kituo cha ujasiriamali cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mafunzo ya uhifadhi maliasili yalitolewa kwa jumla ya wanavijiji na viongozi wao 547 katika Kituo cha Likuyu-Sekamaganga Wilayani Namtumbo, na Chuo cha Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi Jijini Mwanza.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara kwa kushirikiana na wadau inatarajia kuongeza idadi ya *WMAs*, kwa kuwezesha jumla ya *WMAs* kumi katika Wilaya za Rufiji, Kilombero, Kigoma, Urambo, Longido na Mondulu ili kutangazwa, kuzipatia haki ya matumizi ya wanyamapori, kutoa elimu juu ya sera na kanuni, na mafunzo juu ya ujasiriamali na utunzaji fedha kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa wananchi wanaoishi kwenye maeneo yenye wanyamapori wananufaika na rasilimali hii, Wizara imeendelea kugawana mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii kwenye *WMAs* zenye vitalu vya uwindaji. Mwaka 2007/2008, Jumuiya nane zilipata mgao wa jumla ya Shilingi milioni 201.2, zilizotokana na ada za wanyama waliowindwa kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Uhifadhi wa Wanyamapori Tanzania. Mfuko wa Uhifadhi Wanyamapori Tanzania, ulianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na.21 ya Mwaka 1978 kwa lengo la kuboresha shughuli za uhifadhi wa wanyamapori. Katika mwaka 2007/2008, Mfuko ulikusanya Shilingi bilioni 7.0, ambazo zilitumika kwa kazi za kuimarisha doria ikiwa ni pamoja na ununuzi wa ndege mpya, utafiti na mafunzo, kutoa elimu kwa umma na utawala. Mfuko pia uligharimia kazi za maendeleo katika mapori ya akiba na baadhi ya miradi ya ushirikishaji wananchi katika uhifadhi. Matarajio ya makusanyo katika mwaka 2008/2009 ni Shilingi bilioni nane (8.0) ambazo zitatumika kwa shughuli za kuongeza uwezo wa kulinda wanyamapori, utafiti na mafunzo, kutoa elimu kwa umma, kukarabati miundombinu na utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania. Katika mwaka 2007/2008, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori imeendelea kufanya utafiti katika maeneo mbalimbali na aina za wanyamapori zilizoainishwa kwenye Mpango wa Utafiti. Taasisi ilifanya utafiti wa mwenendo wa magonjwa ya wanyamapori kuhusu vifo vya mbwa mwitu katika Pori Tengefu la Loliondo; kifo cha mtoto wa faru mmoja katika Hifadhi ya Mkomazi; magonjwa yanayoenezwa na kupe katika Kreta ya Ngorongoro; ugonjwa wa nyani katika Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara; na kimeta na sotoka katika Hifadhi ya Serengeti na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la tembo waharibifu nchini linaendelea kufanyiwa utafiti kuhusu jinsi ya kuwadhibiti. Majaribio ya kupunguza tatizo hilo kwa kutumia tumbaku na pilipili yamefanyika katika Wilaya za Serengeti na Bunda. Matokeo ya awali yanaonesha mafanikio ya kuweza kutumia mbinu hiyo kukabili tembo waharibifu. Katika mwaka 2008/2009, Wizara inatarajia kuendeleza mbinu hiyo kwenye maeneo yenye matatizo sugu ya tembo waharibifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utafiti wa Mbwa Mwitu ambao walitoweka katika Hifadhi za Serengeti na Ngorongoro miaka ya mwanzoni mwa 1990 umeanza na unaendelea. Matokeo ya awali yanaonesha kwamba kasi ya kuongezeka kwa wanyama hawa ambao inaaminika walihamia nchi ya jirani inaridhisha.

Aidha, Taasisi iliendelea na ukusanyaji wa taarifa za wanyamapori wa jamii inayokula nyama (kanivora). Kanzidata iliyojengwa ya wanyama hawa inaonesha kuwa zipo spishi 34 zinazopatikana hapa nchini na pia zipo taarifa zaidi ya 7,000 zilizotolewa kuhusu kuonekana kwa wanyama hao (*sightings*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha 2007/2008, Sensa tano za wanyamapori zilifanyika kwenye Mapori ya Akiba ya Ugalla, Muhesi-Kizigo, Hifadhi za Taifa za Mkomazi na Serengeti pamoja na eneo la wazi la Ziwa Natron. Sensa hizo zimeonesha kuongezeka kwa idadi za wanyamapori aina ya nyati, pofu, swala granti, tandala mdogo, swala twiga, swala pala, mbuni, choroa na ngiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha 2008/2009, Taasisi itaendelea na tafiti ambazo hazijakamilika. Vilevile, itafanya kazi za kupitia upya Mwongozo wa kusimamia na kuratibu utafiti wa wanyamapori nchini; kufanya utafiti na kuendesha mafunzo ya ufugaji wa nyuki kwa njia za kisasa; kuidadi wanyamapori katika mapori yote ya akiba, mapori tengefu na maeneo ya wazi ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya ugawaji upya wa vitalu vya uwindaji; na kuendesha mafunzo ya kuidadi wanyamapori kwa wadau wakuu wa sekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maduhuli, katika mwaka 2007/2008, hadi kufikia mwezi Mei, 2008, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya Shilingi 18,353,037,154.52. Katika mwaka 2008/2009, Wizara inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi 29,165,453,000 Ongezeko hili litatokana na marekebisho ya nyongeza ya viwango vya ada katika maeneo mbalimbali ya uwindaji wa kitalii, baada ya kushauriana na wadau mbalimbali katika biashara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi za Taifa. Shirika la Hifadhi za Taifa lina wajibu wa kusimamia na kuendeleza shughuli za uhifadhi wa wanyamapori na mazingira yao ndani ya maeneo yaliyotengwa kisheria kama Hifadhi za Taifa.

Katika kutimiza wajibu huu, Shirika liliendelea kufanya doria za kuzuia ujangili, kuendeleza utalii na kuimarisha miundombinu ndani na nje ya Hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai 2007 hadi Machi 2008, watalii 617,776 walitembelea Hifadhi za Taifa. Hili ni ongezeko la asilimia 10.8 ikilinganishwa na watalii 557,370 waliotembelea hifadhi katika kipindi kama hicho mwaka 2006/2007. Vilevile, Shirika lilikusanya Shilingi bilioni 61.7, ikiwa ni ongezeko la asilimia 6.1 ikilinganishwa na mwaka 2006/2007 ambapo Shilingi bilioni 58.3 zilikusanywa. Mafanikio hayo yalichangiwa kwa kiasi kikubwa na juhudi za kutangaza utalii ndani na nje ya nchi pamoja na uboreshaji wa miundombinu ndani ya hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inathamini mchango wa wananchi katika kutunza na kuhifadhi maeneo yanayozunguka hifadhi zetu za taifa. Katika bajeti za kila mwaka Hifadhi za Taifa hutenga kati ya asilimia saba na nusu (7.5) hadi kumi (10) ya bajeti yake kwa ajili ya miradi ya ujirani mwema. Miradi inayohusika ni ujenzi wa miundombinu na huduma za kijamii kama shule, zahanati, miradi ya maji na nyumba za Walimu.

Katika mwaka 2007/2008, Shirika lilichangia jumla ya Shilingi 3,781,555,203. Fedha hizo zilitumika katika shughuli za kuboresha maisha ya wananchi kwenye vijiji vinavyopakana na hifadhi za taifa, na jumla ya Shilingi bilioni 2.8 zilitumika kusaidia miradi ya maendeleo iliyobuniwa na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyoahidiwa katika Bunge lako mwaka jana, utaratibu wa kutumia *Smart Cards* na *Credit Cards* katika kukusanya mapato ulianza kutumika. Kwa kuanzia, utaratibu huu unatekelezwa kwenye Hifadhi za Serengeti, *Lake*

Manyara, Tarangire na Mlima Kilimanjaro. Katika mwaka wa fedha 2008/2009, utaratibu huu utaendelezwa kwenye hifadhi nyingine zilizobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kuwa hifadhi zetu zinatunzwa na kuendelea kuwa kivutio kikubwa cha watalii wa ndani na nje ya nchi, mipango ya usimamizi wa hifadhi imeandaliwa. Katika mwaka 2007/2008, mpango wa uendeshaji wa Hifadhi za Serengeti na Mikumi ulifanyiwa mapitio. Aidha, zoezi la kuandaa mipango ya usimamizi na uendeshaji wa Hifadhi za Saadani, Mkomazi, Ruaha na Kitulo imepangwa kufanyika mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Shirika la Hifadhi za Taifa linakusudia kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja katika hifadhi zote ili kusaidia shughuli za utalii na utawala, kupanua wigo wa uwekezaji katika hifadhi za kusini mwa nchi yetu; kuendelea kutangaza vivutio vya hifadhi zetu ndani na nje ya nchi kwa kushirikiana na Bodi ya Utalii pamoja na Balozi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro. Mamlaka imepewa jukumu la kusimamia uhifadhi wa maliasili, kutangaza utalii na kuwaendeleza wenyeji wafugaji ndani ya eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.

Katika kipindi cha 2007/2008, Mamlaka ilitekeleza miradi ya maendeleo kwa vijiji vinavyozunguka eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, chini ya programu ya Ujirani Mwema. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa madarasa nane katika Wilaya za Ngorongoro, Monduli na Karatu, ujenzi wa malambo katika Wilaya ya Ngorongoro, ununuzi wa mabati 216, kuweka umeme wa jenereta kwenye shule ya sekondari Loliondo wilayani Ngorongoro na kujenga mfumo wa maji wenye urefu wa kilomita 10 kwenye kijiji cha Makhoromba. Kazi zote hizi ziligharimu mamlaka kiasi cha Shilingi 652,500,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia uamuzi wa kupunguza msongamano wa idadi ya wakazi ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro, Mamlaka kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro, imeendeleza juhudi za kuimarisha miundombinu katika kijiji cha Oldonyosambu, Tarafa ya Sale, ambako wananchi wanaoishi ndani ya eneo la Ngorongoro watahamia kwa hiari. Kiasi cha Shilingi bilioni 1.1 zimetengwa kwa ajili ya kugharimia miundombinu kwenye kijiji hicho katika mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha miundombinu ndani ya eneo la Hifadhi, Mamlaka imekarabati barabara ya Lodoare–Golini yenye urefu wa kilomita 82 kwa kiwango cha changarawe. Aidha, barabara za ndani ya kreta zenye urefu wa kilomita 150 na barabara ya Enduleni–Kakesio yenye urefu Kilomita 45 zilifanyiwa matengenezo kwa kiwango cha changarawe. Vilevile barabara nyingine ya Enduleni–Kakesio yenye urefu wa kilomita 70 na *"View point"–Lemala* yenye urefu wa kilomita 24 zimefanyiwa matengenezo ya kawaida.

Mamlaka imejenga nyumba sita (6) za watumishi zenye uwezo wa kuishi familia 28 katika eneo la Kamyn Estate. Kama ilivyoahidiwa kwenye hotuba ya bajeti mwaka

2007/2008 ujenzi wa ofisi mpya za Makao Makuu ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro uko kwenye hatua za mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wageni waliotembelea Hifadhi ya Ngorongoro katika kipindi cha Julai 2007 hadi Machi 2008 ni 426,230; kati yao 244,379 ni kutoka nje na 181,851 ni watalii wa ndani. Katika kipindi hicho, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro imekusanya kiasi cha Shilingi 31,942,989,130.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Mamlaka inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi 42,336,858,035, na imekusudia kununua helikopta, mitambo ya kutengeneza barabara za hifadhi, vifaa na silaha za kisasa ili kukabiliana na majangili. Aidha, Mamlaka itaanza ujenzi wa ghala la kuhifadhia mahindi kwa matumizi ya jamii iliyo ndani ya hifadhi, ujenzi wa miundombinu kwenye kijiji cha Soitambu, pamoja na kuweka mfumo wa “Smart Card” ili kuboresha na kudhibiti ukusanyaji wa maduhuli ya Mamlaka. Shughuli hizi zitagharimu mamlaka jumla ya Shilingi 19,385,785,598.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ndogo ya misitu na nyuki. Wizara iliendelea na jukumu la kusimamia, kuhifadhi, kutunza rasilimali ya Sekta Ndogo ya Misitu na Nyuki na kukusanya mapato yatokanayo na sekta hiyo. Jukumu hili lilitekelezwa kwa kusimamia shughuli za ugani, kuratibu ushirikishwaji wa wadau, kuweka mipango ya nguvukazi na maendeleo yake, kusimamia na kuratibu shughuli za mafunzo na utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera na Sheria. Katika mwaka 2007/2008, Wizara iliendelea na mchakato wa kupitia Sera ya Taifa ya Misitu ya Mwaka 1998 ili kuendana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kimazingira duniani.

Mchakato huo ulihusisha tathmini ya utekelezaji wa sera hiyo kwa kushirikisha wadau mbalimbali, ili kubaini mafanikio, changamoto na mapungufu yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwaka 2008/2009, Wizara itakamilisha mapitio ya Sera ya Misitu na kuanzisha mchakato wa kupitia Programu ya Taifa ya Misitu na ya Ufugaji Nyuki. Katika kutekeleza zoezi hilo wadau wakuu wa sekta ndogo ya misitu na nyuki watashirikishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika kuongeza uelewa wa wadau kuhusu Sheria za Misitu na Ufugaji Nyuki, Wizara ilichapisha nakala 3,000 za Kanuni na Taratibu za Ufugaji Nyuki na kuzisambaza kwa wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, Usimamizi na Matumizi Endelevu ya Rasilimali. Wizara ilikamilisha Miongozo mbalimbali ya usimamizi wa misitu ambayo ni pamoja na Mwongozo wa kuandaa mpango wa usimamizi wa misitu ya asili; usimamizi misitu shirikishi *(Participatory Forest Management Guidelines)*; tathmini ya athari za mazingira kwa miradi ya kisekta *(Sector Specific Environmental Impact Assessment)*; na Mwongozo wa Wadau kushiriki kwenye usimamizi na uendelezaji wa misitu ya asili na mashamba ya miti. Kukamilika kwa miongozo hii kutaweka mazingira mazuri ya kuimarisha usimamizi endelevu wa rasilimali ya misitu. Aidha, mwongozo wa uvunaji wa misitu na

biashara ya mazao ya misitu unaendelea kutumika kwenye wilaya zenye maeneo ya uvunaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvunaji kwenye mashamba ya miti umetekelezwa kulingana na mpango wa usimamizi wa kila shamba. Aidha, kipaumbele katika ugawaji malighafi kimetolewa kwa wenye viwanda waliotimiza masharti yaliyowekwa. Mwaka 2008/2009, Wizara imekadiria kuvuna kiasi cha meta za ujazo 1,056,105 kwenye mashamba 16 ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka 2007/2008, Wizara ilifanya tathmini ya mfumo wa kanzidata ya misitu na ufugaji nyuki (National Forest and Beekeeping Database). Kazi hii ilifanyika kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo watumishi saba (7) wa Wizara na 150 kutoka halmashauri za wilaya 36 walipatiwa mafunzo kuhusu matumizi ya mfumo huo.

Mwaka 2008/2009, Wizara itaimarisha ukusanyaji na uingizaji kumbukumbu katika kanzidata ya misitu na nyuki. Kazi hii itahusisha wilaya 36 za majaribio na kupanua mfumo huo katika wilaya nyingine 28. Mfumo huu wa kanzidata utaenezwa pia kwenye Taasisi zisizo za kiserikali na Sekta binafsi zilizojikita katika matumizi na biashara ya mazao yasiyo timbau *(non timber products)* ikiwa ni pamoja na asali na nta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uendelezaji wa Mashamba ya Miti. Katika mwaka 2007/2008, Wizara ilikuza miche milioni 6.3 na kuipanda kwenye mashamba 16 ya miti yanayomilikiwa na Serikali. Kiasi cha hekta 4,802.6 za maeneo yaliyokuwa wazi katika mashamba hayo zilipandwa na hekta 4,084 zilipogolewa matawi na kupaliliwa. Aidha, mipaka na barabara za kuzuia moto zenye urefu wa kilometa 2,241.2 zilifyekwa na barabara za ndani ya msitu zenye urefu wa kilomita 1,233.9 zilitengenezwa.

Mwaka 2008/2009, mashamba 16 ya miti ya Serikali yataendelea kuhudumiwa kikamilifu na maeneo yote ya wazi kwenye mashamba hayo yatapandwa miti. Aidha, Wizara inatarajia kuotesha jumla ya miche 9,819,900 ambayo itapandwa katika hekta 6,933 kwenye mashamba yote ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tathmini ya Rasilimali. Tathmini ya miti ya kupandwa katika mashamba 16 ya Serikali inaendelea ili kupitia upya na kutayarisha mipango ya usimamizi wa mashamba hayo. Mwaka 2007/2008, Wizara kupitia Mradi wa Hifadhi na Uendelezaji Misitu *(Tanzania Forest Conservation and Management Project)* ilifanya makadirio ya ujazo wa miti iliyosimama. Kazi hiyo ilifanyika kwenye Shamba la Miti la Sao Hill lenye ukubwa wa hekta 42,000 na kubaini kuwepo kwa meta za ujazo 10,284,951 ya miti ya Misindano na Mikaratusi. Mradi uliwezesha tathmini ya msitu wa asili wa Angai ulioko Wilaya ya Liwale wenye ukubwa wa hekta 138,000. Takwimu hizo zinachakatwa ili kubaini ujazo wa aina mbalimbali za miti zilizopo kwenye msitu huo na kuweza kupanga mipango bora ya matumizi endelevu ya msitu huo.

Aidha, Wizara ilipima na kuchora ramani za misitu 18 ikiwemo misitu ya hifadhi inayosimamiwa na Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na ile ya Ushirikishaji jamii/vijiji.

Misitu iliyopimwa ina eneo la hekta 85,191.6 katika Mikoa ya Morogoro (misitu 4), Tanga (msitu 1), Iringa (msitu 1), Singida (msitu 1) na Mbeya (misitu 11).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Finland na Benki ya Dunia iliandaa Mradi wa Kitaifa wa Tathmini ya Rasilimali za Misitu *(National Forest and Ecosystem Inventory)*. Madhumuni makubwa ya mradi huu ni kubainisha rasilimali za misitu tulizo nazo nchini ambazo zipo hatarini kutoweka, zile zinazoweza kuvunwa na kuona uwezekano wa biashahara ya hewa mkaa *(carbon trade)* inayotokana na misitu yetu kunyonya hewa ya *carbon*. Aidha, mradi huu utasaidia katika kupanga, kusimamia kuwa na matumizi endelevu ya Misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ulinzi wa Rasilimali. Katika kulinda rasilimali za misitu na nyuki, Wizara iliendelea kuimarisha vikosi vya doria na kuvijengea uwezo. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara ilianzisha vikosi viwili vya Kanda ya Ziwa (Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Kagera na Mara) na Kanda ya Kaskazini (Mikoa ya Arusha, Tanga na Kilimanjaro). Aidha, Wizara ilinunua boti mbili ziendazo kasi ili kudhibiti watoroshaji wa mazao ya misitu kupitia baharini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhakiki na ukaguzi wa viwanda vya uchakataji wa mazao ya misitu ulifanyika Mkoani Dar es Salaam na kubaini kuwa viwanda vingi vinaanzishwa bila kufuata vigezo vilivyowekwa na Serikali. Aidha, baadhi ya viwanda hivyo ni vichakavu, havikidhi viwango vilivyowekwa kwenye mwongozo wa uvunaji endelevu na havina wafanyakazi wenye sifa zinazotakiwa, hivyo kutoa mazao yasiyokidhi ubora unaotakiwa.

Baada ya ukaguzi huo, Wizara ilikutana na wenye viwanda na kutoa maelekezo kuhusu kuboresha viwango na ubora wa mazao ya misitu; utunzaji kumbukumbu na umuhimu wa kuwa na watumishi wenye sifa na ujuzi pamoja na kutumia teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ili kuongeza pato la Taifa kutokana na Sekta ya Misitu, Wizara ilielekeza wawekezaji waanzishe viwanda vya kuchakata magogo hapa nchini na hatimaye wasafirishe bidhaa iliyokamili kama vile samani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara itaanzisha vikosi vitatu vya doria katika Kanda ya Kati (Mikoa ya Dodoma, Manyara na Singida), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mikoa ya Mbeya na Iringa) na Kikosi maalum kwa ulinzi wa baharini. Aidha, mafunzo yatatolewa kwa Maafisa Misitu 58 kwa ajili ya kuanzisha vikosi hivyo. Ofisi nyingine za kudumu zinatarajiwa kujengwa katika vituo vya ukaguzi wa mazao ya misitu vya Kamanga na Ukiliguru Mkoani Mwanza. Vilevile, ukaguzi wa viwanda vya mbao utaendelezwa katika mikoa yote nchini. Wizara imeandaa utaratibu wa kusajili upya viwanda ambao utazingatia uwekezaji na teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Ardhi na Vyanzo vya Maji. Utunzaji wa vyanzo vya maji ulifanyika ikiwa ni pamoja na uhakiki wa mipaka ya misitu 30 ya kuhifadhi ardhi na vyanzo vya maji kwa kufyeka mipaka na kupanda miti. Kazi ya

kuwaondoa wavamizi wa misitu katika Mikoa ya Tabora, Kagera, Dar es Salaam, Iringa na Tanga ilifanywa kwa kushirikiana na Polisi, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya. Kutokana na misitu mingi kuathiriwa na tatizo la moto, Wizara iliendelea na kampeni za kuzuia moto kwa kushirikisha viongozi wa Wilaya na Mikoa. Wizara itaongeza juhudi za kuelimisha Umma wa Tanzania ili tatizo la moto liweze kupungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inakamilisha Mpango Mkakati wa Hifadhi ya Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki *(Eastern Arc Mountain Conservation Strategy)* ambayo ni vyanzo muhimu vya mito ya Pangani, Wami, Ruvu, Kihansi, Kilombero, Ruaha ndogo na Rufiji. Mpango huu utatumika kuhifadhi kilometa za mraba 5,400 katika Mikoa ya Iringa, Morogoro, Tanga, Kilimanjaro na Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu huo, misitu 98 iliyopo katika Milima ya Tao la Mashariki imependekezwa kwa Shirika la Dunia la Hifadhi ya Mazingira *(International Union for Conservation of Natural – IUCN)* ili kutambuliwa Kimataifa kama misitu ya hifadhi kwa vigezo vya *IUCN*. Kuhifadhi misitu hii kwa vigezo vya *IUCN* kunaiwezesha Wizara kunufaika kitalaamu na kifedha kupitia mashirika ya Kimataifa ambayo ni washirika wa *IUCN*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya 14 ndani ya eneo la Milima ya Tao la Mashariki mwa Tanzania zimeridhia hatua ya serikali ya kupendekeza misitu hiyo kuwa kwenye orodha ya urithi wa dunia. Eneo hili limewekwa kwenye orodha ya muda ya urithi wa dunia ikiwa ni hatua ya mwanzo ya mchakato wa kukamilisha azma hiyo. Kuiweka misitu hii kwenye orodha ya urithi wa dunia itapanua wigo wa vivutio vya utalii Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uendelezaji Utalii-Ikolojia. Kama ilivyoahidiwa katika Bunge lako mwaka jana, Wizara imefanikiwa kupanua maeneo ya utalii ikolojia *(Eco-tourism)* kwa kupandisha hadhi misitu ya hifadhi ya West Kilombero, Matundu na Lyondo kuwa Hifadhi ya Mazingira Asilia *(Nature Reserve)* ya Kilombero, iliyopo wilayani Kilombero, yenye ukubwa wa hekta 134,511. Vilevile, Msitu wa Hifadhi wa Nilo, wilayani Muheza, umepandishwa hadhi kuwa Hifadhi ya Mazingira Asilia yenye ukubwa wa hekta 6,023. Wizara inakamilisha mchakato wa kuifanya Misitu ya hifadhi za Uluguru Kaskazini, Bunduki na Uluguru Kusini yenye jumla ya hekta 24,000 kupandishwa hadhi kuwa Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Uluguru, Mkoani Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka 2008/2009, Wizara itaendelea na mchakato wa kupandisha hadhi misitu ya Chome (Same), Shume – Magamba (Lushoto), Udzungwa Scarp (Morogoro/Kilolo) na Mlima Rungwe (Rungwe) kuwa Hifadhi ya Mazingira Asilia hivyo kuwa chini ya ulinzi madhubuti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuendeleza Ufugaji Nyuki. Katika kuhakikisha kuwa wananchi wanafaidika na rasilimali za nyuki, mpango kabambe wa kuendeleza ufugaji nyuki umeanza kutekelezwa katika wilaya 30 kwa kutathmini hali halisi ya ufugaji nyuki katika wilaya hizo. Wilaya 15 zimenufaika kwa kuwezeshwa kununua mizinga na vifaa vya ufugaji nyuki vya mfano kwa ajili ya kuchochea utengenezaji wa vifaa hivyo katika

maeneo ya ufugaji nyuki. Jumla ya mizinga 1,000 ya mfano na vifaa vya ufugaji nyuki seti 600 vilitengenezwa. Aidha, vikundi 51 vya wafugaji nyuki vimeanzishwa katika Wilaya hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashamba ya ufugaji nyuki ya mfano yaliendelezwa katika Wilaya za Handeni, Kondoa, Kibondo na Manyoni na vifaa vya ufugaji nyuki vilinunuliwa na kusambazwa katika vituo hivyo. Aidha, maeneo ya hifadhi za nyuki manne yenye ukubwa wa jumla ya ekari 12,290 yametengwa katika Wilaya za Manyoni na Handeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika kipindi cha mwaka 2007/2008, mauzo ya mazao ya nyuki nje ya nchi yalikuwa kiasi cha tani 413.77 za nta zenye thamani ya Shilingi bilioni 2.36 na tani 369.74 za asali zenye thamani ya Shilingi milioni 521.27.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka 2007/2008, Wizara kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali liitwalo *National Honey Show* iliandaa maonesho ya asali yaliyofanyika katika Viwanja vya Bunge - Dodoma. Maonesho hayo yalishirikisha wafugaji nyuki 102 na wataalam 75 kutoka wilaya 24 nchini. Vilevile, Tanzania ilishiriki mkutano wa *Apitrade Africa* uliofanyika nchini Kenya ambao lengo lake lilikuwa ni kuweka mikakati ya kutangaza na kutafuta masoko ya mazao ya nyuki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, mauzo ya mazao ya nyuki nje ya nchi yanakadiriwa kuwa kiasi cha tani 600 za nta na tani 450 za asali zenye thamani ya Shilingi 4,057,432,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ubora wa Mazao ya Nyuki. Tanzania inawajibika kuandaa na kutekeleza mpango wa udhibiti wa mabaki ya kemikali katika asali *(Chemical Residue Monitoring Plan)*. Hatua hii inachukuliwa ili kukidhi ubora wa asali kimataifa. Mwaka 2007/2008, Wizara ilikusanya na kuchunguza sampuli 14 kutoka wilaya za Mpanda, Chunya, Sikonge, Manyoni, Kondoa, Bukombe, Kahama, Uyui na kiwanda cha uchakataji cha *Honeycare Africa (T) Ltd* cha Dar es Salaam. Matokeo ya uchunguzi huo yalionesha kuwa asali ni bora na imekubalika katika soko la Jumuiya ya Ulaya. Aidha, asali kutoka Wilaya ya Manyoni ilipata medali ya dhahabu ya Ubora wa Asali katika soko hilo.

Katika mwaka 2008/2009, Wizara itaongeza idadi ya sampuli zitakazochunguzwa kutoka 14 hadi 60 na itaanzisha vituo kikanda kwa ajili ya kupima ubora na kiasi cha asali kabla ya kuuzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwezesha wazalishaji mazao ya nyuki kukidhi ubora unaotakiwa, Wizara ilitoa mafunzo kwa wadau 708 wakiwemo wataalamu, wafugaji nyuki, wafanya biashara wa mazao ya nyuki na wachakataji. Mafunzo yalihusu kanuni na mbinu bora za ufugaji wa nyuki, ubora, usalama, uhakiki na mfumo wa ufuatiliaji asali. Washiriki walitoka Wilaya za Sikonge, Urambo, Bukombe, Kahama, Kibondo, Nkasi, Mpanda, Chunya, Kondoa, Handeni na Manyoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo hayo yalitolewa kwa kushirikiana na Shirika la Utafiti wa Viwanda na Biashara *(TIRDO*), Shirika la Viwanda Vidogo vidogo *(SIDO)*, Kampuni ya Ufuatiliaji Ubora wa Mazao ya Chakula *(Traceability Tanzania Ltd)* na Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara itaanzisha mchakato wa kuandaa mfumo wa kufuatilia ubora wa asali kuanzia kwenye uzalishaji, usindikaji, uchakataji na usambazaji wa asali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushirikishaji Jamii na Elimu kwa Umma. Katika mwaka 2007/2008, Wizara iliendelea kuwezesha, kuratibu na kutekeleza mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwenye vijiji 1,821 katika wilaya 59 zenye jumla ya hekta 3,672,854. Kati ya vijiji hivyo, vijiji 1,102 vinasimamia misitu ya jamii *(Community Based Forest Management)* yenye jumla ya hekta 2,060,608 na vijiji 719 vinasimamia misitu kwa pamoja *(Joint Forest Management)* yenye jumla ya hekta 1,612,246.

Katika kuendeleza Kampeni ya Kupanda Miti Kitaifa, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na wadau wengine, ilihamasisha upandaji miti nchi nzima kwa kufuata majira ya mvua. Katika msimu wa mvua wa mwaka 2006/2007, wananchi walihamasishwa kupanda miti ambapo miche 135,098,575 ilipandwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara kwa kutumia vyombo vya habari, magazeti, vipeperushi, mabango na maonesho mbalimbali itaendelea kuhamasisha uanzishaji misitu ya vijiji na jamii kisheria na kuandaa mipango ya usimamizi. Vilevile, shughuli mbadala za kujiongezea kipato zitaainishwa na kuendelezwa ili kupunguza msukumo wa matumizi ya rasilimali za misitu na kuchangia katika kuondoa umaskini. Shughuli hizi ni pamoja na kuanzisha bustani za miti, ufugaji nyuki na matumizi ya majiko banifu. Aidha, Wizara itapanua wigo wa usimamizi shirikishi wa misitu kwenye wilaya nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendeleza elimu kwa umma kuhusu sera, sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya misitu na uendelezaji wa ufugaji nyuki, Wizara ilitayarisha na kutangaza vipindi 74 vya redio na vipindi 11 vya televisheni. Aidha, ilichapisha na kusambaza mabango 9,100, vipeperushi 10,000, kalenda 5,000, vitabu 11,000 na nakala 3,000 za Jarida la Misitu ni Mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara itaandaa na kutangaza vipindi vya redio na televisheni; kuchapisha na kusambaza kalenda za misitu, Jarida la Misitu ni Mali, mabango, vipeperushi na stika ili kuelimisha na kuhamasisha umma juu ya umuhimu wa rasilimali za misitu. Vilevile, Wizara itaendeleza kampeni za upandaji miti kitaifa na kuzuia uchomaji moto misitu ambao ni tatizo kubwa nchini. Aidha, vituo vya ugani vitaimarishwa ili kuhamasisha umma hasa wajasiriamali, juu ya matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na nyuki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maduhuli. Hadi kufikia Mei 2008, Wizara kupitia Sekta ndogo ya Misitu na Nyuki ilikusanya Shilingi 20,335,551,864 na kuvuka lengo la mwaka 2007/2008 la kukusanya Shilingi 15,601,745,000. Kati ya hizo Shilingi 20,331,640,464 zilitokana na mazao ya misitu. Makusanyo hayo yamevuka lengo kwa asilimia 30.34, kutokana na kuimarishwa kwa usimamizi wa biashara ya mazao ya misitu na uanzishaji wa vikosi vya doria katika kanda na juhudi mbalimbali za kuelimisha Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2008/2009, Wizara inatarajia kukusanya Shilingi 23,673,889,000 kutokana na sekta ndogo ya misitu na nyuki.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Utafiti wa Misitu. Taasisi inalo jukumu la kufanya tafiti zinazohusu uhifadhi wa ardhi, vyanzo vya maji, uhifadhi wa rasilimali za misitu na nyuki, kilimo mseto, hifadhi ya bioanuai, usimamizi wa misitu na ugunduzi wa teknolojia ya kupata mbegu bora za miti zinazokua haraka kulingana na maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi iliendelea na utafiti wa aina mbalimbali za mikaratusi inayofaa katika maeneo mbalimbali nchini. Mashamba 15 ya miti ya majaribio yaliendelea kutunzwa katika ukanda wa pwani, maeneo tambarare, maeneo ya miinuko, maeneo ya miombo, maeneo yenye ukame na kanda ya ziwa. Aidha, utafiti kuhusu matumizi ya maji kwa aina mbalimbali za miti uliendelea kwa kushirikiana na Kituo cha Kimataifa cha Kilimo Mseto. Katika utafiti huo, Taasisi ilikusanya takwimu za awali huko Kilolo Iringa na uchambuzi unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Utafiti wa Misitu, kwa kushirikiana na Taasisi za Utafiti za Finland na Norway iliendelea kufanya majaribio ya kukuza na kuhifadhi misitu ya miombo huko Kitulangalo, Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Utafiti wa Misitu iliendelea na mchakato wa ujenzi wa Makao Makuu ya Taasisi Kingolwira, Morogoro. Hadi sasa, Mtaalamu Mshauri amepatikana na awamu ya kwanza ya michoro imekamilika. Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Taasisi itaanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa Makao Makuu.

Aidha, Taasisi itaendelea kuandaa machapisho ya teknolojia zinazofaa katika kuendeleza matumizi bora ya misitu na kuzisambaza kwa wadau ili kuelimisha jamii. Miradi ya majaribio iliyoanzishwa sehemu mbalimbali nchini kwa mfano Lushoto, Korogwe (Mombo), Mwanga (Kifaru) itaendelea kutunzwa na miradi mipya itaanzishwa kulingana na mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Mbegu za Miti. Wakala inalo jukumu la kuzalisha, kuuza mbegu na miche, pamoja na kuhakiki, na kupima ubora wa mbegu kabla ya kuhifadhiwa au kuuzwa kwa wateja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwezesha upatikanaji endelevu wa mazao ya misitu na utunzaji wa mazingira, Wakala wa Mbegu za Miti ilizalisha na kuuza mbegu bora za miti pamoja na miche. Wakala ilikuwa na kilo 19,200 za mbegu za miti katika

maghala yake hadi Mei, 2008. Katika kipindi hicho, Wakala ilikusanya kilo 10,077 za mbegu za miti na kuuza kilo 8,739 na miche 45,779 sehemu mbalimbali nchini. Aidha, kilo 348 ziliuzwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ili kuhakikisha kuwa upatikanaji wa Mbegu bora unakuwa endelevu, Wakala ilianzisha vyanzo vitatu vya mbegu za miti ya Mikaratusi na Misindano. Vyanzo vinne vya miti ya kiasili ya Mkongo, Mninga, Mvule na Mkangazi vilitambuliwa na kuandikishwa katika sehemu mbalimbali hapa nchini. Wakala pia, iliendelea kutunza vyanzo 26 vya mbegu za miti vya aina mbalimbali.

Katika mwaka 2008/2009, Wakala itakusanya kilo 12,500 za mbegu bora za miti na itauza kilo 11,000 na miche ya miti 50,000 nchini, na kilo 1,000 za mbegu nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ndogo ya utalii. Wizara kupitia Sekta ndogo ya Utalii, ina jukumu la kusimamia uboreshaji huduma na uendelezaji utalii ili kuhakikisha kuwa mchango wa sekta katika pato la Taifa unaongezeka. Ukuaji huo unapaswa kuzingatia Sera ya Utalii ya mwaka 1999 inayosisitiza utalii endelevu unaokubalika kijamii, kiutamaduni, kiuchumi na unaohifadhi mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera na Sheria. Katika mwaka 2007/2008, Sekta ndogo ya Utalii iliendelea kutekeleza jukumu la kusimamia uendelezaji wa utalii nchini kupitia sera na sheria. Napenda kuliarifu Bunge lako kuwa kufuatia kupitishwa kwa Sheria ya Utalii ya mwaka 2008, Kanuni za kusimamia utekelezaji wake zitakamilika na kuanza kutumika katika mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Takwimu na Utafiti. Wizara kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali nchini, imeendelea kuunda mfumo wa ukusanyaji takwimu za sekta ya utalii. Mfumo huo ujulikanao kama *Tourism Satellite Account'* utatumika kupima ukuaji wa sekta na mchango wake katika pato la taifa. Katika hatua za uundaji wa mfumo huo, Wizara kwa kushirikiana na Benki Kuu, Idara ya Uhamiaji na Wakala wa Ukusanyaji Takwimu itaanza kukusanya takwimu za watalii wanaoingia nchini kwa njia ya elektroniki kupitia Vituo vya Viwanja vya Ndege vya Mwalimu J. K. Nyerere, Zanzibar na Kilimanjaro pamoja na Kituo cha Namanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Upangaji wa Hoteli katika Daraja. Wizara imechapisha nakala 1,000 za vijitabu vinavyoonyesha vigezo vya kuweka hoteli katika daraja mbalimbali. Vijitabu hivi vitasambazwa kwa wadau wote. Makundi ambayo yameandaliwa vijitabu ni yafuatayo: *Town Hotels, Lodges, Vocation Hotels*, *Restaurants, Motels na Tented Camps*. Kazi hii ni hatua ya awali ya utekelezaji wa zoezi la kupanga hoteli katika daraja. Upangaji wa hoteli katika daraja utasaidia kuboresha huduma zitolewazo, kuinua hadhi ya hoteli na kuridhisha wateja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara itakamilisha zoezi la kuweka Hoteli katika daraja kwenye Mikoa ya Arusha, Manyara, Dar es Salaam, Pwani, Tanga, na Kilimanjaro. Vilevile, hoteli katika Mikoa ya Morogoro, Iringa, Mbeya na Lindi zitahakikiwa ili kufahamu idadi na baadaye kuziweka katika daraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Mafunzo ya Utalii. Wizara inatekeleza Mradi wa Mafunzo unaogharimiwa na Jumuiya ya Nchi za Ulaya. Katika mwaka 2007/2008, mradi umekamilisha rasimu za viwango vya stadi za kazi katika maeneo ya huduma ya mapokezi, uandaaji wa vyakula na vinywaji, upishi na huduma za vyumba na uongozaji watalii. Vikundikazi vya wataalamu na wadau vimeundwa ili kupitia rasimu hizo kabla ya kufanyika warsha ya Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya mradi huo, rasimu ya mtaala wa mafunzo yanayohusu tasnia ya ukarimu inayokidhi mahitaji ya wadau imetayarishwa. Rasimu hiyo itaboreshwa zaidi baada ya kukamilika kwa viwango vya stadi za kazi na hatimaye kupitishwa kwa wataalamu na wadau husika. Tovuti ya Mradi (*www.ttptanzania.com*) imetayarishwa ambayo itatumika kutambulisha viwango vya stadi za kazi, mitaala na kutoa mafunzo kazini, hususan kwa wafanyakazi wa hoteli.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa mradi wa mafunzo wa Sekta ya Utalii, Wizara imetoa mafunzo kwa wafanyakazi 300 yaliyolenga katika utoaji wa huduma bora kwa wageni. Walioshiriki mafunzo hayo ni watumishi wanaotoa huduma za hoteli, wakala wa utalii na waongoza misafara ya watalii. Mafunzo hayo yalifanyika kuanzia Machi hadi Mei 2008 kwenye Tawi la Chuo cha Taifa cha Utalii, Arusha. Wizara itaendelea kufanya mafunzo hayo kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Mradi wa mafunzo unaoendelea chini ya ufadhili wa Jumuiya ya nchi za Ulaya, utatoa mafunzo ya ualimu kwa wakufunzi wa vyuo vilivyosajiliwa na *National Acredictation for Technical Education (NACTE)* na *Vocational Education Training Authority (VETA)*. Kwa kuanzia, vyuo vitakavyonufaika na mafunzo hayo ni Chuo cha Taifa cha Utalii (Dar es Salaam na Tawi la Arusha), Njuweni (Pwani), Masoka (Kilimanjaro), Chuo cha hoteli cha Zanzibar, na *VETA* tawi la Mikumi na Morogoro. Mpango wa mafunzo kazini utaanza kutekelezwa katika fani za malazi na chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Utalii. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara ililiarifu Bunge lako kwamba, Tanzania imepata heshima ya kujenga Chuo Kikuu cha Utalii kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Biashara cha Dunia *(World Trade University)*. Ninayo furaha kuliarifu Bunge lako kwamba eneo limekwisha patikana mkoani Pwani na mchakato wa ujenzi utaanza mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kuondoa Umasikini Kupitia Utalii. Katika mwaka 2007/2008, eneo la Pangani/Saadani lilipata kiasi cha Dola za Kimarekani 77,500 kutoka Shirika la Utalii Duniani *(United Nation World Tourism Organisation – UNWTO)* kupitia Mradi wa Kuondoa Umaskini kutokana na Utalii Endelevu *(Sustainable Tourism for Eradication of Poverty – STEP Initiative)*. Utekelezaji wa mradi huo ambao unasimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Pangani umeanza kwa kujenga Kituo cha Kutoa Taarifa kwa Watalii *(Tourist Information Centre)*. Vilevile, mafunzo yametolewa kwa watendaji wanne wa Kituo na ununuzi wa vitendea kazi umefanyika.

Katika mwaka 2008/2009, ujenzi wa jengo la kituo cha kutoa taarifa za Utalii cha Pangani utakamilika. Aidha, mafunzo yatatolewa kwa wananchi wanaozunguka eneo la mradi, ambao wanatoa huduma kwa watalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushirikishaji Jamii na Elimu kwa Umma. Katika kuhamasisha uhifadhi wa mazingira na kuinua kipato cha jamii zinazoishi katika maeneo ya pwani, Wizara kupitia Mradi wa Programu ya Maeneo ya Hifadhi za Bahari na Ukanda wa Pwani *(Marine and Coastal Environmental Management Programme (MACEMP)* imeainisha namna wadau wa utalii watakavyoweza kushirikishwa. Mradi huo unatekelezwa kwa kushirikiana na uongozi wa Wilaya za Kilwa na Mafia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi uliendesha warsha mbili za uhamasishaji kwa wananchi 170 kutoka Wilaya za Kilwa na Mafia. Aidha, mafunzo ya muda mfupi katika maeneo ya ujasiriamali, uongozaji watalii, usafi na uandaaji wa vyakula na utoaji huduma bora kwa wageni yalitolewa kwa vikundi vitatu kutoka wilaya ya Kilwa. Katika mwaka 2008/2009, Wizara kupitia Mradi wa *MACEMP* itatota mafunzo kwa vikundi vinne wilayani Mafia na kuendesha warsha za uhamasishaji katika Wilaya za Pangani na Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuendeleza Utalii wa Fukwe. Katika mwaka 2007/2008, Wizara ilishirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kubaini na kutathmini maeneo ya fukwe kwa ajili ya uwekezaji wa utalii. Zoezi hili lilifanyika Mkoani Tanga katika Wilaya za Muheza, Pangani, Mkinga na Tanga. Katika kipindi cha 2008/2009, Wizara itaendelea na zoezi la kubaini na kutambua maeneo ya kuendeleza utalii wa fukwe katika Mikoa ya Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maduhuli. Katika mwaka 2007/2008, Wizara ililenga kukusanya Shilingi 1,182,720,000 kutokana na leseni mbalimbali za wakala wa utalii nchini. Hadi kufikia mwezi Mei 2008, jumla ya fedha zilizokwisha kusanywa zilikuwa ni Shilingi 1,813,914,000 hivyo kuvuka lengo kwa asilimia 53. Hii inatokana na kuongezeka kwa idadi ya kampuni zinazoendesha biashara ya utalii kutoka 500 hadi 545 pamoja na hatua ya Wizara kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa leseni za Wakala wa Utalii ambapo baadhi ya kampuni zililazimika kulipia malimbikizo ya ada za leseni. Katika mwaka 2008/2009, Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi 1,731,118,000 kutokana na leseni mbalimbali za Wakala wa Utalii. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la asilimia 41.6 ya makadirio ya mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Utalii. Bodi inalo jukumu la kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje na nchi, kwa kushirikisha sekta binafsi na wadau mbalimbali ili kuharakisha ukuaji wa Sekta ya Utalii nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utangazaji wa Utalii. Rasilimali ya amani, umoja, mshikamano, demokrasia na ukarimu imeendelea kuwa chachu ya kutangaza na kuviuza vivutio vya utalii vya Tanzania ndani na nje ya nchi. Kwa mwaka 2007/2008, Mlima Kilimanjaro ulitangazwa kuwa miongoni mwa vivutio 52 vyenye mvuto zaidi duniani na

ambavyo watalii walishauriwa kuvitembelea. Aidha, mlima huu ulitangazwa nchini Marekani kama moja ya vivutio tano (5) muhimu kwa watalii kutembelea hapa nchini. Vivutio vingine vilivyotangazwa zaidi ni Hifadhi za Taifa za Gombe, Katavi, Mahale, Tarangire, Serengeti, Mkomazi pamoja na Kreta ya Ngorongoro na Pori la Akiba *Selous*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nchi za Marekani na Uingereza ni miongoni mwa masoko makuu yanayoipatia Tanzania watalii wengi zaidi. Ili kuendelea kupata watalii wengi kutoka nchi hizo, Bodi ilitoa matangazo kupitia Televisheni ya *CNN* - Amerika, *CNN Headline News*, tovuti ya *CNN* na kwenye viwanja 54 vya Ndege nchini Marekani kuanzia Oktoba, 2007 hadi Machi, 2008. Aidha, utangazaji kupitia *CNN – International* ulifanyika kuanzia Desemba, 2007 hadi Februari, 2008 ambapo watazamaji wapatao milioni 152 waliyaona matangazo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Bodi ilibandika mabango yenye picha za vivutio kwenye mabasi 124 yanayosafirisha abiria katika Jiji la London. Matangazo mengine yaliwekwa kwenye kiwanja cha ndege cha Heathrow, London. Matangazo hayo yalidumu kwa muda wa miezi mitatu kuanzia Desemba, 2007 hadi Februari, 2008. Inakadiriwa kuwa, watu milioni 10 waliyaona matangazo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo kwa wakala wa biashara ya utalii walioko Marekani na Canada yalifanyika kupitia mtandao na jarida la *USA Travel Agent*. Mafunzo hayo yaliyoanza Oktoba, 2007 tayari yamevutia wakala 37,000 na kati yao, 1,777 wamefuzu mitihani waliyopewa. Taratibu zinafanywa na Bodi kwa kushirikiana na wadau ili kuwaleta baadhi ya washindi wa mafunzo hayo kuona vivutio vya utalii nchini. Aidha, hapa nchini wakala wa biashara ya utalii wapatao 65 walishiriki kwenye semina sita zilizoandaliwa na Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Agosti mwaka 2007, Wizara ilishiriki tamasha la watengenezaji filamu linalojulikana kama *WildTalk Africa* huko Durban nchini Afrika Kusini. Kampuni za televisheni za *CNN, BBC, SuperSports* na *SABC* zilishiriki tamasha hilo na kurusha matangazo hayo moja kwa moja. Waandaji wa tamasha hilo walikadiria kuwa watazamaji zaidi ya milioni 100 duniani kote waliona matangazo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maonesho ya Kitaifa na Kimataifa. Katika kutangaza utalii, Bodi kwa kushirikiana na wadau ilishiriki maonesho ya utalii 22 nje ya nchi. Maonesho hayo yalifanyika katika nchi za Marekani, Canada, Uingereza, Uholanzi, Italia, Hispania, Ujerumani, Urusi, China, Japan, Ubeligiji, Afrika Kusini, Korea Kusini, Australia, na Nchi za Scandinavia na Falme za Kiarabu.

Aidha, mnamo mwezi Februari, 2008, Wizara iliongoza msafara maalum wa kutangaza vivutio vya utalii nchini Marekani kwenye miji ya New York, Phoenix, Los Angeles na Toronto, Canada. Msafara wa pili ulifanyika mwezi Aprili, 2008 kwenye miji ya Frankfurt, Berlin, Munich, Stuttgart, Vienna na Zurich.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza diplomasia ya kiuchumi kwa vitendo, Wizara ilitoa Dola za Kimarekani 450,000 kwa ajili ya kuziwezesha Balozi za Tanzania katika nchi 28 kununua nyenzo za kutangaza vivutio vya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** mwaka 2007/2008, Wizara iliarifu Bunge lako kuwa utangazaji utalii una gharama kubwa hivyo kuwashauri wadau kuchangia. Jumla ya Shilingi bilioni 2.94 zilichangwa na wadau ambao ni Shirika la Hifadhi za Taifa (Shilingi bilioni 1.5); Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (Shilingi milioni 500); Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori (Shilingi milioni 500); na Wadau Binafsi (Shilingi milioni 440). Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza wote waliotoa michango hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Wizara itaendeleza utaratibu huu wa kuchangia bajeti ya utangazaji kuwa wa kudumu kwa kushirikisha wadau wengi zaidi. Utaratibu huu ni miongoni mwa mapendekezo mapya yaliyomo kwenye Mkakati wa Kutangaza Utalii ambao unaandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Wizara imelenga kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea nchini kutoka 724,000 mwaka 2007 hadi milioni 1.2 ifikapo mwaka 2012. Ili kufikia lengo hilo, katika mwaka 2008/2009, Bodi ya Utalii itaendesha kampeni makini ya utangazaji ili kujikita ndani ya masoko makuu ya utalii na masoko mapya yanayoibukia. Masoko hayo ni China, India, Japan, Urusi, Mashariki ya Kati, Australia na Afrika Kusini. Vilevile, Bodi inakusudia kufikia makubaliano ya kutangaza vivutio vya utalii kupitia televisheni za Africa Channel ya California, *Skynews* ya Uingereza, *BBC World News*, *Euronews* na kuendelea kutumia tena *CNN* pale tutakapoona inafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Bodi ya Utalii itaendelea kutangaza utalii kupitia tovuti yake ambayo imeunganishwa na tovuti mbalimbali kwenye masoko makuu. Majarida mapya yenye kauli mbiu ya *"Tanzania The Land of Kilimanjaro, Zanzíbar and the Serengeti*" yatachapishwa sambamba na ramani za kitalii, na utayarishaji filamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Bodi ya Utalii inakusudia kuimarisha Balozi zetu zote na pia kuteua wakala wa utalii kwenye nchi za China na Ujerumani, pamoja na nchi za Scandinavia, Mashariki ya Kati na Mashariki ya Mbali. Lengo ni kuwezesha Bodi kutumia Balozi na wakala hao kuwafikia watalii walengwa na kuwapatia habari za utalii wa Tanzania. Inatarajiwa kuwa, jitihada hizi zitaiwezesha Serikali kuongeza mapato yatokanayo na utalii kutoka Dola za Kimarekani milioni 930 (2007) hadi bilioni 1.5 ifikapo mwaka 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utalii wa Utamaduni. Wizara itaendelea kutoa ushauri wa kuanzisha na kusimamia utalii wa kiutamaduni chini ya Programu ya Utalii wa Utamaduni (*Cultural Tourism Programme*). Hivi sasa kuna jumla ya vikundi 24 vilivyoko Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Pwani, Tanga, Morogoro na Mbeya. Katika mwaka 2008/2009, idadi ya vikundi inatarajiwa kuongezeka hadi kufikia 34 kutokana na kuanzisha vikundi vingine katika maeneo ya Ukanda wa Pwani na Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ndogo ya mambo ya kale. Katika mwaka 2007/2008, Wizara iliendelea kuhifadhi rasilimali za malikale kwa kushirikisha wadau mbalimbali na kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu uhifadhi wa maeneo hayo. Lengo la ushauri huo ni kuwaongezea wananchi uelewa wa kutunza na kunufaika na rasilimali hizo. Hatua hii inasaidia kukuza rasilimali za malikale kama vivutio vya utalii na kupunguza kasi ya uharibifu unaosababisha kupotea kwa rasilimali hizo hususan magofu na majengo ya kale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera na Sheria. Napenda kuliarifu Bunge lako kwamba, katika kuendeleza maeneo ya malikale na kuwezesha Sekta ndogo ya Mambo ya Kale kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi, Wizara ilikamilisha Sera ya Malikale ambayo ilipitishwa mwezi Mei 2008. Sera hiyo inatoa mwelekeo wa kushirikisha wadau katika kuhifadhi, kusimamia na kulinda malikale ikiwa ni pamoja na kuendeleza utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara itachapisha na kusambaza kwa wadau Sera ya Malikale na kuanza utekelezaji wa sera hiyo. Vilevile, itaendelea na mchakato wa kurekebisha Sheria ya Mambo ya Kale ya mwaka 1964 na marekebisho yaliyofanywa mwaka 1979 ili iendane na sera.

Mheshimiwa Naibu Spika, Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali Kale**.** Katika jitihada za kuendeleza na kuhifadhi rasilimali za malikale, mwaka 2007/2008, Wizara iliendelea na ujenzi wa kituo cha taarifa cha kumbukizi ya Dkt. Livingstone kilichopo Ujiji, Kigoma. Ujenzi wa kituo hicho upo katika hatua za mwisho. Kukamilika kwa ujenzi huo kutatoa fursa kwa wananchi wa Ujiji kushiriki, kutumia na kuendeleza urithi wa utamaduni ikiwa ni pamoja na kuibua miradi ya kuwaongezea kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika kuhifadhi rasilimali za urithi wa utamaduni, Wizara imekamilisha kuweka vioneshwa katika vituo vya Caravan Serai, Bagamoyo; Isimila, Iringa; na Kolo, Kondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kuhifadhi maeneo ya malikale na kuboresha huduma zinazotolewa kwa watalii, mwaka 2008/2009, Wizara itayatambua maeneo mapya ya malikale pamoja na kuboresha yaliyopo. Maeneo mapya ni pamoja na Njia ya Kati ya Biashara ya Utumwa na Vipusa, baadhi ya maeneo na kambi za wapigania uhuru na eneo la Ulyankulu, Urambo. Vituo vitakavyoboreshwa ni Eneo la Bonde la Oldupai, Kituo cha magofu ya Kunduchi na Kimondo cha Mbozi, Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2008/2009, Wizara itaendeleza juhudi za kuhifadhi na kuinua utalii wa malikale kwa kubuni na kuandaa michoro ya ujenzi wa vituo vya kumbukumbu na kuhabarisha *(Information Centre)* katika Bonde la Oldupai na Mapango ya Amboni. Vilevile, Wizara itaandaa mpango wa uhifadhi wa magofu ya Kaole yaliyoko Bagamoyo pamoja na kuanza kuutekeleza hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilwa Kisiwani na Songo Mnara ni eneo lililo kwenye Orodha ya Urithi wa Dunia ulio hatarini kutoweka. Ili kulinusuru eneo hilo, katika

kipindi cha 2007/2008, Wizara ilikarabati magofu ya Kasri ya Sultani na Msikiti wa Ijumaa yaliyoko Songo Mnara. Aidha, jumla ya wanakijiji 30 walipatiwa mafunzo ya uhifadhi ambapo watano walifundishwa kukata mawe, 23 ukarabati wa majengo ya kale na wawili kutengeneza na kuhifadhi chokaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2008/2009, Wizara itakarabati na kudhibiti mmomonyoko wa ardhi unaoendelea katika gofu la zamani la gereza lililopo eneo la Urithi wa Dunia Kilwa Kisiwani na Songo Mnara. Aidha, kupitia mradi wa utalii wa utamaduni utakaofadhiliwa na Shirika la *UNESCO* kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa, wananchi wa Kilwa na Songo Mnara watawezeshwa kujenga uwezo wa kuibua miradi ya kuwaongezea kipato pamoja na kuwezeshwa kushiriki katika kuhifadhi urithi wa malikale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tathmini ya Rasilimali. Katika mwaka 2007/2008, Wizara iliandaa mfumo utakaotumika kukusanya, kutunza na kusambaza kumbukumbu mbalimbali za maeneo yenye malikale hapa nchini. Mfumo huo umefanyiwa majaribio katika maeneo ya Kigoma, Rufiji, Mafia, Kilwa, Morogoro na Dodoma na imebainika kuwa unafaa katika ukusanyaji wa kumbukumbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2008/2009, Wizara itatumia mfumo huo kukusanya kumbukumbu za Kituo cha Tembe la Kwihara mkoani Tabora ili kupata taarifa na historia kamili ya tembe hilo kabla ya kulifanyia ukarabati. Aidha, Wizara itaanza mchakato wa awali wa majaribio ya kutunza na kusambaza kumbukumbu kwa kuandaa kanzidata za maeneo yenye urithi wa utamaduni nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** ili kutunza historia ya mchango wa nchi yetu katika ukombozi Kusini mwa Bara la Afrika, Wizara iliona umuhimu wa kuhifadhi kambi za wapigania uhuru. Katika mwaka 2007/2008, Wizara kwa kushirikisha wadau mbalimbali ilikusanya taarifa za maeneo na kambi zilizotumiwa na wapigania uhuru hao. Kazi hiyo ilifanyika katika kambi za Mazimbu na Dakawa mkoani Morogoro; na Kongwa mkoani Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Katika kutunza kumbukumbu za malikale, Wizara kupitia Programu ya Maeneo ya Hifadhi za Bahari na Ukanda wa Pwani (*Marine and Coastal Environment Management Programme – MACEMP*), imekusanya kumbukumbu za maeneo zaidi ya 34 yenye magofu ya kale katika Wilaya za Kilwa, Rufiji na Mafia.

Katika kipindi cha 2008/2009, Wizara itaendelea na zoezi la kukusanya kumbukumbu za maeneo ya urithi wa utamaduni katika Mikoa ya Pwani na Tanga, kwa nia ya kuyahifadhi na kuyaendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uendelezaji na Utangazaji wa vivutio vya Malikale. Wizara inaendelea na mchakato wa kukamilisha kabrasha, kwa ajili ya kuiwezesha Njia Kuu ya Kati ya Biashara ya Utumwa na Vipusa kuorodheshwa kwenye Orodha ya Urithi wa Dunia. Kwa mwaka 2007/2008, Wizara ilikamilisha kazi ya uchoraji wa ramani ya Njia hiyo na kuanza taratibu za kuandaa mipango ya uhifadhi na uendeshaji wa vituo

saba ambavyo ni Bagamoyo mkoani Pwani, Mamboya mkoani Morogoro; Mpwapwa mkoani Dodoma, Kilimatinde mkoani Singida; Kwihara na Ulyankulu mkoani Tabora, na Ujiji Mkoani Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** mwaka 2008/2009, Wizara itaendeleza mchakato wa kukamilisha na kuwasilisha UNESCO Kabrasha la Njia Kuu ya Kati ya Biashara ya Utumwa na Vipusa. Mchakato huu ni pamoja na kukamilisha mipango ya usimamizi wa vituo saba vilivyoainishwa katika mpango huo.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Tanzania imeteuliwa kuwa mwenyeji wa kongamano la Kimataifa la '*African Diaspora Heritage Trail Conference'* litakalofanyika mwezi Septemba, 2009. Maudhui ya Kongamano hilo ni kuhamasisha utalii wa kiutamaduni unao tokana historia ya masuala ya biashara ya biashara ya utumwa duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** aidha, maadhimisho ya kumbukumbu ya miaka 50 ya uvumbuzi wa Fuvu la Binadamu wa Kale (Zamadamu) "*Zinjanthropus boisei*" yatafanyika mwezi Julai, 2009 katika Bonde la Oldupai. Maadhimisho hayo yatashirikisha wadau kutoka ndani na nje ya nchi hivyo kuitangaza Tanzania katika utalii wa urithi wa utamaduni duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Ushirikishwaji Jamii na Elimu kwa Umma**.** Mwaka 2007/2008, Wizara iliendeleza jitihada za kuhakikisha kuwa jamii inapata elimu stahili juu ya historia na urithi wa utamaduni wetu. Wizara ilianzisha programu ya uhamasishaji jamii ambayo itatoa fursa kwa jamii kufahamu, kuendeleza na kutunza historia ya nchi yetu kwa lengo la kukuza utalii. Utekelezaji wake utaanzia Mikoa ya Pwani na Lindi hususan Wilaya za Rufiji, Mafia na Kilwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Utangazaji Tanzania (*TBC*) katika mwaka 2007/2008, iliendelea kurusha kipindi cha Zamadamu kinachohusu masuala mbalimbali ya malikale. Kipindi hicho hurushwa hewani kila Alhamisi saa 1.30 hadi 2.00 usiku na kurudiwa Jumapili saa 5.30 hadi 6.00 mchana. Kipindi hiki kimesaidia kuelimisha jamii juu ya umuhimu na changamoto za kuhifadhi na kuendeleza urithi wa malikale katika taifa letu.

Mwaka 2008/2009, Wizara itaendelea kushirikiana na Taasisi ya Utangazaji Tanzania (*TBC*), kuelimisha jamii kuhusu vivutio vya malikale, tafiti, uhifadhi na ushirikishwaji jamii katika kuhifadhi na kuendeleza urithi wa utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Utafiti wa Malikale. Wizara iliendelea kuratibu na kusimamia utafiti wa akiolojia unaofanywa na watafiti mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi kwa mujibu wa sheria. Katika kipindi cha 2007/2008, Wizara ilitoa jumla ya vibali 11 ambavyo vilihusu utafiti wa akiolojia, usafirishaji wa masalia ya malikale na ukarabati wa majengo ya kihistoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maduhuli**.** Mwaka 2007/2008, Wizara iliweka lengo la kukusanya jumla ya shilingi milioni 226.5 kutokana na ada za viingilio kwenye vituo vya Mambo ya Kale, vibali vya utafiti na mrahaba kutokana na rasilimali kale zilizoko nchini

Kenya. Hadi mwezi Mei 2008, jumla ya shilingi milioni 244.8 zilikusanywa ikiwa ni sawa na asilimia 8.1 zaidi ya lengo lililowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara inatarajia kukusanya Shilingi 263,801,000 kutokana na ada mbalimbali zinazokusanywa na Sekta Ndogo ya Mambo ya Kale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Makumbusho ya Taifa**.** Shirika la Makumbusho ya Taifa la Tanzania lina jukumu la kukusanya, kuhifadhi, kutafiti na kuelimisha jamii kwa njia ya maonesho yahusuyo urithi wa maliasili na utamaduni wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Usimamizi na Uendelezaji wa Makumbusho**.** Katika mwaka 2007/2008, Shirika liliendelea kutoa ushauri wa kitaalamu katika Wilaya za Singida, Morogoro Mjini, Maswa, Nyamagana, Mbulu na Njombe ili kuziwezesha kuanzisha au kuboresha makumbusho za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Shirika lilishauriana na Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu, kuhusu ujenzi wa Makumbusho ya kisasa mkoani Dodoma. Eneo linalofaa kwa ajili ya ujenzi wa makumbusho hayo linatafutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** kama nilivyoahidi katika Bunge lako mwaka jana, ujenzi wa jengo la Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni ulianza mwezi Agosti, 2007 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2009. Kukamilika kwa ujenzi wa Nyumba hiyo kutatoa nafasi ya kurejesha na kuhifadhi rasilimali kale za Tanzania ambazo hivi sasa zinahifadhiwa katika Makumbusho ya Taifa la Kenya, Nairobi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka 2008/2009, Shirika litakamilisha taratibu za kupokea na kuhifadhi rasilimali kale zilizovumbuliwa nchini na kuhifadhiwa katika Makumbusho ya Taifa la Kenya, Nairobi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, uboreshaji wa mandhari ya Kijiji cha Makumbusho ulifanyika kwa kukarabati nyumba za Wafipa, Wahaya, Wachaga na Wanyakyusa. Vilevile, matamasha ya “Watoto wenye Mahitaji Maalum” na “Ya Kale Yanapokutana na ya Sasa” yaliandaliwa. Wizara imebaini kuwa, dhana ya kuzishirikisha jamii mojamoja ina hamasa zaidi kuliko ile ya kimkoa. Kwa ajili hiyo, mwaka 2008/2009 jamii ya Wahangaza na Washubi kutoka Ngara watafanya tamasha la Utamaduni wa Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika lilitoa machapisho mawili yanayohusu miaka 100 ya vita vya Maji Maji na Biashara ya Utumwa. Kila chapisho lilitolewa nakala 1,500 ambazo zinauzwa kwa wadau. Aidha, maonesho kuhusu chimbuko la mwanadamu yaliandaliwa na kutembezwa *(mobile exhibition)* katika maeneo ya Wilaya ya Temeke, Ilala na Kinondoni mkoani Dar es Salaam, mwezi Desemba, 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushirikishaji jamii na elimu kwa Umma**.** Katika mwaka 2008/2009, Shirika litaendelea kuhamasisha jamii na baadhi ya halmashauri za wilaya kuhusu uhifadhi na uendelezaji wa makumbusho nchini. Vilevile, litaendelea kutoa ushauri wa kitaalamu juu ya kukusanya vifaa vya kimila, kuhifadhi vifaa hivyo na kuenzi utamaduni wa jamii zilizo katika wilaya hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utawala na Rasilimali Watu. Katika maendeleo ya watumishi na mafunzoMwaka 2007/2008, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma iliajiri jumla ya watumishi 128, ambapo ajira mpya ni 109 na mbadala 19. Ingawa kibali kilichotolewa ni cha ajira ya watumishi 349, nafasi 129 hazikujazwa kwa sababu ya kukosekana waombaji wenye sifa na taaluma stahili katika kada za wahifadhi wanyamapori, wasaidizi misitu na wasaidizi ufugaji nyuki kwenye soko la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara inalenga kuziba nafasi za ajira zilizobaki wazi katika mwaka wa fedha 2007/2008 na kuajiri watumishi wengine 246.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** watumishi 564 wa kada mbalimbali walipandishwa cheo kwa kuzingatia miundo ya Utumishi wa Umma na watumishi 427 walithibitishwa kazini. Mwaka 2008/2009, Wizara inategemea kupandisha cheo watumishi 494.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa kuwaongezea watumishi uwezo wa kielimu na kuboresha utendaji kazi, Wizara kwa mwaka 2007/2008, iligharimia mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi 650. Kati ya hao, watumishi 590 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi na 60 mafunzo ya muda mrefu. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo elekezi kuhusu Utumishi wa Umma kwa waajiriwa wapya 220.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ustawi wa Watumishi**.** Katika kuboresha ustawi wa watumishi, Wizara imeingia mkataba na taasisi nne za fedha na inaendelea kuwahamasisha watumishi kuchukua mikopo katika taasisi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa watumishi wa Wizara wanakuwa na ushirikiano mzuri na watumishi wengine wa serikali, mwaka 2007/2008 watumishi 54 walishiriki mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara (SHIMIWI) yaliyofanyika mkoani Tanga. Katika mwaka 2008/2009, Wizara itawakilishwa na watumishi 60 katika mashindano hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utawala Bora**.** Kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora, mwaka 2007/2008, Wizara iliandaa mafunzo ya utawala bora kwa wakuu wa idara na maafisa waandamizi. Vilevile, mafunzo hayo yalitolewa kwa watendaji wakuu wa mashirika na taasisi zilizo chini ya Wizara. Aidha, Wizara kupitia Mkataba wa Huduma kwa Mteja inahakikisha kuwa wadau wanapewa huduma bora, wanaelezwa huduma zinazotolewa, namna ya kuzipata, ikiwa ni pamoja na jinsi ya kuwasiliana na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya Wizara. Mwaka 2007/2008, Wizara iliendelea kusimamia na kuboresha vyuo vya mafunzo vilivyo chini yake kwa lengo la kuimarisha taaluma za wanyamapori, misitu, ufugaji nyuki na utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Wanyamapori Mweka**.** Katika mwaka 2007/2008, Chuo cha Wanyamapori Mweka kilidahili jumla ya wanafunzi 341 na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wanafunzi 100 katika fani ya usimamizi wa wanyamapori. Katika kuendeleza taaluma ya wakufunzi na watumishi wa Chuo, jumla ya watumishi saba walipatiwa mafunzo ya Stashahada, Shahada ya Uzamili na Uzamifu *(PhD).*

Mheshimiwa Naibu Spika**,** katika kipindi cha 2007/2008, Chuo, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, kilifanya utafiti katika maeneo ya mgawanyo wa gharama na faida zitokanazo na uhifadhi wa wanyamapori, tathmini ya upunguzaji wa mifugo katika maeneo yanayozunguka Hifadhi ya Ngorongoro na athari zinazosababishwa na kufungwa kwa biashara ya Kobe aina ya "*Pancake*" duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** katika mwaka 2008/2009, Chuo kitaanzisha kozi ya Astashahada ya Utalii wa Wanyamapori (*Wildlife Tourism*), ili kuboresha huduma kwa watalii. Vilevile, kitaandaa mtaala wa Stashahada ya Utalii wa Wanyamapori kuwezesha wanafunzi wanaomaliza mafunzo ya Astashahada waweze kujiendeleza. Kutokana na kasi ya ukuaji na kushamiri kwa biashara ya utalii unaojikita katika vivutio vya wanyamapori nchini, Chuo kinatarajia kutoa elimu ya Shahada ya Utalii wa Wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya Taaluma ya Misitu**.** Wizara inasimamia vyuo viwili vya taaluma ya misitu ambavyo ni Chuo cha Misitu Olmotonyi, Arusha na Chuo cha Viwanda vya Misitu, Moshi. Mitaala ya Astashahada na Stashahada ya Misitu katika Chuo Cha Misitu Olmotonyi imefanyiwa mapitio na itaanza kutumika katika mwaka wa masomo wa 2008/2009. Katika kukabiliana na upungufu wa wataalam kada ya wasaidizi wa misitu katika soko la ajira, Wizara inagharimia wanafunzi watarajali kutokana na sekta binafsi kutovutiwa kuwekeza katika nyanja hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa mwaka 2008/2009, Wizara itaendelea kujenga uwezo wa vyuo vyake kwa kuongeza idadi ya madarasa, nyenzo za mafunzo na kuimarisha miundombinu ili kupokea wanafunzi wengi zaidi, hususan watarajali. Wanafunzi 90 wanaogharimiwa na serikali, watadahiliwa katika Chuo cha Misitu Olmotonyi ambapo 18 watatoka kazini na 72 watakuwa watarajali. Vilevile, vyuo vitaendeleza urafiki baina yake na vyuo vya taaluma ya misitu vya Finland kwa lengo la kukuza mitaala, utafiti na stadi za kufundishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Cha Ufugaji Nyuki Tabora. Kwa kutambua umuhimu wa ufugaji nyuki katika kuchangia juhudi za kuondoa umaskini na kukuza uchumi, Wizara imeelekeza nguvu zake katika kuimarisha ufugaji nyuki. Hatua zilizochukuliwa ni kuanza kutumia tena Chuo cha Ufugaji Nyuki kilichoko mkoani Tabora, kuandaa mitaala ya Astashahada na Stashahada za ufugaji nyuki, kumteua Mkuu wa Chuo na kufanya tathmini ya miundombinu. Wanafunzi wa Astashahada na

Stashahada za ufugaji nyuki watadahiliwa na kuanza masomo katika Chuo cha Misitu Olmotonyi kwa mwaka 2008/2009 na baadaye watahamishiwa Tabora baada ya ukarabati kukamilika. Chuo kitaanza kwa kudahili wanafunzi 30. Kati ya hao, 15 watakuwa wa mafunzo ya Astashahada na 15 wa Stashahada. Miongoni mwao, wanafunzi watarajali ni 20 na wanaotoka kazini ni 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Taifa cha Utalii**.** Biashara ya utalii ni ya ushindani, hivyo mafunzo yanayotolewa katika fani hiyo yanatakiwa kwenda na wakati na kukidhi mahitaji ya wadau. Kwa kuzingatia hayo, Chuo kimeboresha mitaala na kuongeza nyanja za mafunzo kwa kuanzisha Stashahada katika fani ya Usafiri na Utalii *(Travel and Tourism).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Chuo kiliendelea kutoa mafunzo ya Astashahada katika fani za Upishi, Mapokezi, Huduma ya Chakula na Vinywaji, Utunzaji vyumba pamoja na Uongozaji Watalii. Aidha, Chuo kimepata ithibati (*full accreditation*) ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (*NACTE*), hivyo kufanya kozi zinazotolewa kutambulika kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** napenda kulifahamisha Bunge lako kuwa, ujenzi wa jengo jipya la chuo cha utalii umeanza kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa. Inatarajiwa kuwa ujenzi huo utakamilika katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha 2008/2009, Chuo kitapata wataalamu wanne kutoka nje ya nchi ili kusaidiana na wataalamu waliopo kutoa ushauri na kujenga uwezo wa ndani wa wafanyakazi, chini ya makubaliano ya msaada kati ya Serikali yetu na Serikali ya Ufaransa.

Mheshimiwa Naibu Spika, UKIMWI**.** Mwaka 2007/2008, Wizara iliendelea kutoa elimu juu ya janga la Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI), kwa kuendesha semina na kuhamasisha watumishi kupima ili kujua afya zao. Aidha, Wizara imeendelea kuwahudumia watumishi waliopima na kugundulika kuwa wameathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** majumuisho**.** Napenda kwa namna ya pekee, kuwashukuru wadau wote wa Sekta ya Maliasili na Utalii kwa ushirikiano walioonyesha katika utekelezaji wa malengo ya Wizara kwa mwaka 2007/2008. Vilevile, natoa shukrani kwa washirika wa maendeleo ambao ni Denmark, Finland, Norway, Marekani, Ubelgiji, Sweden, Ufaransa, Jumuiya ya nchi za Ulaya, Japan, Uingereza, Ujerumani, Uholanzi, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Ujerumani (KfW), United Nations Development Programme (*UNDP*), *United Nations for Education, Science and Culture Organisation (UNESCO), Food and Agriculture Organisation (FAO), International Union for Conservation of Nature (IUCN), International Centre for the Study of the Preservation of Cultural Property (ICCROM)*, asasi zisizokuwa za kiserikali na sekta binafsi kwa michango yao.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** naomba nikamilishe hotuba yangu kwa kumshukuru Waziri aliyenitangulia, Mheshimiwa Profesa Jumanne Abdallah Maghembe Mbunge na

Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita Mbunge aliyekuwa Naibu Waziri wake, kwa kuweka misingi mizuri ya utendaji katika Wizara. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Ezekiel Maige, Naibu Waziri na Mbunge wa Jimbo la Msalala; Bibi Blandina S.J. Nyoni, Katibu Mkuu; Wakuu wa Idara pamoja na watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa kunipa ushirikiano mzuri katika kutimiza majukumu niliyopewa. Kwa pamoja wamewezesha Wizara kukamilisha majukumu yake ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** baada ya maelezo haya, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii ya jumla ya Shilingi 71,975,518,000 kwa ajili ya matumizi yake**.** Kati ya fedha hizo, Shilingi 10,340,443,800 ni kwa ajili ya mishahara (*PE*); Shilingi 27,835,223,200 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (*OC*); na Shilingi 33,799,851,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Wizara hii.

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika**,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kuniruhusu kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** kwa niaba ya wajumbe wenzangu wa Kamati, naomba kuwasilisha salamu za rambirambi kwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori, Watumishi wa Idara ya Wanyamapori, ndugu jamaa na marafiki wa familia za marehemu Miriam Onesmo Zacharia, Stephen Godfrey Mahinya na Rubani Pius Elisha Ng'walali, ambao walikuwa watumishi wa Idara ya Wanyamapori waliofariki kwenye ajali ya ndege ndogo iliyogonga mlima huko Monduli wiki iliyopita. Mungu azilaze roho za marehemu mahala pema peponi, amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wanakamati wenzangu, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Shamsa Mwangunga (Mb.), kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, pamoja na Mheshimiwa Ezekiel Maige, kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii. Mwenyezi Mungu awatangulie na kuwalinda katika utekelezaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya maliasili na utalii inajumuisha Idara za Wanyamapori, Misitu na Nyuki, Utalii na Mambo ya kale. Kamati ilikutana na watendaji wakuu wote wa Wizara hii wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri huko Dar es Salaam na

kupitia utekelezaji wa majukumu ya wizara na pia kupitia makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2008/09. Aidha, katika majadiliano Kamati ilifahamishwa mambo makuu yafuatayo:-

(i) Dira ya Wizara;

(ii) Uongozi na Muundo wa Wizara;

(iii) Majukumu ya Idara na Vitengo mbalimbali Wizarani;

(iv) Maelezo ya taasisi zilizo chini ya Wizara;

(v) Kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka 2008/09; na

(vi) Utekelezaji wa maagizo mbalimbali ya Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujadili bajeti ya Wizara hii, Kamati ilipata maelezo ya kina toka kwa Mheshimiwa Waziri, alieleza kwamba maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2008/2009, chini ya Mpango wa Muda wa Kati wa Bajeti (*MTEF*), yamezingatia maelekezo mbalimbali ya Serikali yanayolenga katika kutekeleza Sera na Mikakati ya utekelezaji wa MKUKUTA. Aidha miongozo ifuatayo pia ilizingatiwa:-

(i) Ilani ya uchaguzi ya 2005 – 2010 ya Chama Cha Mapinduzi;

(ii) Maagizo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais alipohutubia Bunge la Jamhuri mwezi Desemba 2005 na alipotembelea Wizara;

(iii) Maoni na Mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge waliojadili Mpango na Bajeti ya mwaka 2007/2008;

(iv) Mwongozo wa Wizara ya Fedha na Uchumi wa mwaka 2008/09-2009/2010;

(v) Mpango Mkakati wa Wizara (Julai 2007- Juni 2010); na

(vi) Mabadiliko na maboresho ya Mifumo ya Utendaji Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2007/2008**.** Katika Mwaka wa fedha uliopita, Kamati yangu ilitoa maoni, ushauri na maagizo katika maeneo mbalimbali hasa yanayohusu Wanyamapori, Misitu na Nyuki, Malikale, Utalii na Utafiti katika sekta ya Maliasili na utalii. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara kwa kiasi kikubwa imefanyia kazi maeneo husika na hatua za utekelezaji zimeonekana. Hata hivyo, katika maeneo ambayo Kamati imeona juhudi zaidi zinahitajika, imeshauri na kutoa ushauri ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** katika mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara pamoja na Asasi zake, iliidhinishiwa na Bunge, Bajeti ya shilingi 55,493,624,000, kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Hadi mwezi Machi 2008, jumla ya shilingi 38,691,234,025 zilikuwa zimetumika kwa ajili ya mishahara, matumizi mengineyo na kutekeleza miradi ya maendeleo. Kiasi cha shilingi kilichobaki kilitarajiwa kuwa kimetumika hadi mwishoni mwa mwezi Juni, 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara ilikadiria kukusanya shilingi 74,757,259,000. Kufuatia Idara ya Uvuvi kuhamishiwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, makadirio ya makusanyo ya mwaka yameshuka hadi shilingi 66,701,838,000. Inakadiriwa kuwa hadi mwezi Juni 2008 kiasi cha shilingi 41,533,139,364 kilikusanywa ikiwa ni asilimia 62.3 ya makadirio, pungufu ya asilimia 37.7.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** hivyo basi, mwelekeo wa makusanyo katika Wizara unaonyesha kuwa lengo lililowekwa la shilingi 74,757,259,000 halikufikiwa hadi mwezi Juni 2008 kwa sababu ya kutotumika kwa tozo za awali za uwindaji wa kitalii na baadhi ya makampuni hasa ya kizalendo kushindwa kulipa kwa wakati hata tozo zilizopunguzwa na Serikali. Pia ushuru kwenye mazao ya misitu haukufikia malengo na kuhamishwa kwa Idara ya Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** mafanikio na matatizo katika utekelezaji wa bajeti 2007/2008**,** baadhi ya mafaniko hayo ni pamoja nayafuatayo:-

(i) Wizara iliendelea kuandaa, kusimamia na kutekeleza Sera zake ikiwa ni pamoja na mapitio ya Sera ya Wanyamapori imefanyiwa mapitio;

(ii) Sheria mpya ya Utalii ilipitishwa na Bunge na ipo tayari kutumika;

(iii) Elimu ya uhifadhi iliendelea kutolewa kwa kutumia njia au mbinu mbalimbali vikiwemo redio, luninga, warsha, mikutano na semina;

(iv) Kiasi cha shilingi 36,751,392,939 kilikusanywa ikiwa ni maduhuli;

(v) Asilimia 25 ya fedha zitokanazo na Uwindaji wa Kitalii, ziligawiwa kwa Halmashauri za Wilaya 29 kati ya 44 zenye maeneo ya uwindaji. Fedha hizo zilitumika katika kuhamasisha jamii kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo;

(vi) Wizara ilitangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi, Wizara ilishiriki katika jumla ya maonesho 18 katika nchi za Uingereza, Marekani, Ujerumani, Canada, China na Australia na kadhalika;

(vii) Katika kulinda rasilimali za maliasili na matumizi endelevu, doria za siku 21,478 na doria shirikishi 252 zilifanyika ndani na nje ya mapori ya akiba;

(viii) Mipaka ya misitu ya lindimaji ‘’*catchment forest*” ilisafishwa katika Mikoa sita;

(ix) Kaguzi za hoteli na wakala wanaoendesha biashara ya utalii na hoteli zilifanyika katika Mkoa wa Arusha;

(x) Jumla ya kilomita 252 za barabara, madaraja 7 na nyumba 27 za watumishi ndani ya mapori ya akiba zilikarabatiwa; na

(xi) Zoezi la ukaguzi lilifanyika katika vituo vikuu vinne vya kutokea na kuingilia watalii nchini. Vituo hivyo ni Uwanja wa Ndege wa J.K. Nyerere, *KIA*, Zanzibar na Namanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Bajeti ya 2007/08, pamoja na mafaniko yaliyopatikana, Wizara iliendelea kukabiliwa na changamoto zifuatazo:-

1. Upungufu wa watumishi wa kutekeleza majukumu na program za Wizara ni mkubwa;

2. Kuendelea kuwa na uvunaji haramu na matumizi yasiyokuwa endelevu ya rasilimali;

3. Ufinyu wa bajeti zinazotengwa na Serikali, hivyo kutokidhi utekelezaji wa malengo yalikusudiwa na dharura za uhifadhi;

4. Fedha za Wahisani (*counterpart funds*) kwa ajili ya miradi kutotolewa kwa wakati;

5. Ushiriki usioridhisha wa baadhi ya wadau katika matumizi na kuhifadhi maliasili na malikale; na

6. Fedha zilizoahidiwa na Serikali kwa miradi inayofadhiliwa kwa sehemu kubwa na wahisani kutopatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati**,** Sekta ya Maliasili na Utalii, inajumuisha sekta ndogo za Wanyamapori, Misitu na Nyuki, Utalii na Mambo Kale. Takwimu zinaonyesha kuwa mchango wa sekta hii kwenye pato la Taifa ni takribani asilimia 17.2 na takribani asilimia 25 ya fedha za kigeni hutokana na utalii. Hata hivyo, takwimu hizi hazionyeshi mchango halisi wa sekta hii kutokana na ukweli kwamba baadhi ya shughuli zinazofanywa kwenye sekta hii hazifuati sheria kikamilifu,

nyingine hazipimiki na nyingine mchango wake unajitokeza katika sekta nyingine. Kwa kuzingatia hayo, Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Utalii. Utalii ni sekta inayokua kwa kasi kubwa duniani na tafiti zinaonyesha itaendelea kukua kama sekta kubwa ya kibiashara katika uchumi wa Dunia. Tanzania ina vivutio vingi vya utalii vilivyoenea nchi nzima, lakini bado imeendelea kuwa nyuma katika kanda ya Afrika Mashariki kwa idadi ya watalii na mapato yatokanayo na tasnia hii. Hii imetokana kwa kiasi kikubwa kutegemea utalii wa mbuga za wanyama katika baadhi ya sehemu tu. Kamati inaishauri Wizara, ili kuongeza pato litokanalo na utalii ni muhimu kuendeleza maeneo mengine ya nchi sambamba na kuendeleza na kutangaza aina nyingine za utalii kama utalii wa utamaduni, malikale, ikolojia na utalii wa fukwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria mpya ya Utalii imeainisha vema masuala ya makosa na adhabu mbalimbali ambazo zinaweza kutolewa chini ya Sheria hii, Kamati inasisitiza kuwa hatua kali zichukuliwe kwa wale ambao watakiuka sheria na taratibu zilizopo. Kamati inatoa wito kwa vyombo husika wasimamie sheria ipasavyo na kuwachukulia hatua kali wanaohusika kukiuka sheria na taratibu zinazohusiana na Sheria hii mpya ya Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipata fursa ya kutembelea Chuo kipya cha Taifa cha Utalii ambacho kinaendelea kujengwa na ambacho kitakuwa kinatoa mafunzo ya utalii na huduma za hoteli. Kamati inashauri Wizara kuanza mara moja kutafuta wataalam wenye viwango ambao watakidhi utoaji wa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa karibuni pamekuwepo na malalamiko mengi toka kwa Wabunge na wananchi juu ya unyanyasaji na utendaji usioridhisha wa baadhi ya hoteli za kitalii zilizopo Kaskazini mwa Tanzania. Kamati imepanga kufanya ziara kabla ya mkutano wa Bunge wa 13 wa Oktoba 2008, katika hoteli za Hifadhi ya Ziwa Manyara, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Hifadhi ya Serengeti na Mapori ya Akiba ya Ikorongo na Grumeti. Kamati itazingatia na kupitia kwa makini kuona huduma zitolewazo na hoteli hizo pia Kamati itaangalia ubora wa majengo na mikakati ya ukarabati unaoendelea katika hoteli za zamani. Katika ziara hiyo, Kamati pia itapitia na kujionea eneo ambalo linapendekezwa na Wizara kwa ajili ya kupanua eneo la Hifadhi ya Ziwa Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Wanyamapori. Kamati ilikutana katika kikao na wanachama wa *TCT* (*Tourism Confederation of Tanzania*) Mjini Dar es salaam. Mazungumzo yalijikita katika namna bora ya kuboresha uwindaji wa kitalii ambapo Kamati ilihakikishiwa na wadau hao kuwa wako tayari kutoa ushirikiano kwa Serikali kuhusiana na suala zima la kukuza utalii na kuboresha mapato ya Serikali yatokanayo na uwindaji wa kitalii. Kamati inaishauri Wizara ikae pamoja na wadau hawa na kuzingatia maoni ya wadau pamoja na maoni ya Kamati ili kuboresha biashara ya uwindaji wa kitalii. Pia Wizara ishauriane na Kamati na *TCT* kuhusiana na taratibu bora zitakazotumika katika maamuzi muhimu kuelekea mwaka 2009 ambapo ni ukomo wa umiliki wa sasa wa vitalu vya uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali iunde shirika moja jipya litakalounganisha Mapori yote ya Akiba. Shirika hilo litasimamia shughuli mbalimbali kama uwindaji na utalii wa picha, ambazo zitakuwa zinafanyika katika mapori hayo. Shirika hilo *Tanzania Game Reserves* au Tanzania *Wildlife Reserve* au jina jingine lolote litakalotatuliwa na Serikali, litatatua matatizo mengi sana yanayokabili Mapori ya Akiba yaliyotapakaa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati, inalipongeza Bunge lako Tukufu kwa kuridhia Azimio la Kupandisha hadhi Pori la Akiba la Mkomazi kuwa hifadhi mpya ya Taifa ya Mkomazi. Hatua hii ni muhimu katika kulinda, kuhifadhi na kuboresha mapori ya Mkomazi na Umba ili kulinda bioanuwai za pekee za eneo hili pamoja na spishi za wanyamapori zilizoadimu au zilizo katika hatari ya kutoweka na kukuza rasilimali za wanyamapori kwa ajili ya utalii na vyanzo vya maji. Kamati inaiagiza Idara ya Wanyamapori ikabidhi haraka Hifadhi ya Mkomazi kwa Shirika la Hifadhi za Taifa (*TANAPA*).

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2001, eneo la Ziwa Natron lilitengwa chini ya Mkataba wa Kimataifa wa kuhifadhi Ardhiouevu. Eneo hili linakadiriwa kuwa na *Heroe* wadogo wapatao 2.5 milioni, kiasi cha asilimia 70 ya ndege hawa Duniani huzalia katika eneo hili. Kamati inaishauri Wizara kulihifadhi kwa uangalifu mkubwa eneo hili pia kulitangaza eneo hili kama mojawapo ya kivutio cha utalii. Kamati inashauri eneo la Ziwa Natron na Mlima Oldonyo Lengai yawe chini ya Ngorongoro *Conservation Area Authority* au Mamlaka nyingine yenye kuhakikisha ulinzi wa maliasili zilizopo au Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, itangaze eneo hili kuwa ni *Special Protection Area Authority* au mamlaka nyingine yenye kuhakikisha ulinzi wa maliasili zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi cha fedha kinachotengwa kwa Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI), katika bajeti ya mwaka huu, bado ni kidogo ukilinganisha na kazi zinazotakiwa kufanywa na Taasisi hiyo. Kamati inaishauri Wizara kutenga kiasi cha fedha za kutosha katika bajeti zijazo kwa ajili ya Taasisi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Wizara ipange madaraja ya vitalu vilivyopo katika makundi mawili au matatu ambapo bei za vitalu hivyo itapangwa kwa kuzingatia ubora wa kitalu kwa mahala kilipo, wanyama waliopo kwa aina zake, wingi wa wanyamapori na upatikanaji wa *The Big Five.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Wizara kutopokea ushauri wa kuwabagua wawekezaji wa kigeni katika zoezi la 2009 la kugawa vitalu vya uwindaji wa kitalii lakini pia Kamati inashauri kuwaangalia kipekee Watanzania wenye nia ya kweli ya kuwekeza katika biashara hiyo ama wao peke yao, ama kwa ushirika na Watanzania wenzao na pia Watanzania ambao wana ubia na wawekezaji wa kigeni wapewe fursa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado Kamati inasisitiza Wizara kuwasilisha Bungeni Sheria mpya ya Wanyamapori itakayochukua nafasi ya Sheria iliyopo, *The Wildlife Act*

*No. 12* ya 1974. Aidha, Sheria hiyo inatarajiwa kuja katika sura ya wakati wa sasa na ni matarajio ya Kamati kuwa suala la kuundwa kwa *Agency* mpya ya Mapori ya Akiba, litakuwa limezingatiwa katika mabadiliko yajayo ndani ya Sheria mpya. Kamati inasisitiza Serikali kujenga miundombinu mipya katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ambayo ndiyo hifadhi kubwa kuliko zote Barani Afrika. Hii itasaidia kufungua milango ya utalii kwa Mikoa ya Kusini. Kamati bado inasisitiza kwamba, vikosi vya doria viimarishwe ili kupambana na ujangili ambao sasa umeonyesha kuanza upya na kuongezeka kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Mambo ya kale. Kamati imeridhishwa na ujenzi unaoendelea sasa wa Nyumba ya Makumbusho ya Taifa. Nyumba hii itasaidia katika kuhifadhi utamaduni wetu na historia ya nchi yetu.

Pia Kamati inaishauri Wizara ikamilishe Sera ya Mambo ya kale, pia ile mikataba ambayo Wizara inaona itakuwa na faida kwa nchi yetu, iwasilishwe Bungeni ili iridhiwe vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Misitu na Nyuki. Bado kuna upungufu wa upatikanaji wa Mbegu za Mazao ya Miti na Matunda kwa wananchi. Kamati inasisitiza Wizara itafutie ufumbuzi suala hili.

Pia kwa kipindi kijacho cha fedha, Wizara itenge fedha za kutosha kwa Taasisi za Mbegu zilizo chini yake. Serikali ilishatoa tamko la kupinga usafirishaji wa magogo, Kamati inasisitiza kwamba migogoro yoyote iliyopo kuhusiana na masuala ya magogo, imalizwe na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaridhishwa na maendeleo yaliyopo ya kukarabati na kukirudisha Chuo cha Ufugaji wa Nyuki, Tabora. Ni mategemeo ya Kamati kwamba elimu itakayotolewa na utafiti utakaofanyika katika chuo hiki utahamasisha watu wengi wapende kufuga nyuki na hivyo kuinua mchango wa ufugaji wa nyuki. Aidha Kamati inaishauri Wizara kukitangaza chuo hiki ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2008/2009. Makadirio ya Mwaka wa fedha 2008/2009, ya Wizara ya Maliasili na utalii, yameandaliwa kwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele yanayolenga katika kutekeleza sera na mikakati ya utekelezaji wa MKUKUTA. Baada ya uchambuzi wa kina, Kamati inakubaliana na Makadirio ya Bajeti ya Wizara, Fungu 69, jumla ya shilingi 71,975,518,000 kati ya hizo, shilingi 33,799,851,000 ni kwa ajili ya maendeleo na shilingi 27,835,223,200 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 10,340,443,800 ni kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha fedha zinazoombwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuwatambua wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na utalii ambao ndio waliochambua bajeti hii nao ni;-

Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mwenyekiti, Mheshimiwa Hassan R. Khatib, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa James Daudi

Lembeli, Mheshimiwa William V. Lukuvi, Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mheshimiwa Dkt. Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mheshimiwa Dkt. Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Aziza S.Ally, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati yangu ina wajumbe 25 ni moja ya kamati kubwa kabisa humu Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, kwa niaba ya Wanakamati wenzangu, napenda kumshukuru Mheshimiwa Shamsa Mwangunga (Mb), Waziri wa Maliasili na Utalii, Naibu wake Mheshimiwa Ezekiel Maige (Mb), Katibu Mkuu wake Ndugu Blandina Nyoni, Wakurugenzi wa Idara na Watumishi wote wa Wizara hii na Taasisi ama Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati katika kipindi chote ambacho tumefanya nao kazi. Kamati inawashukuru sana na kuwatakia mafanikio makubwa zaidi katika kazi za Ujenzi wa Nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** napenda pia kuwashukuru Wajumbe wenzangu, kwa ushauri na busara zao zilizoniwezesha kama Mwenyekiti wa Kamati kuiongoza Kamati hii, Michango yao kwa wakati wote ilitolewa kwa uwazi na uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshukuru kwa dhati Kaimu Katibu wa Bunge, Ndugu Thomas Kashilila na Makatibu wake wasaidizi wa Kamati hii, Ndugu Michael Kadebe na Elieka Saanya, kwa kazi nzuri walioifanya ya kuratibu shughuli zote za Kamati. Pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuihudumia Kamati ipasavyo katika hatua zote za maandalizi ya taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha, ninaunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa hotuba nzuri. Sasa nitamuita Msemaji wa Kambi ya Upinzani na siyo mwingine ni Mheshimiwa Magdalena Sakaya. Nimearifiwa kwamba Kiongozi wa Kambi ya Upinzani anayekaimu sasa ni Mheshimiwa Abubakar Bakary.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kuchukua nafasi ya kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha leo hii kuwakilisha, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99 (7) toleo la 2007, maoni ya Kambi ya Upinzani, kwa Wizara ya Maliasili na Utalii,

kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2008/09. Aidha, natoa shukrani zangu kwako binafsi kwa kunipa fursa hii adimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi za Upinzani, natoa salaam za pole kwa ndugu, jamaa na watumishi wote wa Idara ya Wanyamapori, kwa kupoteza watumishi wenzao watatu katika ajali mbaya ya ndege iliyotokea tarehe 3/7/2008 huko Arusha. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuchukua fursa hii, kutoa shukurani zangu za dhati, kwa viongozi na wanachama wa Chama changu, kwa kuniwezesha kuwepo hapa kutetea haki na maslahi ya wananchi wa nchi yetu. Nawaahidi, nitaendelea kuwa mwaminifu na nitasimama kidete katika kuwatetea na kusimamia haki na rasilimali zetu mpaka dakika ya mwisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapa shukurani zangu za pekee viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid (Mb) na Naibu wake, Mheshimiwa Dr.Willibrod Slaa (Mb) kwa kunipa ushirikiano katika muda wote wa maandalizi ya hotuba yangu hii. Pia namshukuru Naibu wangu, Mheshimiwa Ali Khamis Seif kwa maandalizi ya hotuba hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutambua jitihada za Mheshimiwa Waziri, dada yangu, Shamsa Mwangunga (Mb.), kwa kazi kubwa anayoifanya kuhakikisha Sekta hii inatoa mchango mkubwa katika uchumi wa nchi , bila kumsahau Naibu wake Mheshimiwa Ezekiel Maige (Mb.), pamoja na timu nzima ya watendaji ikiongozwa na Katibu Mkuu wake, Mama Blandina Nyoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Mipango Katika Bajeti ya Mwaka 2007/2008. Katika kuyatekeleza malengo ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2007/2008, Bunge lako Tukufu lilipitisha matumizi ya Wizara kiasi cha shilingi 55,493,625,000/- ambapo kati ya fedha hizo shilingi 30,817,624,000/- ni kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo ambayo ilikuwa ni sawa na asilimia 55.5% na shilingi 24,676,001,000/- kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ambayo ilikuwa ni sawa na asilimia 44.5%.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa yangu hii iingie kwenye Hansard kama ilivyo kwa sababu ya muda inawezekana nikashindwa kusoma yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanyamapori. Tanzania ni nchi mojawapo iliyobahatika kuwa na wanyamapori wa kila aina ambao ni rasilimali kubwa kwa nchi yetu na ni muhimu sana katika kuchangia pato la Taifa. Hadi kufikia Machi 2008, sekta hii iliingizia Taifa jumla ya shilingi 10,554,562,182.77. Ingawa ninapata wasiwasi juu ya kiasi hiki cha makusanyo kwani kuna utofauti mkubwa unaojitokeza kati ya Kitabu cha Hali ya Uchumi 2007/08 ambacho kinaonyesha makusanyo yaliyotokana na wanyamapori yalikuwa 7,567,819,341/= na kile kilichowasilishwa kwenye Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ambacho kinaonesha hadi kufikia Machi 2008

makusanyo yote ya sekta hii ni 10,554,562,183/=, ambayo ni sawa na tofauti ya 2,986,742,842/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, utofauti huu mkubwa wa vitabu hivi viwili, umetupa wasiwasi mkubwa juu ya makusanyo sahihi ya sekta hii. Hivyo Kambi ya Upinzani, inamtaka Mheshimiwa Waziri, atueleze ni makusanyo ya kitabu kipi ambayo ni sahihi? Pia atupe ufafanuzi wa kina juu ya utofauti huu. Ni vema Serikali ikawa makini na takwimu zake kwani hizi takwimu ndizo zinazoletea hisia tofauti kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna njia nyingi kama Wizara ingekuwa na mipango madhubuti ingeweza kuongeza pato la Taifa. Kwa mujibu wa takwimu za Maliasili, kuna vitalu 163. Kwa wakati huu, Serikali inakodisha kwa wastani wa USD7500 (kwa miaka 3), mara nyingi wamiliki nao hukodisha kwa wenye fedha kwa wastani wa USD100,000 kwa mwaka. Mwaka 2007/2008, Kambi ya Upinzani ilipendekeza hatua zifuatazo zichukuliwe ili kuongeza mapato kama ifuatavyo :-

- Kuwajasirimisha Watanzania vitalu vyote vya uwindaji;
- Ili kupata thamani halisi washauriwe kuingiza vitalu hivyo katika soko la mitaji kwa kutumia *eletronic commerce*.

- Kupandisha viwango vya Kodi ya Uwindaji; na

- Kutoza asilimia 30% ya mapato yatokanayo na Mtanzania atakayekodisha kwa mtu mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu wa fedha, 2008/2009, Kambi ya Upinzani, inataka kupata Taarifa ya kina ni hatua zipi zimechukuliwa kati ya hizo na zimeipatia fedha kiasi gani na kama hakuna, ni sababu zipi hasa imeifanya Serikali kutokuchukua ushauri huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wizi uliokithiri unaofanywa kwenye sekta ya utalii, ambapo hotel za *Sopa Lodge* ambazo zinatoza ghali sana kwa wageni na zinapokea wageni wengi sana kwa siku, kwa mgeni mmoja zinatoza dolla 60-100 kwa mtu kwa siku. Lakini wanalipa dolla 1-3 kwa hifadhi husika na hawachangii chochote kuendeleza hifadhi hizo. Hali hii inapelekea kukosekana kwa fedha za kutosha kwa ajili ya uhifadhi na vile vile manufaa kwa rasilimali kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni ukwepaji wa ulipaji wa kodi kwa baadhi ya *Camp Operators*. Kuna *Camps* ambazo hazikulipa *Concession Fees* na *Park Fees* kwa miaka zaidi ya 10 na zimeendelea kufanya kazi. Mfano wa *Camps* ambazo hazikulipa kodi hizi ni kama zifuatazo:-

- *Tembo Camp* ambayo mwanzoni ikijulikana kama *Stieglers George:*

*Concession Fee* 1995-2005 (miaka 11) @ USD 12,000 = USD132,000.

*Minimum Park Fees* @ USD 30,000 = USD330,000.

- 3 *sites at Kinyanguru :*
  *Conservation Fee* kwa kila *camp* kwa mwaka USD 12,000.
  *Minimum Park Fee* kwa kila *camp* kwa mwaka ni USD 30,000.

- *Kinyaguru camp/ Hippo tours:*
  *Conservation Fees* kwa miaka 4 = USD12,000x 4 = USD 48,000.
  *Minimum Park Fee* 3= USD 30,000x3 = USD 90,000.

- *Ladwa Camp:*
  *Conservation Fee* kwa miaka 4 = USD12,000x 4 = USD 48,000.
  *Minimum Park Fee* kwa miaka 3 = USD 30,000x3 = USD 90,000.

- *Pilot camp:*
  *Conservation Fee* kwa miaka 4 = USD12,000x 4 = USD 48,000.
  *Minimum Park Fee* kwa miaka 3 = USD 30,000x3 = USD 90,000.

- 2 *Other Ladwa site:*
  *Conservation Fee* kwa miaka 4 = USD12,000x2x 4 = USD 48,000.
  *Minimum park fee* kwa miaka 3 = USD 30,000x2x3 =USD 90,000.

- *Beho Beho Camp:*
  *Concession Fee* imelipwa.
  *Minimum Park Fee* 1995-2005 (miaka 11) = USD 30,000x11 = USD 330,000.

- *Sites* 5 mpya ambazo wamepewa operators wapya na Mkurugenzi wa wakati huo:
  *Conservation Fee* = USD 12,000x5 = USD 60,000.

Jumla ya fedha zote ambazo hazikulipwa ni *USD* 1,542,000 ambayo ni sawa ni Tshs 1,850,400,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inamtaka Mheshimiwa Waziri aeleze kama kweli zabuni ya wazi ilifanyika, je, ni kiasi gani cha fedha kililipwa kwa Serikali?

Pili, fedha hizi zote zimekwenda wapi kama kweli zililipwa? Kama hazikulipwa, ni kwa vipi au nani aliwapa ruhusu ya kuendelea na biashara kinyume na Sheria na mpango mkuu wa usimamizi wa *Selou Game Reserve*? Watanzania wanahitaji ufafanuzi wa kina katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu hizi, tunaweza kuona ni kiasi gani nchi yetu inavyoporwa. Watumishi tuliowapa dhamana ya kusimamia na kutunza rasilimali zetu badala yake wakiangaliana au kushirikiana na wawekezaji wasio waadilifu au kwa kushindwa kuweka miongozo sahihi yenye maslahi kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwezesha sekta hii muhimu kuongeza pato la Taifa zaidi inavyochangia sasa, Waziri aliyepita Mheshimiwa Profesa Maghembe, alitembelea nchi nyingi na kuangalia jinsi wanavyoendesha suala zima la uwindaji wa kitalii. Aligundua utofauti mkubwa sana wa bei za vitalu pamoja na wanyamapori kati ya wenzetu na sisi. Serikali ilileta mapendekezo ya bei mpya za wanayamapori hapa Bungeni na Bunge lako Tukufu liliridhia kwa furaha kubwa ili Taifa na wananchi wake liweze kufaidika na uwindaji wa kitalii tofauti na ambavyo miaka yote makampuni ya kitalii ndio yamekuwa yananufaika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kushangaza, Wizara ilibadili bei hizo kinyemela na kurudia bei za awali bila hata Bunge kufahamishwa. Kwa taarifa tulizo nazo, hii ilitokana na shinikizo la wafanyabiashara wenye makampuni ya uwindaji ambao lengo lao ni kuendelea kufaidika zaidi. Hawana uchungu na rasilimali hii wala wananchi wanaoendelea kuteseka na hali ya umaskini. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kulieleza Bunge na Watanzania kwa ujumla ni vigezo gani vya msingi vilivyopelekea kubadilishwa kwa viwango vilivyoridhiwa hapa Bungeni? Ni kwa nini maamuzi ya Bunge yabadilishwe nje ya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kuwa kabla ya pendekezo la bei mpya kuletwa Bungeni, utafiti ulifanyika wa kutosha. Pia ni ukweli uliowazi kuwa pamoja na nchi yetu kuwa na wanyama wengi, wa aina mbalimbali, wanene na wanaoishi kwenye mazingira halisia, sifa hizi zinaifanya Tanzania kuwa nchi ya pekee na hivyo kuwavutia wawindaji kutoka sehemu mbalimbali za Ulimwengu kuja kuwekeza kwenye sekta hii ya uwindaji. Lakini bei za wanyama wetu zimekuwa chini sana ukilinganisha na nchi nyingine za Bara la Afrika na hivyo kusababisha Taifa kutonufaika na maliasili hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupata maendeleo ya kweli katika sekta hii, ni muhimu sana kuwepo kwa mipango madhubuti na watendaji wabunifu na wanaoaminika. Kuna mifano mingi inayoonyesha majirani zetu wameendelea sana kwa rasilimali hii na ukizingatia kwamba sisi tuna rasilimali zaidi ya wao, hii imetokana na mipango madhubuti walionayo wenzetu na watendaji wabunifu na kuweza kuingizia pato kubwa la nchi. Mfano mzuri ni Afrika Kusini, ada yao ya kuulia mnyama aina ya *cape buffallo'* ni US *$ 16,200,* wakati Tanzania ni US$ 2200. Ada ya kuulia *Nyasaland wildbeest* Afrika Kusini na Namibia ni us $ 1100, wakati kwetu Tanzania ni us$750.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya mambo muhimu ya kuendeleza wanyamapori, ni wanajamii kuwa na elimu ya kutosha na ufahamu juu ya umuhimu wa wanyamapori, pia kushirikishwa kikamilifu katika suala zima la uendelezaji wa sekta hii kuanzia upangaji wa sera na ushirikishwaji kwenye mgao wa mapato kwani wao ndio waangalizi wakubwa wa wanyama hao pia wanaweza kuwa waharibifu wakubwa ikiwa watadharauliwa na kukosa elimu ya kutosha. Sekta nyingi nchini zinashindwa kufikia malengo yaliyowekwa kwa sababu ya kuwatenga wanajamii au kuwashirikisha lakini kwa njia ya maneno na si kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Wanyapori inaeleza kuwa asilimia 25 ya pato litokanalo na wanyamapori lirudi kwenye Halmashauri zinazozunguka maeneo hayo ili ziweze kuendeleza uhifadhi pamoja na wananchi kunufaika na rasilimali hiyo. Kambi ya Upinzani, inataka kupata maelezo kwa nini Halmashauri 13 kati ya 44 zinazozunguka maeneo ya hifadhi hazikupata mgawo wa asilimia 25 mwaka 2007/08, wakati fedha zilikusanywa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika historia za nchi zetu za Afrika, hakuna jambo lolote lenye lengo la kuleta maendeleo kwa wananchi kufanikiwa bila ya ushirikishwaji wa wanajamii kikamilifu. Mfano mzuri ni nchi ya Ghana, kabla ya mwaka 1920, walikuwa wanaendeshwa na Sera ya *Wildlife Community Base* na mafanikio makubwa yalipatikana. Mwishoni mwa miaka ya 1980s, Ghana walianzisha Sera mpya za Umiliki Binafsi na matokeo yake kiasi cha zaidi ya 70% ya misitu, iliharibiwa na wanyamapori wengi walitoweka na hii ilipelekea hadi leo hali ya wanyamapori kuwa ni ya wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na athari hizo mbaya, nchi kama Namibia, wako mbioni kubadilisha mfumo mzima wa Katiba kwa ajili ya kuwashirikisha kikamilifu wanajamii baada ya maendeleo mabaya yaliyotokana na mfumo wa awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa wanavijiji katika suala zima la uhifadhi, Kambi ya Upinzani, inaiomba Serikali kuziwezesha jumuiya za vijijini kuweza kumiliki na pia kusimamia wanyamapori, kutoa msaada unaohitajika katika kuzipatia jumuiya za vijijini miliki na kuweka mipango ya matumizi ya wanyamapori, kuwalazimisha wafanyabiashara wenye leseni kuajiri vibarua kutoka maeneo ambayo shughuli za matumizi ya wanyamapori zinafanyika kwa lengo la kuwapatia ajira na kunyanyua mapato yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni nchi inayoongoza duniani kwa kuwa na sera nzuri na za kuvutia. Kwa bahati mbaya, utekelezaji wake unaishia kwenye makaratasi na majukwaani kwa wanasiasa. Kwa upande mwingine ni miongoni mwa nchi chache kwa kutokutekeleza sera zake. Mfano halisi ni kuwa kwenye kitabu cha sera za wanyamapori, zimeorodheshwa sera nyingi nzuri ambazo kama ingekuwa kuna utekelezaji basi leo hii tusingekuwa hapa tulipo. Moja ya malengo ya sera za wanyamapori ni kama zifuatavyo nanukuu:-

*"Kushirikiana na kutumia vyema ushirikiano na jamii za vijijini, kukabidhi madaraka ya wanyamapori kwa jumuiya za vijijini, kuruhusu jumuiya za vijijini kufaidika*

*na miradi ya uhifadhi na kushirikishwa kwa jamii za vijijini na wadau wengine katika usimamizi wa rasilimali za wanyama pori"* mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama sera hizi zingekuwa zinafuatwa na kutekelezwa kikamilifu basi leo hii wananchi wanaoishi kuzunguka maeneo yenye rasilimali ya wanyamapori, wangekuwa na hali nzuri ya maisha tofauti na walivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo jingine ni lugha inayotumika katika kuandaa sera zetu. Lengo kuu la sera za Serikali, ni kuwafikia wananchi ambao ndio walengwa wakuu. Jambo la kushangaza, sera hizo zimeandikwa kwa lugha ya kigeni ya kingereza ambayo wananchi wengi hawaifahamu vizuri. Hivyo basi, watawezaje kuyafahamu na kuyatekeleza yaliyomo ndani ya sera? Zaidi ya hayo, sera hizi zinaishia maofisini kwenye makabati tu haziendi vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuzitafsiri sera hizi kwa lugha inayofahamika na wananchi na kuzisambaza kwa wananchi hasa zile sehemu ambazo zilizozunguka hifadhi za wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la uhifadhi wanyamapori, njia/mapito ya wanyama, ni suala muhimu sana kwani hutumiwa na wanyama kuhama kutoka eneo moja kwenda lingine kwa shughuli mbalimbali, ikiwemo kufuata malisho pamoja na kwenda kuzaliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya miaka 40, Wabarbaig wamekuwa wakiishi vizuri katika njia kuu ya wanyama inayounganisha Tarangire na Ziwa Manyara bila matatizo na njia hiyo wanyama wameendelea kuitumia hadi leo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji hicho ambacho kina zaidi ya familia 70, kimehamishwa kwa nguvu na eneo hilo limeuzwa kwa mwekezaji wa Kifaransa anayejulikana kama *EN-Lodge Afrique*. Amepewa eneo la hekta 4,084 za kijiji cha Vilima-vitatu kwa lengo la kujenga hotel katika njia ambayo hupitisha wanyamapori toka na kurudi Tarangire na ziwa Manyara, tena bila wanakijiji kushirikishwa katika uamuzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kutoa maelezo ya kina ni kwa nini *hotel* hiyo ijengwe katikati ya njia hiyo ya wanyamapori na kwa nini Wanakijiji hao wameondolewa kwa nguvu bila kufuata utaratibu unaoeleweka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utalii ni miongoni mwa sekta ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Tanzania imebahatika kuwa na eneo la ufukwe lipatalo kilomita 804, maporomoko ya maji, mito mikubwa, chemchem za maji moto *(hot spring water )*, hifadhi za wanyama zilizokusanya wanyama mbalimbali, sura ya nchi na hali ya hewa nzuri, ambayo ni muhimu kwa kuvutia watalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya umuhimu wa sekta hii, lakini bado mchango wake ni mdogo katika kuchangia pato la Taifa licha ya vivutio vingi tulivyonavyo

ukilinganisha na nchi nyingine, hadi sasa sekta hii inachangia si zaidi ya 17% katika Pato la Taifa (*GDP*), ambalo ni dogo sana hasa ukizingatia rasilimali tulizonazo ni za kipekee duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mifano hai ya nchi ambazo hata si maarufu kwa Utalii na hazina vivutio ukilinganisha na Tanzania lakini kutokana na mipango mizuri walionayo, sekta hii imeweza kuchangia na kunyanyua pato lao kwa kiasi kikubwa, mfano mzuri ni Namibia, India, hata Zambia ambayo wala si maarufu kabisa kwa sekta hii ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya Wizara kujisifia juu ya sekta hii, lakini hali ya kushangaza na ya kusikitisha, ni kuwa katika nchi 15 za Sub-Sahara (nchi za Ukanda wa Jangwa la Sahara) ambazo ni maarufu kwa kujishughulisha na sekta hii ya utalii basi nchi yetu ni ya tatu kutoka mwisho, imeshindwa hata na majirani zetu wa Kenya. Ama Katika nchi 20 ambazo ni maarufu kwa utalii katika nchi zinazoendelea basi Tanzania haipo kabisa na inashindwa na hata nchi ya Zimbabwe. Katika nchi 50 zinazoendelea, Tanzania ni ya 19 ambapo tumepitwa na Kenya, Msumbiji, Madagaska, Mali, Ethiopia na Nigeria. *(We maintain peace and stability yet development remains patchy).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa ajira, ilitarajiwa sekta hii iwe ni mfano kwa sekta nyingine kwa kufungua nafasi nyingi zaidi za ajira kwa wazawa na kuweza kupunguza na kama si kuondosha kabisa tatizo la ajira nchini, lakini hali ni tofauti, hii inatokana na kutokuwepo kwa manufaa ya pande zote kwenye mzunguko wa uzalishaji na sekta hii, ukilinganisha na nchi nyengine zinazoendelea kwa mfano nchi ya India inachangia 4.1% na jumla ya watu walioajiriwa ni zaidi ya 25 million mbali ya ajira hizo, ajira nyingine ambazo zimechangiwa kutokana na sekta hii ni 38.6 milioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa Serikali itahakikisha mahusiano ya moja kwa moja ya sekta ya utalii na sekta nyingine kama vile kilimo na ufugaji basi tutaweza kusaidia sana wakulima na wafugaji kunufaika sana na sekta hii kwa kupata soko zuri la mifugo yao, nafaka zao, matunda na mboga mboga na hivyo kuinua hali za maisha za Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la ajabu katika hoteli zetu nyingi za utalii, wanaagizia nje karibu vyakula vyote vikiwemo vitoweo, nafaka, matunda na hata mboga mboga. Hii ni kwa nini? Mfano mwaka 2007, tumepata wageni 719,031 na kama tutakadiria kwa mgeni mmoja kwa mlo wa asubuhi atakula mayai mawili kwa wastani wa kila yai ni Tsh. 200 basi tungewaingizia wafugaji hawa kiasi cha Tsh. 287,612,400. Kwa mlo wa usiku ikiwa kila mgeni mmoja atakula nusu kuku na kwa kila kuku mmoja anagharimu Tsh 5,000, basi tungeweza kuwaingizia wafugaji hawa kiasi cha Tsh. 1,797,577,500. Kwa mantiki hiyo, tunaweza kuinua hali ya uchumi kwa wafugaji wa kuku wa Mkoa wa Singida kwa kuuza kuku na mayai ya kienyeji tu. Vivyo hivyo kwa vitu vyingine kama vile matunda, mboga, nafaka na mazao mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kukosekana kwa miundombinu mizuri, watalii wengi wamekuwa wanashukia Kenya, wanamalizia siku zao huko na kupita Tanzania

wakiwa wanarudi makwao. Mfano mzuri watalii wengi wanafika hifadhi ya Masai Mara kama kituo kikuu cha utalii na kuifanya hifadhi ya Serengeti kama kipitio tu (*transit*).

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaleta athari kubwa katika ukusanyaji wa mapato na unyanyuaji wa uchumi wa nchi, katika mwaka 2006/07 Masai mara ilikusanya *US D.* 750 milioni, wakati mbuga yetu ya Serengeti imekusanya *USD 30* milioni ambao ni sawa na tofauti ya *US$ 720* milioni ambazo ni sawa na Tsh B.864.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda ifahamike kuwa maendeleo mazuri ya utalii kwa nchi wenzetu kama ya India, hayakuja kirahisi bali yanatokana na mipango mizuri waliyonayo wenzetu. kwa mfano, nchi ilianzisha *India Railway Catering and Tourism Development Corporation Limited* tokea 1999, ambayo huwa inatumika kutoa huduma za usafiri wa treni kwa watalii kuwafikisha sehemu zinazotakiwa, kuboresha na kuanzisha ushindani wa mawasiliano, ukarabati wa viwanja vya ndege, kuanzishwa kwa '*Pradhan mantra Gram sadak yojaina*' kwa ajili ya kuboresha na kurahisisha maingiliano na maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa juhudi zinazochukuliwa na Wizara kuitangaza Tanzania na vivutio vyake ni matumaini yetu kuwa watalii wataanza kuongezeka. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali iangalie kwa makini suala la kuongeza hoteli nyingi na zenye hadhi ya juu ili kuongeza ushindani. Aidha tunatoa angalizo ujenzi wa hoteli uzingatie uhalisia wa hifadhi zetu na athari zake kwa mazingira yanayozunguka hifadhi. Pia taratibu zote lazima zifuatwe na kutilia maanani maslahi ya Taifa na wananchi wake. Sambamba na hayo kuboresha mambo muhimu ambayo yatapelekea kuleta maendeleo ya sekta hii ikiwa ni kuwa na usafiri wa uhakika, mawasiliano, mahoteli na wahudumu waliopewa elimu ya kutosha na ambao watatoa ushindani wa kutosha kwenye sekta hii inayokuwa kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inadhihirika pale ambapo majirani wetu wa Kenya kwa mwaka 2007 kabla ya uchaguzi waliingiza watalii wa kimataifa wapatao milioni mbili huku nchi yetu tunatarajia tutafikia kiwango cha milioni 1.2 ifikapo 2012 kutoka 700,000 mwaka 2007/08, hii inaonyesha kiwango cha watalii wanaongia Kenya tutakifikia mnamo mwaka 2020. Hivyo, hii inathibitisha kuwa tuko nyuma kimaendeleo katika sekta ya utalii kwa muda wa miaka 12 ukilinganisha na Kenya. Tunahitaji mpango madhubuti wa kubadilisha sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999, inakataza Ardhi kumilikishwa kwa wageni. Wawekezaji wageni, wanakodishiwa ardhi kwa muda fulani wa makubaliano. Kitendo cha Serikali kummilikisha mwekezaji *Reserve* ya Grumeti na akajenga *VIP HOTEL* ndani ya *reserve* hiyo yenye eneo la kilomita za mraba 149, ni kinyume na utaratibu na kanuni za nchi. Kambi ya Upinzani, inataka majibu kutoka kwa Serikali, ni taratibu gani zilifuatwa kumilikisha ardhi ya wananchi wa Mkoa wa Mara kwa mwekezaji huyo raia wa Marekani Ndg. Johnes *Tudor*.? Kuna usiri mkubwa wa shughuli zinazofanywa kwenye eneo hili na mtu yeyote haruhusiwi kuuliza. Tuna wasiwasi hata mapato yanayokusanywa na Serikali kutoka eneo hili siyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwekezaji huyu amekuwa anawanyanyasa sana wananchi wanaozunguka eneo hilo. Amekuwa anatumia Askari wake kuwapa kipigo kikali mwananchi yeyote anayekutwa hata jirani na eneo lake. Kumekuwepo na malalamiko kuwa Askari hawa wanawalazimisha wananchi kula nyama mbichi pale wanapokamatwa na mnyama. Hii ni haki kwa nchi inayoendeshwa kisheria? Ni kwa nini Watanzania wanyanyaswe ndani ya nchi yao? Jamaa huyu ana jeuri ya ajabu, hatuelewi anapata wapi kiburi hicho? Amefikia hatua ya kukataza Kamati ya Bunge kufanya kazi zake ndani ya *hotel* kwa kisingizio kuwa watasumbua wageni wake!

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana Kamati tulitembelea wananchi waozunguka eneo hilo, tulipata malalamiko mengi sana kutokana na manyanyaso wanayopata kutoka kwa mwekezaji huyu.Wakati wa kikao kati ya Wabunge na Uongozi wa *hotel*, Mkuu wa Wilaya, alionyesha wazi kumtetea mwekezaji na kwaacha wananchi wake. Kwa taarifa tulizo nazo ni kwamba, mwekezaji mahusiano yake ni yeye na viongozi wa juu tu hana habari na wananchi yeyote. Tunaitaka Serikali ifuatilie suala hili na kutupatia majibu hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuangalia upya uwekezaji wa mahoteli makubwa yanayojengwa ndani ya hifadhi kwani yanaharibu uhalisia wa mbuga zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2007 katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mali Asili na Utalii katika kipengele cha changamoto zinazotukabili katika sekta ya Utalii alilieleza Bunge lako Tukufu kwamba Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa itaanza rasmi ujenzi wa chuo kipya cha Utalii mwezi Agosti, 2007 ambao utachukua mwaka mmoja kukamilika ukurasa wa 110. Lakini katika Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Waziri mwaka 2008 ameeleza kuwa ujenzi wa chuo hicho cha Utalii ndio kwanza unaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Kambi ya Upinzani inataka maelezo ya kutosha juu ya ucheleweshaji wa ujenzi wa chuo hicho ambacho mwaka huu kilikuwa kinatarajiwa kiwe tayari kimeshakamilika. Kambi ya Upinzani pia ina wasiwasi juu ya kutengwa tena kwa bajeti ya chuo hiki kwa mara ya pili baada ya bajeti 2007 ya chuo kutokumalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya rasilimali tuliyojaliwa ni uwepo wa Ziwa Natron lililotengwa chini ya mkataba wa kimataifa wa kuhifadhi ardhi oevu mwaka 2001. Eneo hili linalokadiriwa kuwa na ndege wa aina ya Heroe wadogo *(lesser flamingoes)* wapatao milioni 2.5. Kiasi cha asilimia 70 ya ndege hawa duniani huzaliana hapa. Ni ndege wa pekee wanaopenda utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la ajabu kuona Serikali inataka kuteketeza mazalia haya na kuwafukuza ndege hawa ambao hawapatikani mahali pengine popote na wamekuwa ni kivutio kikubwa kwa watalii hapa Tanzania.

Uridhiwaji wa ujenzi wa kiwanda cha magadi na Serikali ndicho chanzo cha kuwafukuza ndege hawa, hata kiwanda kikijengwa mbali, lakini malighafi yatatoka katika ziwa hili na hivyo kusababisha usumbufu kwa ndege hawa. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutambua kwamba zipo njia nyingine za kuongeza Pato la Taifa bila kusababisha uharibifu wa mazingira wala kupoteza maliasili zetu tulizopewa na Mwenyezi Mungu. Tunasisitiza Kiwanda kisijengwe kama hakuna eneo lingine la kupata malighafi zaidi ya ziwa *Natron*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imebahatika sana kuwa na rasilimali kubwa ya misitu ambayo ni hazina kubwa kwa maendeleo endelevu ya nchi yetu, afya na mazingira kwa ujumla ingawa Serikali hawaitumii sana sekta hii inavyotakiwa. Nchi yetu ina takriban hekta milioni 33.3 za misitu. Kati ya hekta hizo, Serikali imetenga na kuhifadhi kisheria hekta millioni 13 katika sehemu mbalimbali na eneo la hekta millioni 20.3 hazikuhifadhiwa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya sekta hii kwa kiasi kikubwa yanategemea sana ushirikishwaji wa jamii na uwepo wa mwamko juu ya umuhimu wa misitu kwa maendeleo ya nchi. Serikali inatakiwa kuishirikisha jamii kikamilifu katika ngazi zote kuanzia utunzaji, utaratibu wa uvunaji na hata kwenye mapato na sio katika uhimizaji wa upandaji wa miti tu. Kwani wanavijiji hao wana uwezo mkubwa wa kusaidia katika kuzitumia mila na tamaduni zao katika utunzaji wa rasilimali hizi bila hata ya kutumia gharama yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kutokushirikishwa wananchi kikamilifu kwa jamii katika sekta hii, athari zake ni kubwa, kwani uchambuzi unaonyesha kuwa ukataji holela wa misitu umeongezeka kutoka hekta 300,000 hadi 400,000. Leo hii ndio maana Tanzania imekuwa nchi ya nne duniani kwa uharibifu wa misitu ikiongozwa na Indonesia. Hali hii ni hatari kwa usalama wa maisha na kizazi kijacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya misitu pia inakabiliwa na matatizo kama vile uhaba wa watendaji, elimu ndogo kwa watendaji, rushwa iliyokithiri, kutokuwajibika na kukosekana kwa uaminifu kwa baadhi ya wafanyakazi na ushirikishwaji mdogo wa wadau katika mambo muhimu ya maendeleo ya sekta. Hivyo Kambi ya Upinzani inaitaka Wizara kuyatekeleza mambo yafuatayo ili iwe ni chachu ya maendeleo kwa sekta:-

Kuwapatia elimu ya kutosha wafanyakazi wa idara ya misitu, ikiwa ni pamoja na kuwapa maadili ya kazi;

Kuwepo kwa uwazi wa kusahihi mapato wa ukusanyaji wa mapato;

Kuwahusisha wadau muhimu katika usimamizi wa misitu;

Kuwepo kwa mipango mizuri ya uvunaji maliasili yetu, unaofuata sheria;

Kubuni vianzo mbadala vya fedha kama ulipaji na matumizi ya huduma za mazingira; na

- Sheria ichukue mkondo wake pale mtumishi yeyote anapogundulika kwamba amekwenda kinyume na taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vyanzo na njia nyingi za kuweza kuongeza mapato katika sekta hii ya misitu. Chanzo kikubwa ambacho mapato yake hayakusanywi kikamilifu ni bidhaa za magogo na mbao. Katika taarifa za kiutafiti kutoka kwa kundi la wahisani na pia Asasi kadhaa zisizo za kiserikali, (Kama *TRAFFIC)* (2005/2006) wametoa mapendekezo mbalimbali pia katika hotuba yetu ya Mwaka jana tulitoa ushauri jinsi ya kukusanya mapato zaidi kwenye sekta ya misitu na Serikali imeshindwa kabisa kutumia fursa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo kwa njama na kulindana katika asasi mbalimbali za Serikali na Sekta binafsi sio tu kumeendelea kuwahusisha watu muhimu katika Wizara ya Maliasili na Utalii bali hata wafanyabiashara wa mbao kwenye chama chao cha wasafirishaji wa mbao nje ya nchi. Hii ni moja ya mambo yaliyobainishwa kwenye taarifa ya *TRAFFIC,* mambo ambayo bado hadi sasa yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka kuelewa taarifa ya *TRAFFIC* iliyowasilishwa kwenye Semina ya Wabunge mwaka 2007, yenye mapendekezo kuhusu njia za manufaa kupata mapato yatokanayo na sekta hii. Je, ni kwa kiasi gani Serikali imeyatekeleza?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Sheria kukataza usafirishaji wa miti aina ya mipingo *(African Black wood)* mwaka 2007 jumla ya *container* 52 za mipingo zilisafirishwa kupitia Bandari ya Dar es Salaam. Kambi ya Upinzani inataka Serikali itoe majibu ni hatua zipi zimechukuliwa kwa wahusika au kurejesha magogo hayo au tunasubiri tukanunue vinyago na mapambo ya mipingo kutoka Asia wakati miti hiyo Mungu ametupa Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tumeuza viwanda vyetu vya mbao na sasa tunanunua samani zisizo na ubora kwa gharama kubwa kutoka nje, wakati magogo na mbao vinapelekwa nje kwa bei karibu na bure. Kambi ya Upinzani inataka kujua hatma ya viwanda vya mbao vilivyokuwa chini ya *TWICO* baada ya kubinafsishwa, vinaendelea kufanya kazi ya kuchakata mazao ya misitu au ilikuwa ni njama ya kuviua na kuwakosesha ajira Watanzania ajira?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilipopiga marufuku usafirishaji wa magogo nje, magogo yaliyokuwa tayari yamekatwa na yalikuwa porini, hatua gani zilichukuliwa na Taifa limepata kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani pia inataka kujua tangu Januari, 2006 hadi Juni, 2008 kwa utaratibu mpya uliowekwa wa uvunaji wa mazao ya misitu, magogo na mbao kiasi gani kimesafirishwa nje na nchi zipi na imepata kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka majibu ya timu iliyoundwa na Serikali na kutumwa China kwenda kuchunguza ni kiasi gani cha magogo kinauzwa nje na kwa bei gani na *cubic* mita moja, kwani Serikali iliahidi hapa Bungeni kuwa ndani ya wiki mbili ingetoa taarifa , lakini hadi leo bado.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya upinzani inaishauri Serikali bidhaa za mazao ya misitu yaongezewe thamani hapa nchini ili Watanzania wengi wapate ajira na kuviwezesha viwanda vyetu kufanya kazi ya kutengeneza samani na kuziuza nje. Tuachane na utaratibu usio na tija tunaoutumia sasa wa kuwasafirisha magogo na mbao kuwapelekea Wachina, wao wanatengeneza samani na kutuletea hapa na tunazinunua ghali sana, tuamke tubadilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka hatua zifuatazo zichukuliwe:-

(i) Halmashauri za Wilaya zilizo katika maeneo ambayo bidhaa hizi zinapatikana ziwe mawakala wa kukusanya mapato kutokana na bidhaa za maliasili. Uamuzi huu utapunguza kwa kiasi kikubwa ufisadi uliopo sasa katika Wizara ya Maliasili. Kila Halmashauri inayokusanya kodi ipatiwe gawio kutoka sehemu ya makusanyo;

(ii) Mapato yote yakusanywe na *TRA* kwa kutumia stakabadhi za *TRA* kupitia Halmashauri za Wilaya kama ilivyo elezwa hapo juu;

(iii) Mtu yeyote atakayekamatwa kwa kutorosha maliasili afilisiwe kwa mujibu wa sheria, kama haipo itungwe; na

(iv) *TRA* mbali na kukusanya mapato, ishirikiane na Bodi ya Mauzo ya Nje kuhakiki bei za bidhaa zetu zinazouzwa nje ili kupata mapato halali ya rasilimali zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya ufugaji wa nyuki ni muhimu katika kuchangia juhudi za kunyanyua pato na uchumi wa Tanzania ingawa sekta hii haipewi msukumo kama inavyostahili. Lakini umuhimu wake ni mkubwa kwa jamii na kwa maendeleo ya nchi kwa ujumla. Sekta hii imekuwa inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwepo uvunaji usio endelevu wa misitu, kufyeka na kuchoma misitu, upungufu wa wataalam, upatikanaji wa taarifa sahihi na ukosefu wa masoko ya uhakika imekuwa ni kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya ufugaji nyuki wenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji wa nyuki wamekuwa wakipata matatizo makubwa ya ardhi kwa sababu ya kutokuwa na maeneo ya ufugaji yanayotambulika kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jumla ya idadi yote ya mavuno karibu asilimia 75 ya mavuno haya yanauzwa katika masoko ya nyumbani na asilimia 25 tu ndio yanayosafirishwa nje ya nchi, kwa mfano, katika mwaka 2007/2008 tani 413 tu za nta kwa mwaka ndizo zinazosafirishwa nje. Hii inaonyesha jinsi gani sekta hii inavyohitaji

msukumo mkubwa toka Serikalini hasa suala la kuwatafutia wafugaji masoko ya nje na kuweza kuitangaza biashara hii kwa ajili ya kuwawezesha wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu inakadiriwa kuwa na uwezo wa kuhifadhi makundi ya nyuki karibu milioni 10 katika maeneo mbalimbali ya misitu na mashamba. Maeneo haya yangeweza kuzalisha tani zipatazo 9,200 za nta na tani 138,000 za asali kama Serikali ingelielekeza nguvu zake katika sekta hii. Katika mwaka 2007/2008 Wizara iliarifu uuzaji wa tani 413 tu za nta ambazo ni kidogo sana ukilinganisha na idadi ya makundi ya nyuki yaliomo katika mashamba na misitu mbalimbali nchini ambayo ilikuwa ni sawa na asilimia 4.5 kwa maana nyengine asilimia 95.5 hazijazalishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata bei wanayopewa wafugaji hawa wa nyuki hairidhishi ukilinganisha na ubora wa hali ya juu na uhalisia wa bidhaa hii na ya kipekee inayozalishwa nchini na kazi kubwa wanayoipata wafugaji hawa hadi kupatikana kwa mavuno hayo. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iangalie tena upya uhalisia wa bidhaa hii na kazi kubwa na ngumu wanayoipata wafugaji na hivyo kuwatafutia soko zuri na la uhakika pamoja na vifaa vya kisasa vya ufugaji wa nyuki ili ufugaji wao uwe na tija na hivyo kuinua hali zao za maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza kuhifadhi na kuendeleza maeneo ya mambo ya kale kiutalii mwaka 2007/2008 Wizara ya Maliasili na Utalii iliahidi kuweka umeme na maji katika Kituo cha Amboni na Olduvai kwa ajili ya kuboresha zaidi.

Kambi ya Upinzani inaona wazo hili ni zuri na ingelisaidia katika kuvifanya vituo hivi viwe vya kisasa na kuweza kuwavutia watalii zaidi wa ndani na nje ya nchi. Kambi ya Upinzani inauliza: Mbona hakuna mabadiliko yoyote ya kimaendeleo katika sehemu hizi ambazo ni rasilimali kubwa kwa Taifa hili? Lakini zaidi ya yote, Serikali imeshindwa kuboresha kabisa sehemu hizi zaidi ya kujikaza kwa ukusanyaji wa mapato. Ingawa wanasema mwanzo wa safari ni hatua, lakini mbona matayarisho na dalili za safari hazionekani? Pia wanadai kuwa ukiweza kujenga mlango wa nyasi, basi wa chuma unafuatia, mbona miaka inapita na nyasi zenyewe zinaanza kuliwa na mchwa? Dalili ya mvua mawingu, mbona kuko shwari?

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imebahatika kuwa na vivutio vingi sana vya mambo ya kale, lakini bado havijatangazwa wala kuendelezwa na mifano mizuri ni ya Magofu ya Kilwa Kivinje yameanguka na mengine yamemilikiwa na watu binafsi na Serikali inayafahamu haya, lakini inaendelea kukaa kimya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa sekta hii kwa maendeleo la Taifa hili, Kambi ya upinzani inafikiria kuna umuhimu mkubwa wa kuitangaza sekta hii katika nchi za nje kwa ajili ya kukuza soko na pato la Taifa kwa ujumla, kwani kuna mambo mengi yanayohusiana na mambo ya kale bado hayajulikani kitaifa wala kimataifa. Hivyo katika kukuza sekta hii Kambi ya Upinzani inashauri yafuatayo:-

- Kusambaza picha na mikanda ya video mbalimbali zinazohusu mambo ya kale ndani na nje ya nchi;

- Kuweka majarida mbalimbali na vitabu ambavyo yanazungumzia mambo ya kale;

- Kuajiri watumishi wa kutosha na kuwapatia mafunzo kuhusiana na mambo kale ili kuleta ufanisi;

- Kuboresha na kuyatunza maeneo ya kale kwa ajili ya kuvutia watalii; na
- Kuwashirikisha wanajamii kikamilifu kuanzia utunzaji hadi ugawaji wa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna uhifadhi endelevu bila kuwepo utafiti. Ni utafiti ndio utakaotufanya tuelewe mwelekeo wa hifadhi zetu na viumbe vinavyoishi katika hifadhi hizo pamoja na bahari na maziwa. Baadhi ya Taasisi zinazofanya utafiti katika sekta hii ni *Tanzania Wildlife Research Institute (TAWIRI)* na *Tanzania Forestry Research Institute* (*TAFORI).* Pamoja na umuhimu mkubwa wa Taasisi hizi katika suala zima la uhifadhi bado zimekuwa zinatengewa fedha kidogo sana na hata hizo kidogo zinatoka kwa wahisani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutegemea fedha za wahisani katika utafiti ni hatari mno kwani ni dhahiri kabisa pale ambapo wahisani hao wanasitiza misaada yao na miradi mingi ya utafiti haifanyiki. Ni muhimu Serikali ikahakikisha inatenga fedha za kutosha kwa ajili ya Tasisi za utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata wakati mwingine fedha zinazotolewa kwenye Taasisi hizi zinakuwa hazina mipangilio mizuri na kutolewa kwa wakati zinapohitajika. Mfano mzuri ni pale Wizara ilipotenga kiasi kikubwa cha fedha na kupelekwa *TAWIRI* kwa ajili ya kutafuta idadi ya mamba nchi nzima (Mapitio ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo na bajeti ya mwaka 2007/2008 ukurasa wa sita), huku katika hotuba ya Waziri wa mali asili na Utalii 2007/2008 ukurasa wa 71 ikionesha idadi ya mamba tayari imeshajulikana ambao ilikadiriwa kuwa 72,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona utafiti huo ulikuwa ni ufujaji na uharibifu wa fedha za wananchi. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri atueleze kulikuwa na umuhimu gani wa utafiti huo na idadi kamili ya mamba hao ilikuwa inajulikana? Je! hakuna tafiti nyingine muhimu ambazo zingeweza kufanyika?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inahitaji majibu ya hoja zifuatazo kutoka Serikalini.

(1) Wizara itueleze tofauti ya mapato ya wanyamapori iliyopo kwani hadi Machi, 2008, mapato yalikuwa ni shilingi bilioni 10.554 kwa mujibu wa Wizara, wakati kitabu cha Hali ya Uchumi 2007/2008 ni shilingi bilioni 7.567;

(2) Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri aeleze kama kweli zabuni ya wazi ilifanyika kwa *camps* za *Selous:* Je, ni kiasi gani cha fedha kililipwa kwa Serikali?;

(3) Pili, fedha hizi zote zimekwenda wapi kama kweli zililipwa? Kama hazikulipwa ni kwa vipi au nani aliwapa ruhusu ya kuendelea na biashara kinyume na sheria;

(4) Kwanini Serikali ikaruhusu kujengwa *EN LODGE AFRIQUE* kwenye njia ya kupitia wanyama kati ya Tarangire na Ziwa Manyara?

(5) Kwanini Serikali ikammilikisha ardhi Johnes Turdor wa Marekani eneo la kilometa za mraba 149 kinyume na sheria ya ardhi ya mwaka 1999?

(6) Serikali iliahidi kujenga Chuo cha Utalii kuanzia Agosti, 2007. Tunataka maelezo kwa nini ujenzi huo ulichekewa kuanza?

(7) Kambi ya Upinzani inataka Serikali itoe majibu, ni hatua zipi zimechukuliwa kwa wahusika au kurejesha magogo yaliyokamatwa yakisafirishwa kinyume na sheria?

(8) Kambi ya Upinzani inataka kujua hatma ya viwanda vya mbao vilivyokuwa chini ya *TWICO* baada ya kubinafsishwa.

(9) Serikali inasemaje juu ya uvunaji wa magadi *(soda ash)* kutoka ziwa Natron?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, nawashukuruni wote kwa kunisikiliza. Kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kama kawaida yetu tunaanza na wale ambao hawajapata nafasi kabisa, ambao wako wawili kwa hapa, waliochangia mara moja wako, wako 16. Waliochangia mara mbili ni mmoja. Lakini nafasi ipo kwa sababu hii Wizara ina siku mbili. Sasa kuna wengine wanaogopa kwamba wakichangia hapo wanaweza kukosa mahali pengine na huko unaweza kukuta wakawa wengi ukakosa na huko. Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Philemon Ndesamburo atafuatiwa na Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro na Mheshimiwa James Daud Lembeli. Nafikiri hao ndiyo watatosha asubuhi hii.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia katika hoja ya Utalii katika siku ya leo. Kwanza ni-*declare interest*, mimi ni mmoja katika wadau wa utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Serikali ina mkakati wa kutaka kukuza utalii. Ni kweli ni jambo zuri lakini katika kukuza utalii tunataka Watanzania wote wafaidi utalii. Isiwe ni utalii utakaofaidisha wachache au wanaotoka nje. Haya manufaa, hii baraka tuliyopewa na Mungu iwafaidishe Watanzania wote. Ninasema hilo kwa sababu tumekuwa na fikira potofu. Tunafikiria katika utalii mwekezaji lazima atoke nje. Tunafikiria mtalii lazima akae katika hoteli ya *Five Star*. Kwa hiyo, lazima tulete

wawekezaji watoke nje, wajenge mahoteli makubwa ili watalii waje na wahakikishieni hiyo ni fikra potofu. *(Makofi)*

Watalii hawataki kukaa katika *Five Star Hotel,* watalii wanahitaji hoteli za kawaida. Wanaokaa *Five Star Hotel* ni wafanyabiashara na wageni wa Serikali. Sisi tunataka kuondoa umaskini, tunataka watu wote wa-*participate* katika utalii. Huku nyuma niliwahi kuzungumza hapa Bungeni nikatoa mfano wa *Mozambique*, nikatoa mfano wa zile nchi zilizo katika *Madeteranean Sea* zinazozunguka ambazo zinakuwa na watalii wengi. Wanaofaidi utalii na pesa za utalii ni wenyeji wa sehemu ile yenye vile vivutio. Tunapozungumzia utalii wa baharini ambao tunataka wafaidi ni wakazi wa Pwani. Ni wakazi wenyeji wanaokaa kule! Tunapozungumzia Serengeti tunataka Wamasai wanaokaa Serengeti na wale wanaokaa kule ndio wafaidi pesa za utalii. *(Makofi)*

Watafaidije pesa za utalii, mahoteli ya sehemu zile yaendeshwe na wenyeji wa sehemu zile. Wawezeshwe kwa kupitia Halmashauri zao. Halmashauri zao ziwe ndizo zinazojenga mahoteli ya watalii. Wenyeji wafundishwe namna ya kufua nguo, namna ya kuvaa, namna ya kupika, namna ya kuwatembeza watalii kule porini. Siyo watu watoke nje waje wakafaidi matunda ya utalii katika sehemu zile. Kama mtasema Halmashauri zitakuwa hazina pesa za kujenga hoteli, mimi ninakataa kwa sababu Serikali yetu ina pesa nyingi. Maana yake hata nyingine zinaibiwa hatujui.

*Local Government*, Halmashauri zinaweza kuwa na kitengo maalum ambacho kitakuwa kinafanya kazi ya utalii ili kiweze kuwezesha wenyeji wa eneo lile, siyo mtu wa Dar es Salaam anafaidi samaki wa baharini. Aende tena mpaka Serengeti aende akafaidi utalii wa kule Serengeti, aende akafaidi utalii wa kule Serengeti. Kwa kweli mimi hilo naona siyo utalii mzuri ambao utasaidia Watanzania wote. Kama tunataka kuondoa umaskini, utalii usambae kwa wenyeji na wenyeji wawe ndiyo wanaoendesha utalii na mahoteli ya sehemu zile ambazo zina vivutio vya utalii. Siamini kabisa ulete watu wa nje.

Mheshimiwa Lazaro alikuwa anachangia hapa, akasema tunauza nchi yetu kirejareja. Unapompa Mzungu miaka 99, ule ni mkataba. Miaka 99 anakuwa na ardhi na anajenga hoteli. Huwezi kumwondoa pale. Ile ardhi, ardhi ni mali na hakuna tajiri yeyote duniani anaweza kuwa tajiri bila kupitia kwenye ardhi. Kwa hiyo, ardhi Halmashauri ndiyo ziwe na ardhi. Haya matatizo ya kusema Guruneti na nini, haya yangekwisha na pangekuwa hakuna matatizo. Zile hoteli zote zingekuwa ziko mikononi mwa Watanzania na ardhi yetu ingekuwa haina matatizo. Hilo ni moja nimesema.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, wageni wetu wanapokuja Tanzania, wale ndiyo lulu, ndiyo almasi wanaotuletea pesa. Ni lazima tuwe makini kwa kuwalinda na kuhakikisha usalama wao. Pametokea au pametokea mtindo au pamezuka mtindo *Northern Cicurt* ambao unaweza kuleta hatari. Tumekuwa tunazungumza hapa Bungeni juu ya kubadilisha *chases* za malori na kufanya mabasi na yamekuwa yanapinduka, watu wamekufa wengi na tumekemea na tumeweka mpaka siku ya mwisho ya kuzuia.

Kule Arusha na Moshi pametokea mtindo, *pick up* zinabadilishwa magari madogo ya kubeba abiria wa kitalii. *Chases* ikishachomwa moto, *chases* ya gari yoyote ikishachomwa moto ile gari siyo gari tena. Gari ya watu wanne inageuzwa inabeba watu 8 mpaka 10. Atakapokufa Mzungu mmoja na magari hayo hayapo popote duniani ni Tanzania kwa sababu sisi wanakuja kufanya *experiment* hapa. Hicho kiwanda kiko Moshi. Wanabadilisha magari, gari linatengenezwa Ulaya, ni *TOYOTA* linakuja kubadilisha *more than a hundred fifty percent.* Sijui linaitwa gari gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui hawa wanaowapa leseni ni watu gani! Sijui *Bureau of Standards* wapo wapi? Tutakuja kuuwa watu, tumekataa malori, sasa wamehamia kwenye *pick up.* Wamehamia kwenye hizi gari ndogo, mkonge linafanywa refu. Hebu niambie gari la watu wanne linafanywa linabeba mpaka watu 10 na mizigo yao. Mheshimiwa Waziri nadhani wakati atakapokuwa anajibu atakemea kitendo hicho na haya magari yaachwe kufanywa marefu ili watu wapate faida zaidi *at the cost* ya kuuwa watalii wetu, hata watu wa *insurance* naambiwa wanakataa kurudishiwa magari yale kama mtu akiumia.

Hata Kampuni ya *TOYOTA* imetaka kwenda Mahakamani kukemea na kukataza gari zao kugeuzwa na kufanya kitu kipya. Lakini Serikali inakaa kimywa, wakati watu wanachezea haya magari. Wakati watu wachache wenye uchu wa kutaka kupata pesa za ziada, wanageuza gari lililo sawa ambayo duniani kote ndivyo linavyotumika wanaleta gari la Kitanzania ambalo sijui litakuwa linaitwa jina gani. *Tanzania TOYOTA*, sijui litaitwa Tanzania nini! Mimi naona ni jambo la hatari, litakuja kuuwa watalii halafu tutakuja hapa.

Kama tumekemea malori, mabasi *chases* zisichomwe na zigeuzwe na sasa naomba ikemewe vile vile hii tabia ya kurefusha magari ili ibebe abiria wengi na hasara nyingine ambayo tunapata katika hili, badala ya magari mawili kwenda ili Tanzania ifaidike kwa kupata pesa zaidi inakwenda gari hii moja. Kwa hiyo, hilo nadhani nimekwishalisema na Serikali imesikia na nadhani huyo anayefanya mambo haya, aache tufuate magari kwa kufuata yalivyoundwa huko yalikotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mlima wa Kilimanjaro ni mmoja katika vyanzo vinavyoingiza pesa nyingi za utalii kuliko chombo kingine chochote. Nadiriki kusema pato la Taifa mchango wa mlima wa Kilimanjaro ni zaidi ya madini yote Tanzania ambayo tunayapigia kelele hapa Bungeni. Mchango wa Taifa wa Mlima huu mmoja wa Kilimanjaro unazidi madini Tanzania yetu. Kwa sababu kule madini kuna wizi mwingi, wanatudanganya. Kwa hiyo, nadhani na ninaomba tuupe kipaumbele Mlima wa Kilimanjaro.

Theluji ya Mlima wa Kilimanjaro inayeyuka. Tunaambiwa na wataalam mlima unayeyuka kwa sababu ya *global warming,* kwa sababu ya hewa ya joto inayotoka Bahari ya Hindi ina-*blow* kule juu na inatoka vile vile kwa sababu ya uoto wa ile sehemu inayozunguka ule mlima umekuwa ni jangwa na inatoka, vile vile kwa sababu mvua zimepungua katika Mlima wa Kilimanjaro.

Tulikuwa na mkakati mzuri sana wakati wa Ihefu wakati tulipata matatizo ya umeme. Kweli Serikali ikafanya bidii zote na sasa Mto Ruaha unajaa maji. Ile sehemu ya Ihefu sasa ina uoto mzuri, kunapendeza, hakuna tena matatizo. Ni mkakati maalum uliofanywa na Serikali. Mimi ningeomba Serikali kwa umuhimu wa huu mlima, ifanye mkakati wa kufanya uoto unaozunguka ule mlima urudie kama ulivyokuwa zamani. *(Makofi)*

Ukirudia nina hakika patakuwepo angalau na kasehemu kadogo ka ule mlima, barafu itaendelea kuwepo na watalii watazidi kupenda kupanda ule mlima. Mimi hata siku moja sijawahi kusimama hapa Bungeni kulalamika barabara mbaya, hatuna maji, siwezi kwa sababu kwa kweli kule kwetu kumeendelea. *(Makofi)*

Wenzangu wanalalamika, ni kweli sehemu nyingine ziko nyuma. Lakini pesa za kuendeleza kule kwingine zinatoka wapi? Kilimanjaro. Kwa hiyo, tusiwe tunasema tusiendeleze Kilimanjaro ati kumekwishaendelea. Tusipoendeleza Kilimanjaro na mapato ya kuendeleza hii sehemu nyingine zitakuwa hazipo. *(Makofi)*

Nasema hivyo kwa sababu tunakisahau kiwanja cha ndege cha Moshi. Moshi ndiyo mji wa Mlima Kilimanjaro. Wageni wengi wangekuwa wanaruka kuja kupanda Mlima Kilimanjaro kushukia Moshi kama kile kiwanja kingekuwa kinafanya kazi. Niliwahi kuahidiwa hapa pesa zimetengwa kwa ajili ya kujenga ile *run way*. Lakini hakuna chochote kilichofanywa zaidi ya miaka mitatu sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Moshi tumejaribu tangu nimekuwa Mbunge mwaka 2000, unakuwa namba *one* Tanzania kwa usafi. Kwa sababu nashirikiana na Halmashauri ya Moshi kuufanya mji wa Moshi uwe unavutia kwa ajili ya watalii, waje wengi, tupate pesa na zisambae Tanzania nzima, siyo kwa ajili ya Moshi. Nimesema pato la Mlima wa Kilimanjaro ni zaidi ya dhahabu yote inayochimbwa Tanzania. Sasa kwa nini tunaudharau ule mlima? Kwa nini hatuupi kipaumbele kinachotakiwa? Kwa nini hatutaki uendelee tuuendeleze uoto?

Mheshimiwa Naibu Spika, wale Wachaga wanakaa chini ya Mlima. Zamani palikuwa na miti, juu pana migomba, katikati kuna kahawa chini. Jua halikuwa halifiki kwenye ardhi. Ardhi ile sasa imekuwa tupu, kwa kweli ni hatari kubwa. Narudia hili kwa sababu ni hatari kubwa. Kwa sababu mapato ya ule mlima, kama barafu ile ikipotea kabisa, nina hakika itateremka. Sio lazima na sidhani kama itapotea, lakini kuna *balance* ya kuweza kusema labda itapotea na sisi tunataka watalii wazidi Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la mwisho, pesa zinazotolewa na Shirika la *TANAPA* kwa ujirani mwema, sio sawa. Zile pesa zingekuwa zinapewa kwa Halmashauri zinazozunguka, kwa sababu hatuelewi kigezo wanachotumia kugawa zile pesa za ujirani mwema, vile vile hawa *TANAPA* hawajui matatizo yaliyo katika zile Halmashauri. Halmashauri ndiyo wanajua matatizo na *priority* zao ni nini? Kwa hiyo, fungu lile la ujirani mwema lingeongezwa na kupewa Halmashauri ambao ndiyo wanajua ni matatizo gani yaliyo katika Halmashauri zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo, hilo tungeliomba sana, pesa za ujirani mwema zisiwe za kuwapa watu kwa majina yao. Zipewe Halmashauri ili ziende katika mkondo unaofaa ili ziweze kufaidika kwa Watanzania wote na wote wale wanaohusika katika utalii na katika kuleta uimara ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kupigiwa kengele ya pili. Naomba kuwasilisha hoja yangu. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mzee Ndesamburo. Sasa nitamwita Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro na Mheshimiwa James Lembeli ajiandae.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii. Lakini kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia, naomba uniruhusu pia mwanzoni nitoe neno la shukrani. Kwanza, ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya maisha, lakini pia kwa kunijalia afya njema na kuweza kuwa hapa leo. *(Makofi)*

Pili, ningependa kushukuru chama changu Chama cha CCM kwa kunipa heshima kubwa na kuniteua kuwa mgombea nafasi ya Ubunge katika uchaguzi mdogo kwenye Jimbo la Kiteto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kuwashukuru wapiga kura wangu wote wa Kiteto kwa imani kubwa walioionyesha kwangu waliponichagua tarehe 24 Februari, 2008. Mwisho, naomba niwashukuru familia yangu, marafiki na Wabunge wa CCM kwa kuniunga mkono kwa hali na mali katika mchakato huo mzima wa uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nirudi katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Kwanza ningependa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Waandamizi wao katika Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kazi nzuri sana walioifanya kwa sababu hotuba iliyotolewa hapa kwa kweli ni nzuri. Inatoa picha nzuri juu ya mwelekeo wa Wizara. Lakini pia yale yaliyoweza kufanyika katika jitihada zote za Wizara kuboresha shughuli zake na pia wamebainisha aina ya changamoto zinazowakabili kama Wizara na matarajio walionayo pia katika kipindi kinachokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kweli ni Wizara muhimu sana. Ni muhimu kwa sababu imeunganisha rasilimali zote tunazohitaji moja kwa maendeleo yetu kama nchi. Lakini pia kwa maendeleo ya watu, mmoja mmoja, kaya, pamoja na jamii hasa zile zinazozunguka maeneo hayo ya wanyama kama ni hifadhi za Taifa, hifadhi ya Ngorongoro na maeneo mengine ambayo yamebainishwa kuwa ni ya muhimu. *(Makofi)*

Lakini pamoja na umuhimu huu, kawaida imekuwa kwamba watu kutoka nje wananufaika zaidi na rasilimali hizi kuliko jinsi wenyeji na wenyeji wanavyonufaika kutokana na rasilimali hizi. Tukichukua mifano, mfano wa wanyamapori, wanyamapori kwa kweli ni rasilimali ya muhimu. Lakini bado tunapashwa kujitahidi kama Wizara kuhakikisha kwamba rasilimali hii itatunufaisha sisi wenyeji kwanza na sisi kama nchi kwanza kabla ya kuwanufaisha wageni. Lakini picha inayojitokeza ni kwamba ukitazama wanyamapori katika sura yoyote kama ni kwenye hifadhi ya Taifa, kwenye vitalu hivyo vya uwindaji, picha unayoipata ni kwamba kumekuwepo na upendeleo, watu kutoka nje kwa jina la uwekezaji wamekuwa wananufaika zaidi. Ni vizuri kwanza kutazama kwamba wanyama hawa tutawatumiaje zaidi kwa manufaa yetu na kwa maendeleo yetu kama nchi. *(Makofi)*

Nadhani kuna njia nyingi, tukianza kuwa wabunifu na kutazama moja kwamba kwanza wanyama hawa ili waendelee kuwepo tunahitaji kuchangia kiasi gani na kwa namna gani katika hifadhi yao. Ukichora ramani ya wanyamapori kama rasilimali, Tanzania nzima unaweza ukakuta wanyama hawa wamekusanyika katika maeneo fulani fulani zaidi, Kaskazini mwa nchi, lakini pia katika ukanda fulani Kusini. Ukitazama maeneo haya zaidi utakuta kwamba mara nyingi wanyama hawa wamehifadhiwa kwa kweli na mifugo na wamehifadhiwa na wafugaji. Kwa sababu hiyo, kuna haja ya Wizara kuwaona wafugaji na mifugo kama kweli ni wadau wa muhimu sana katika kuendelea kuhifadhi rasimali hii ambayo ni ya muhimu sana. *(Makofi)*

Ni wazi kwamba kuna matatizo yanayotokana na wanyama wale wa porini na mifugo kuishi pamoja kwa sababu kuna kuambukizana magonjwa. Kuna matatizo mengine ya wanyama wakali hasa simba kuwashambulia mifugo. Ingekuwa ni vizuri sana Wizara kama Wizara kuwa na mkakati maalum mmoja wa kushughulikia magonjwa hasa yale yanayotokana na wanyama pori halafu mwishoni wanaambukiza mifugo na mara nyingine pia kuambukiza binadamu. Wizara ikichangia katika uboreshaji wa afya ya mifugo na afya ya wanyamapori kwa kweli rasilimali hii itaendelea kuwa ya manufaa kwetu na ya manufaa kwa Taifa zima kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikija kwa namna nyingine ambazo rasilimali nyingine hasa ya wanyamapori inavyovunwa. Kumekuwepo na vitalu hivi vya wawindaji, ni njia nzuri, lakini kwa kuwa kumekuwepo na mkakati wa kujaribu ku-*transform* vitalu hivyo viwe ni *WMAs* ni vizuri kwa sasa jitihada zifanyike ili kuhakikisha kwamba wenyeji wanaoishi kwenye maeneo hayo watakuwa ni wahifadhi wazuri wa wale wanyama, lakini pia ni watu watakaonufaika kutokana na matunda na faida nyinginezo zinazotokana na hawa wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, nadhani kuna haja ya kuanza kufikiria kama mwanzo mzuri badala tu ya vitalu hivyo kugawanywa katika ngazi ya Wizara, hasa Idara ya Wanyamapori. Kwanini utaratibu usiwekwe ili maombi yaanze katika ngazi ya kijiji, ngazi ya Halmashauri ya Wilaya na mwishoni Idara ya Wanyamapori, ikapewa dhamana tu zaidi ya kuidhinisha maombi yale ambayo yamekuwa yamepitishwa na watu katika ngazi husika? Njia hii ingewapa watu wawe na *sense* ya *ownership* kwa wale wanyama, kwamba hawa wanyama ni wetu, tunanufaika nao na wale wanaokuja kuvuna wanakuja

lakini wanavuna kwa idhini yetu. Ninaomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuchukua hilo wazo kwa sababu hili litakuwa ni wazo la kuwashirikisha kikamilifu wale watu wanaoishi katika maeneo haya waweze kujiona kwamba rasilimali hii ni yao na ni sharti wawe na nafasi ya pekee katika kutunza rasilimali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija katika eneo lingine hili la utalii, ni wazi utalii unapaswa bado kuboreshwa katika nchi yetu. Kuwa na rasilimali haitoshi, huduma zinazosaidia katika kuboresha utalii hasa upande wa hoteli, usafiri na huduma nyinginezo ni sharti ziende sambamba na uboreshaji wa utalii kama sekta. Lakini Waziri, katika hotuba yake kwenye ukurasa ule wa 51 amegusia *cultural tourism.*

Ni kweli kuna makundi ya watu hasa wenyeji, wanojaribu nao kuona jinsi ya kunufaika na sekta hii ya utalii na wameanza kujaribu kuwa na *program* hizo za *cultural tourism.* Lakini nyingi bado ni hafifu, zinahitaji kupewa ushauri, zinahitaji kupewa maelekezo na ninadhani ni wakati muafaka sasa kwa Wizara kuwa na dawati maalum la mtaalamu anayeweza kushauri na kuelekeza jinsi ya kuboresha hiyo *cultural tourism.* Kwa sababu kwa njia hii, nadhani sisi kama nchi tungeweza kunufaika vizuri zaidi kuliko tunavyonufaika sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchangia hapo, ninaomba pia niongelee suala zima lililo ongelewa la *lake Natron.* Ni kweli ni eneo zuri sana na kama tulivyosikia ni eneo la pekee ambalo ndege aina ya *Flamingo*, wale wadogo wanazaliana mle. Kwa hiyo, ni eneo ambalo lina maana sana *East africa* na katika Afrika nzima, lakini pia hata ulimwenguni ni eneo ambalo ni muhimu sana. Kwa kipindi sasa kumekuwepo na majadiliano na mapendekezo kwamba eneo hilo lifanye kuwa ni la *Ramsa Site.*

Ningependa tu kusema kwamba hili ni wazo zuri, lakini Wizara itakapokuwa inajarimu kutekeleza pendekezo hilo, wakazanie dhana nzima ya *Ramsa* inayosisitiza kwenye matumizi ya busara kwa rasilimali husika. Sio kufikiria kuwaondoa watu kwa sababu dhana ya *Ramsa site* ni *wise use* sio kutotumia eneo hilo kabisa. Kwa sababu wenyeji wa eneo hilo wana hofu kwamba eneo linapoonekana kwamba ni muhimu sana, kidogo kidogo mchakato utaanza wa kuwasukuma wao pembeni na kujaribu kufanya eneo hilo kuwa kama maeneo mengine hasa katika zile hifadhi za Taifa ambazo hakuna shughuli za kibinadamu zinazoruhusiwa kufanyika mle.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri *concept* kama ni ya *Ramsa* izingatiwe lakini pia kuwepo na uadilifu katika kuitekeleza *concept* hiyo bila kuchagua chagua. Kwa sababu kwa njia hiyo mkazo ukiwa ni matumizi mazuri, matumizi ya busara, wenyeji watakuwa na moyo na watashiriki kikamilifu katika kuchangia katika ufanisi wa shughuli hiyo nzima. Kwa hiyo, ninaomba Wizara ijaribu kuhahakikisha kwamba kama ni *Ramsa Site,* watekeleze kwa sura hiyo, sio kwa namna ya baadaye kuanza kuwaondoa watu ambao wamekuwa wakiishi na maisha yao yamekuwa yakitegemeana na rasilimali hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba pia kupendekeza kwa Wizara kama kuna uwezekano: Moja, kuhakikisha kwamba ile asilimia 25 ya mapato kwamba kiasi

hicho kwa kweli kinakwenda kwenye Halmashauri husika, kwa sababu kuna Halmashauri nyingi hazipati kitu. Lakini hata kama kuna uwezekano, kwa nini Wizara isifikirie kuongeza kiasi hicho na kufikisha angalau asilimia 40 ya mapato yote ili Halmashauri na vijiji husika waweze pia kuwa na kitu cha kugawa? Labda Halmashauri ichukuwe asilimia15 na zile asiimia 25 ziende kwa ajili ya maendeleo ya vijiji husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nikushukuru tena na ninaomba niseme kwamba ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi.*

**NAIBU SPIKA:** Mtakubaliana na mimi kwamba sio kama ni ya kwanza, ni kama ya zamani kabisa hotuba hii. Kwa hiyo, amechangia vizuri sana, nashukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa James Lembeli, nadhani ndiye atakayemalizia kwamchana huu.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa fursa hii. Mchango wangu siku ya leo utajikita katika maeneo mawili, nayo ni sekta ya utalii na sekta ya uhifadhi. Napenda niseme tangu mwanzo kwamba sitaunga mkono hoja hii kama yale ambayo nitayauliza hayatapewa majibu yanayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hizi mbili, ya utalii na ya uhifadhi ni sekta muhimu sana kwa uchumi wa nchi hii, lakini ni sekta ambazo zimeendelea kuiweka Tanzania katika ramani ya dunia, jambo ambalo ni sifa sio tu kwa nchi, lakini kwa Watanzania wote. Leo hii ukisafiri sehemu mbalimbali za dunia ukisema unatoka Tanzania, utasikia watu wanazungumza wanajibu kwa kusema unatoka Kilimanjaro, Serengeti, Ngorongoro na wakati mwingine *Selous.* Sasa sekta hizi mbili ni utambulisho kwa Mtanzania wa hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na sekta ya uhifadhi. Tanzania inasifika duniani kwa sera yake nzuri ya uhifadhi, Tanzania inasifika duniani kwa kuwa na pori la akiba kubwa kuliko yote duniani kama sio la pili, lakini sifa ya Tanzania ni kuwa na hifadhi kubwa kuliko zote Barani Afrika, hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Tanzania hiyo hiyo inasifika kwa kuwa Makao ya Serengeti, Kilimanjaro, Ngorongoro na kadhalika. Tanzania pia inasifika kwa sera yake nzuri ya kutenga asilimia 25 ya eneo lake kwa kazi za uhifadhi. Hili ni jambo zuri kwa ustawi, sio tu wa binadamu lakini kwa ustawi wa dunia yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti na nchi nyingine, shughuli hizi za uhifadhi hapa nchini kwetu zinafanywa na Watanzania wenyewe. Ukienda pale *TANAPA* sifa zote ambazo *TANAPA* inapata hapa nchini na duniani, *TANAPA* inaongozwa na Watanzania, Ngorongoro inaongozwa na Watanzania, vivyo hivyo *Selous* inaongozwa na Watanzania. Pale Mlima Kilimanjaro ni watanzania. Ni jambo la kujivunia na naipongeza Serikali kwa kuwasomesha Watanzania hawa ambao kwa kweli wanafanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi huu wa mafanikio unatokana na hotuba ya Baba wa Taifa, aliyoitoa mwaka 1961 pale Arusha, mwezi Septemba, hata kabla nchi yetu haijapata uhuru. Napenda ninukuu sehemu ndogo ya hotuba hiyo ya Baba wa Taifa: *"The survival of our wildlife is a matter of grate concern to all of us in Africa. These wild creatures amid places they inhabit are not only important as a source of wonder and inspiration but are an integral part of our natural resources and our future livelihood and wellbeing. In accepting the trusteeship of our wildlife, we solemly declare that we will do everything in our power to make sure that our children's grand children will be able to enjoy this rich and precious inheritance."* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachelea kusema kwamba msingi huu sasa umeanza kuingiliwa na siasa za hapa na pale. Uhifadhi ukishaingiliwa na siasa, baada ya muda mfupi hatutakuwa tena na Serengeti, hatutakuwa tena na Kilimanjaro, hatutakuwa tena na *Selous.* Badala ya kuacha taaluma ya uhifadhi ifanye kazi zake, kila siku utasikia viongozi na hususan wa Serikali kuingilia maamuzi ya Taasisi hizi. Hii ni hatari!

Katika hotuba ya bajeti ya Waziri wa Wizara ya Fedha, aliyoitoa hapa Bungeni, ukurasa wa 25 naomba ninukuu:*"Kwa kuzingatia hili sheria ya fedha za umma sura ya 348, itafanyiwa marekebisho ili kumpa mamlaka Mlipaji Mkuu wa Serikali, kuzitaka asasi hizo kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali kulingana na bajeti ya taasisi hizo. Utaratibu wa kuchangia utaainishwa katika kanuni za fedha za umma."*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina hakika kwa mashirika na Taasisi nyingine, lakini kwa *TANAPA* na Ngorongoro, huu ndio mwisho wao. Serikali inataka kuyauwa haya mashirika. Mimi najua *TANAPA* haizalishi ziada, vivyo hivyo Ngorongoro. *TANAPA* inasimamia. Leo hii hifadhi za Taifa 15, zinazozalisha ni hifadhi tano tu, hizi nyingine ambazo baada ya Serikali kuziachia zikamalizwa, inakabidhi *TANAPA* bila kuwapa hata sumni wala kitendea kazi. Sasa inataka kuleta hoja, zile pesa ambazo ziko benki zimewekwa na Taasisi hizi, watu wa Hazina waende wakazichomoe. Hii sio haki! Naomba sana, sheria hii isiguse Taasisi hizi mbili. Hebu tujiulize, nani analipia uhifadhi wa nchi hii? Serikali Kuu? Ni utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa pesa zilizoko benki za *TANAPA* na Ngorongoro wameweka makusudi, endapo utalii utaporomoka waweze kutumia pesa hizi angalau kuendesha uhifadhi kwa takribani mwaka mmoja. Pesa hizi zikishachomolewa zikapelekwa Hazina, ukitokea moto pale mlima Kilimanjaro, kwa urasimu wa Hazina, mlima huo utakwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba suala hili Serikali ilizingatie na isifanyie mchezo. Tunajivuna kila siku Serengeti! Mheshimiwa Rais anakwenda anazungumza, kesho na keshokutwa hela hizi zikichotwa zikapelekwa Hazina. Hatutakuwa na Serengeti tena! Kama Serikali inafikiri kwamba ina utaratibu bora wa kutumia pesa, mbona inashindwa hata hii leo *Selous* kuiendesha? *Selous* inapata mapato hayo hayo, inapata pesa zake kutokana na utalii, lakini sehemu kubwa ya pesa inakwenda Serikalini. Kwanini wanashindwa kuiendesha *Selous* kikamilifu? Mimi nina wasiwasi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato ya Wizara hii na hususan mapato yanayotokana na wanyama na uwindaji. Kabla sijaendelea kuchangia, kusema yale ambayo nataka kusema nataka nisome yaliyomo katika Kitabu cha Mwongozo wa *CCM* 1981, ukurasa wa 103 kama kuna mtu anasema katika ibara ya 109:

*"Wakati wote ni muhimu kwa Chama na umma kuwa na hakika na anayekabidhiwa madaraka haya ya Serikali, maana yakiangukia mikononi mwa mpinga mapinduzi, madaraka hayo yanaweza kutumiwa dhidi ya maslahi ya umma wenyewe. Hivyo Chama kuongoza maana yake ni kuhakikisha kuwa pia madaraka muhimu ya Serikali na ya Mashirika ya Umma yanakabidhiwa watu ambao pamoja na uwezo wao wa Kitaalamu ni wenye msimamo wa kizalendo, waaminifu kwa Chama na kwa wakulima na wafanyakazi wa Tanzania."* Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu mwaka 2007 Bunge hili tulipitisha tozo mpya za uwindaji na leseni. Mheshimiwa Maghembe, alisimama hapa kwa majigambo na kila mmoja humu ndani alimshangilia, sio wa *CCM* sio *CUF*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, utasema, aliyekuwa Waziri na Cheo chake. Ukisema kama Maghembe, tena umeharibu.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunielekeza.

**NAIBU SPIKA:** Utaongezewa dakika yako.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Lakini kwa sababu ambazo mimi sizielewi, Serikali imekaa huko kimya kimya bila kurejesha hapa Bungeni, kuelezea hayo mabadiliko yametokea vipi? Badala ya shilingi bilioni 48, mwaka huu tunaletewa makusanyo ya shilingi bilioni 20, ni akina nani hao? Mimi nina taarifa kwamba kuna wafanyabiashara ambao waliishinikiza Serikali kupunguza tena hizo ada. Sasa hao viongozi ambao wanajichukulia madaraka ya kuteremsha bila kurejesha hapa Bungeni ni akina nani? Waliutoa wapi huo uwezo? Sheria ipi iliwaruhusu kufanya mambo haya? Haya ndio mambo ya kuruhusu rasilimali ya nchi hii inaporwa usiku na mchana. Nitaomba nipate ufafanuzi kulitokea kitu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme. Ukitazama bei ya wanyama wetu na hili, nina uhakika nalo, kama kuna mtu atataka kusema nithibitishe naweza kuthibitisha hata baada ya kikao hiki. Sisi tunawindisha nyumbu kwa dola 650, *South Africa* wanawindisha kwa dola 1,500; Zimbabwe dola 1,500, Botswana dola 1,500; nani kaweka hiki kiwango cha dola 650? Kuna mdudu mdogo hapa anaitwa *caracal*, *South Africa* anawindwa kwa dola 950, sisi dola 150. Pofu, yule mnyama mzuri, sisi tunawindisha kwa dola 1,500, *South Africa* 3,200 Zimbabwe 2,800, Botswana 2,750, ninazo.

Nyati tunawindisha sisi kwa dola 950 mpaka dola 1,400; Zimbabwe 3,000, Botswana 3,750. Pundamilia, sisi tunawindisha 1,200, Botswana wanawindisha 2,500,

Zimbabwe 1,800, *South Africa* 1,800. Tembo/ndovu, sisi tunawindisha kati ya dola 7,500 mpaka dola 20,000. Botswana dola 20,000, Zimbabwe dola 12,500 mpaka 14,500 data hizi ninazo. Sasa hawa waliokaa na kuzipunguza jamani, halafu Serikali hiyo hiyo inachangisha wananchi kule vijijini shule, zahanati, wakati pesa iko hapa, lakini wanaochukua ni wachache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyozungumza hivi wako hapa. Wamekuwa wakipitapita hawajaniona kwa sababu wanafahamu msimamo wangu, ni hatari kwa hii nchi. Lazima mafisadi wa aina hii wamulikwe na ndio maana nimesoma mwongozo wa *CCM. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongee kidogo kwenye utalii. Mapesa mengi sana ya nchi hii yanatumika bila kuzingatia utaalamu. Siasa inaingia hapo inashinikiza wataalamu kukubali mambo ambayo hayawezekani na ya kuliingizia Taifa hasara. Nitatoa mfano, mwaka jana tumetumia karibu dola 1,000,000 kutangaza Marekani kwa miezi mitatu/minne. *The idea was good, but it was wrong time.* Kwanza, wametangaza kwenye *electronic media*, baada ya miezi mitatu hakuna mtu atakayesikiliza tena habari ya Tanzania. Lakini katika kipindi kile *the dollar was weak.* Katika mambo ya *travel, when your currency is weak it becomes very expensive to travel.* Kwa hiyo, zile pesa zilidumbukizwa tu huko, sidhani kama watu wa *TTB* walichangia katika hili. Zimepelekwa dola 450,000 kwenye Balozi zetu, mimi hili kila siku nalipinga.

Kule ubalozini wale watu hawawezi kuifanya hii kazi, kwanza kila ubalozi una upungufu wa wafanyakazi. Sasa nani anayeifanya hii kazi? Badala ya ku-*attend road shows* na kadhalika wanapeleka kwa watu shilingi milioni karibu 500. Nina hakika viongozi hawaitendei haki nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa inayopatikana kidogo inayopatikana itumike vizuri na ninaomba niishukuru Serikali kwa kuendelea kupandisha bajeti ya *TTB*, hawa watu wanafanya kazi kweli kweli. Lakini wapo baadhi ya viongozi hawawapendi na wanasema huyo hajui kitu kwasababu hawakubaliani na matakwa yao. *TTB* wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, hawana vitendea kazi, bajeti ndogo, lakini bado wameendelea kuitangaza nchi hii vizuri sehemu mbalimbali za dunia. Mimi ni shahidi kwasababu nilishiriki nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema hapo mwanzo kwamba sitaunga mkono hoja hii kama sitapata ufafanuzi wa kina kwanini Bunge litumie muda mrefu kujadili na kupitisha mambo hapa halafu watu wachache wanakwenda wanakaa huko wanabadilisha uamuzi wa Bunge bila kuleta hapa ndani ya Bunge? Nisipopata maelezo hayo Mheshimiwa, utanisamehe, sitaunga mkono hoja. Lakini pili, nataka kupata ufafanuzi juu ya hizi pesa ambazo zimepelekwa kwenye Balozi. Zikafanye nini? Zimefanya nini? Vinginevyo, hizo pesa zimepelekwa mikononi na vinywani mwa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa kengele ya pili inigongee, nakushukuru kwa kuniongezea muda wangu uliopotea. Nitaunga mkono hoja baada ya kupata ufafanuzi huo. Ahsante sana. *(Makofi).*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliobakia hauwezi kumtosha mtu mwingine kujadili. Kwa hiyo, tutakaporudi mchana Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, atakuwa msemaji wa kwanza, atafuatiwa na Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Lucy Owenya ajiandae, Mheshimiwa Dunstan Mkapa pia ajiandae na wengine.

Waheshimiwa wabunge, baada ya kusema hayo, najua Mheshimiwa Lembeli ni mtaalamu wa eneo hili. Kwa hiyo, msimchukulie kama wengine wengine, ni mtaalamu wa eneo hili. Ni kweli, kama waliahidi, Serikali imebadilisha utaratibu wake, ni lazima itoe maelezo kwa nini ilibadili? Hiyo ni utaratibu kabisa. Baada ya kusema hivyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni. *(Makofi)*

*(Saa 06.56 mchana Bunge, lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*
*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla ya kusitisha shughuli za Bunge mchana, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Estherina J. Kilasi, Mheshimiwa Lucy F. Owenya na Mheshimiwa Dunstan Mkapa wataanza kuchangia.

Sasa namwita Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, karibu!

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuwa wa kwanza kwa jioni hii ya leo kuongea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo matatu tu ya kuongea ingawaje yana vipengele vingi ndani yake. La kwanza, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu za kuunga mkono ni hizi zifuatazo: Moja, ni kwamba naifahamu Wizara hii inavyofanya kazi nzuri kwa majukumu mazito kabisa waliyokabidhiwa na ninawatakia kila la kheri waendelee kuifanya kazi hii nzito sana. Sehemu kubwa ya Wizara hii kazi zinafanyika porini, iwe ni ya kulinda wanyama au kufanya utafiti, iwe ni ya kulinda misitu na mengine mengi. Lakini hata utalii nao wana jukumu la kuingia kwenye maeneo hayo hayo ili wayafahamu vizuri na ili hatimaye waweze kuitangaza Tanzania kiutalii ambayo sehemu kubwa ni wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni sahihi kabisa kuiunga mkono na ninaomba Waheshimiwa Wabunge wengine kuiunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa uongozi wa Mheshimiwa Waziri huyu tuliyenaye sina shaka kwamba ataiongoza vizuri Wizara hii ambayo ina wataalamu wengi wenye uwezo wa kuyafanya mambo ambayo yanatarajiwa ili sekta kubwa ya Maliasili na Utalii iweze kuchangia katika maendeleo ya nchi hii. Mheshimiwa Waziri huyu nimefanya naye kazi, kwa hiyo, ninaposema anaweza ni kwa sababu namfahamu na kwamba alikuwa ni kiongozi wangu, ni Mama mmoja ambaye sina shaka naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, naunga mkono hoja kwa sababu pamoja na changamoto nyingi zilizopo kwenye Wizara hii, kwanza, wao wanazifahamu tumekuwa tukizisema humu Bungeni na tutaendelea kuzisema hata safari hii na zinasemwa hata na wananchi. Lakini nafahamu ni azma ya Serikali kuhakikisha kuwa changamoto hizo zinashughulikiwa na ninafahamu Wizara hii kuanzia ngazi ya Mawaziri mpaka Watendaji wote wanalielewa hilo, wanalizingatia hilo na kwa nyakati mbalimbali wanachukua hatua na ninafahamu hata harakati nyingine ambazo wanazishughulikia ili kuhakikisha kuwa changamoto ambazo tumekuwa tukizisema zinashughulikiwa.

Moja ya changamoto hiyo ni hili suala la uwindaji wa kitalii. Ni wazi kuwa uwindaji wetu wa kitalii bado uko chini katika maana ya mapato na namna jinsi unavyoendeshwa kwa ujumla na ndiyo maana inakuwa wakati mwingine ni mjadala mkali kabisa ambao ni sahihi kabisa kwenye eneo hili. Wizara wanalifahamu. Lakini nafahamu kuwa wanachukua hatua za kuhakikisha kuwa haya yanayosemwa siyo ya mzaha na kwa hiyo, wanayashughulikia. Haiwezekani sisi tukawa na dhahabu hii juu ya ardhi ambayo itadumu kwa muda mwingi tu, lakini tukaiangalia hivi hivi tu bila kuleta faida inayotakiwa. Kwa hiyo, ni lazima tulisemee suala la uwindaji wa kitalii kwa sababu tunafahamu bado hatujafika kwenye kiwango ambacho tunasema sasa tumefika ili kusudi tuweze kufaidika ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ni suala la maeneo ya uhifadhi unaosimamiwa na wananchi kwa Kiingereza ni *Wildlife Management Areas* au kwa kifupi ni *WMAs*. Tunazo sasa *WMAs* takribani 16 hivi. WMAs hizi kwa mtazamo wangu naziona kuwa ni sehemu za kiuchumi yaani Economic *Centres* ambazo Serikali kwa kutekeleza Sera za Maendeleo ikaamua maeneo haya yasimamiwe na wananchi na inufaishe wananchi. Sasa mimi nafahamu jinsi hizi *WMAs* zilivyotayarishwa na Sheria inasema nini hii Sheria iliyopo sasa hivi na Sheria inayotarajiwa kuja.

Moja ya lengo kubwa ni kuhakikisha kuwa wananchi wanafaidika na wanyamapori waliopo kwenye maeneo hayo ambayo watayasimamia, kwa hiyo, inatarajiwa kuwa wao ndiyo wawe wasimamizi wa kuamua kwamba tunalitumia namna gani hili eneo ili kusudi haya mapato tuweze sisi wenyewe kufaidika nayo na kwa sababu hiyo baada ya kipato kupatikana Serikali itakuwa na uwezo wa kutoza kodi na kwa hiyo, itafungua njia nyingine ya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu changamoto iliyopo kwa sasa hivi mimi naiita changamoto kwa sababu ni muhimu ishughulikiwe bado kuna ugumu wa Watendaji hasa Idara ya Wanyamapori wa kuachia hiyo, maana Sheria ya Wanyamapori inampa Mamlaka Mkurugenzi wa Wanyamapori kusimamia mnyamapori popote alipo. Kwa hiyo, bado kuna tatizo kidogo hapa la ugumu la kuachia hayo madaraka ili kusudi wananchi wajiamulie nani anakuja, kwa mfano kuwekeza kwenye eneo letu, tunawinda wanyama wapi? Tunawinda wanyama wangapi? Mimi najua hili ni suala tu wakati mwingine ni la mtazamo tu. Naiomba Serikali ihakikishe kuwa mtazamo huu tunaubadilisha ili kusudi tuwaachie wananchi wasimamie na waamue cha kufanyia haya maeneo kwa faida yao na kwa faida ya uhifadhi, tukumbuke kuwa uhifadhi ni gharama

na kwa hiyo na wao ni lazima wazibebe hizo gharama lakini gharama hizo wazibebe kupitia wanyama hao wanaowasimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami naungana na Mheshimiwa James Daud Lembeli alipozungumzia suala la gharama ya uhifadhi. Uhifadhi ni gharama sana. Haya Mashirika na Taasisi zilizopewa dhamana ya kusimamia wanyamapori hawa, yaani kuwalinda, yanaingia gharama kubwa sana kuhakikisha kuwa hawa wanyama tunaowaona kwenye maeneo mengi haya tunayoyaona yanakuwa hivyo na wanyama wanabaki.

Sisi wakati nilipokuwa mtafiti tulishirikiana na watafiti wengine, tulijiuliza swali moja kwamba nani analipia uhifadhi? Je, hela inayotoka kwenye Pamba ndiyo iende kwenye uhifadhi? Hela inayotoka kwenye Dengu ndiyo iende kwenye uhifadhi? Hela inayotoka kwenye Madini ndiyo iende kwenye uhifadhi? Sisi tulijibu swali hilo na baadaye kitabu kitatoka kinachoelezea suala zima hilo. Tukasema ni lazima wanyama hawa wajilipie wenyewe uwepo wao na maeneo yao, katika maana kwamba tuyatumie haya maeneo kupata pesa, pesa ambazo ni sharti zirudi huko ili kusudi maeneo haya yabaki kuwepo na kwa kufanya hivyo hapo tutakuwa sasa tuna uhakika wa kuendelea kuwa na wanayamapori kama hivi tunavyowaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunapoona haya mashirika na Taasisi zinapata pesa, sio vizuri kuharakisha kusema tuzichukue hizi pesa, ni vizuri tujue hizi pesa ni za kuhakikisha kuwa ulinzi wa wanyamapori unakuwa unaendeshwa kwa pesa inayozalishwa kutoka kwenye maeneo hayo na bahati nzuri mimi huwa nafurahi kuona kuwa wanyamapori wetu wanalindwa chini ya Mamlaka ambazo zinaendeshwa na Watanzania kwa asilimia mia moja. Ni mfano mzuri sana.

Nenda *TANAPA* na hata Ngorongoro, nenda Idara ya Wanyamapori inayosimamia maeneo mengine, ni Watanzania kwa asilimia mia moja. Nawapongeza sana katika hilo na ninaiomba Serikali iendelee kuliona hilo na kuhakikisha kuwa uhifadhi huu tunauacha mikononi mwa taasisi zetu na ukiendeshwa na Watanzania wenzetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama ya uhifadhi ni pamoja na gharama za utafiti. Nimekuwa nikifuatilia kwa muda mrefu pesa inayotolewa kwa mfano kwenye Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania yaani *TAWIRI*, bado mimi sijaridhika na kiwango hicho cha pesa, ni kidogo mno na Mheshimiwa Waziri anafahamu ni kidogo sana, lakini kazi wanayofanya ni kubwa sana.

Naiomba Serikali iliangalie hili ili kusudi *TAWIRI* waweze kupata pesa za kutosha ili waweze kuendesha utafiti ili kusudi Watanzania wengi waweze kushiriki kwa sababu kwa taarifa tu ni kuwa watafiti wa Wanyamapori hapa nchini, wengi ni wageni, sababu ni hiyo hiyo kwamba tunatoa pesa kidogo kwa ajili ya Watanzania kushiriki kwenye utafiti na kwa taarifa tu ni kuwa watafiti wanaokuja nchini kutoka nchi za nje zaidi ya nusu wanafanya utafiti wa wanyamapori. We jiulize kwenye sekta ya afya, misitu, maji na mengine yote, ukiangalia watafiti wa wanyamapori ni zaidi ya nusu. Sasa ni vizuri

*TAWIRI* ikapewa pesa za kutosha ili kusudi iweze kuhakikisha kuwa inashirikisha na inaajiri Watanzania wengi ili waweze kushiriki katika utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ni utalii. Utalii hauwezi ukaendelea kwa Bodi ya Utalii Tanzania kupewa hela kidogo, najua tumekuwa na ongezeko la pesa, lakini ni muhimu ikaongezwa hela zaidi ifikie angalau shilingi bilioni 15, hapo ndipo itakuwa na uwezo wa kuitangaza nchi yetu ili kusudi tuweze kupata watalii wengi, kwani haitoshi kuwa na watalii chini milioni moja hadi sasa na hili lengo lililowekwa la kufikia watalii milioni moja ifikapo 2010 haitoshi. Ukiwapa *TTB* pesa tutafika milioni tatu kwa muda mfupi sana. Naiomba Serikali iliangalie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yapo mengi ya kuongea, lakini basi tuendee hivyo hivyo.

La mwisho, niseme kwamba kwenye eneo la utalii, Mashirika yetu ya ndege ambayo yanasaidia sana katika utalii ni *Air Tanzania* na *Precision Air,* ni vizuri Serikali ikayaangalia haya mashirika ili kuangalia namna ya kuyasaidia yaendelee kuwepo katika biashara kwa sababu ndiyo mashirika pekee yanayoitangaza nchi yetu. Lakini kumekuwa na mtazamo kwamba kwa kuwa *Precision Air* siyo Shirika la Umma, basi labda tusiangalie, hapana! Tubadilishe hilo! Hii *Precision Air* ni Shirika la Ndege lililoko Tanzania, lipo hapa nchini kwetu, ni vizuri Serikali ikawa na mtazamo wa kutumia vyombo vyake vyote vinavyopatikana hapa nchini ili kuhakikisha kuwa tunatumia kila aina ya silaha ili kuhakikisha kuwa utalii unakua kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie kwa kuunga mkono hoja na nilikuwa naongea kwa niaba ya wananchi wa Shinyanga Mjini na katika mpango huu wa utalii natumaini hata Waziri wa Maliasili na Utalii ataungana na mimi katika kupigia debe uwanja wa ndege wa Shinyanga ili kusudi uwe kiungo muhimu katika utalii hususani kufungua mlango wa utalii kwenda Serengeti na Ngorongoro kupitia upande wa Magharibi, kwa sababu kwa sasa Serengeti inaingilika kutokea Mashariki peke yake na ndiyo maana kwa sasa Serengeti inazalisha shilingi bilioni 20 tu. ingeweza kuzalisha mara mbili ya hapa au zaidi kama ingefunguliwa katika milango mingi na uwanja wa ndege wa Shinyanga umekaa vizuri sana kufungua mlango. Unaweza ukawachukua watalii wanaokuja Kigali na Bujumbura kwa kutumia *Air Tanzania* na *Precision Air* ambayo inakwenda kila siku Shinyanga na Jumanne na Jumamosi inakwenda mara mbili, unawapata wale watalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, nashukuru. Sasa namwita Mheshimiwa Estherina J. Kilasi.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na niweze kuungana na wenzangu kuchangia hoja hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii na kabla sijasema lolote, ninaomba kwanza nitoe salamu za

rambirambi kwa Mkurugenzi Msaidizi wa Wizara ya Maliasili na Utalii ndugu yangu mpendwa Miriam na wenzake wote ambao walifariki pamoja naye, naomba Mwenyezi Mungu aziweke roho mahali pema Peponi, Amin!

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefarijika kwamba nimepata nafasi hii ingawa mambo ambayo nitachangia hapa mengi nilichangia kwenye Wizara ya Waziri Mkuu kwenye fungu la Waziri Mkuu na kama unavyofahamu kwamba tumekuwa tukiambiwa kwamba ukichangia hoja kwenye Ofisi ya Waziri au Bajeti itajibiwa kwenye Wizara inayofuata. Lakini kwa utaratibu nilionona kwenye Miundombinu imenigusa kwamba sikujibiwa chochote ambacho nilichangia kule. Kwa hiyo inabidi nichangie hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze tu kwa kusema hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kweli ni nzuri na ninawapongeza sana. Naipongeza kwa maana yale yaliyowekwa huku kwa upande wa ukusanyaji wa mapato kwamba wamejikita zaidi jinsi ya kuboresha utalii, jinsi ambavyo Serikali itaweza kuongeza pato la Taifa kwa kupitia Wizara hii ambacho kimekuwa ni kilio cha muda mrefu sana.

Vilevile nampongeza kwa sababu Wizara hii Katibu Mkuu wake alikuwa ni Mhasibu Mkuu wa Serikali ambaye tulikuwa tunapambana naye sana kwenye Kamati ya Hesabu za Serikali. Ni jinsi gani ambapo mapato yanavuja huko sasa, naamini hili lipo kwake tutakapokuwa tunapitia kutakuwa na ongezeko kubwa sana la mapato. Kwa hiyo, naamini sasa Wizara imepata mtu makini pamoja na Waziri na Naibu Waziri, naomba niwapongeze wote kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nizungumzie jambo lingine la ujumla kwa upande wa mapato yanayotokana na Taasisi ambazo zinaangukia kwenye Wizara hii. Wenzangu wamezungumza hapa na tukisema Maliasili na Utalii watu tunajikita kwenye *TANAPA*, Ngorongoro na Taasisi nyingine.

Lakini nimekuwa nikipata taabu sana, tunapopitisha bajeti hapa ya matumizi ya Wizara hii, kuna matumizi ambayo angalau yalichangia na wenzangu yamekuwa yakitumika miaka mingi nje ya bajeti hii *direct* kutoka *TANAPA*, Ngorongoro lakini hatuoni sasa matumizi yake kuwa yameingizwa huku. Sasa Waziri wa Fedha alipotoa hotuba yake alisema atataka Taasisi hizi zote zichangie mfuko mkuu wa Serikali na hii itakuwa rahisi sana kupitia na kujua Taasisi hizi zimechangia kwa kiasi gani. Sasa kuna mgongano hapa, ndani ya Wabunge tunasema: Je, kwa mfano *TANAPA* ambayo naifahamu zaidi kwa ukaribu na Ngorongoro wakisema wachangie, kodi watalipa? Maana yake sasa wanalipa kodi na bado walipe gawio na bado wawekeze kwenye miradi mingine mipya.

Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu hizi ni Taasisi zake pale ambapo kigezo kitakuwa kimezingatiwa kwamba ni kiasi gani kichangiwe kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, wasisahau kuangalia hili kwamba Taasisi hizi ili ziboreshe Wizara hii au ziboreshe mapato yake inabidi tena zenyewe zijitegemee. Kwa hiyo, ni vitu vya muhimu sana hivi vya kuzingatia.

Lakini kuchangia Mfuko wa Serikali na mimi naunga mkono kwa sababu ndicho ambacho tunakitegemea kwa sasa kwamba Serikali iliwekeza huko ili iweze kupata gawio na gawio ili liweze kuja kuwekeza tena kwenye miradi mingine. Kwa hiyo, ningeomba sana hilo lizingatiwe.

Lingine ni kwa upande wa mapato yanayotokana na Idara ya Misitu. Mimi eneo langu nimeona ni sehemu ambapo mapato yamekuwa yakivuja sana na huku lingetakiwa lizungumzwe kwa uzito. Tunauza mbao na hata magogo lakini kinachopatikana kwetu ni kidogo sana, lakini tunakwenda kununua *furniture* hizo hizo za kutoka China ambazo unatumia kwa miezi mitatu au mwaka mmoja zimeshavunjika zote.

Sasa hilo nafikiri kwamba Serikali hapa ndipo mahali pa kusimamia na ifike wakati muafaka kwamba Serikali yoyote ina *corrective responsibility,* waangalie hao wanaosimamia upande wa misitu na hawa wanaosimamia biashara na wenzetu wa *TRA*, basi *furniture* zinazotoka nje zipewe ushuru mkubwa zaidi kusudi ku-*discourage* watu wasiagize *furniture* kutoka nje wategemee za huku ndani. Kwa hiyo, limekuwa likinigusa sana hilo. *(Makofi)*

Lakini kuna mapato yanayotoka na leseni, Watanzania bado hatuna hulka, unakuta mtu ameanzisha kampuni yake ya utalii, yaani ya kuwasafirisha watalii, lakini kulipia leseni inakuwa ni tatizo, ile inawajibika kulipia kila mwaka, analimbikiza miaka miwili hadi mitatu mpaka umfuatilie, sasa na Sheria hapa haiwabani vizuri. Sheria ndogondogo ni vizuri likaangaliwa hili kwamba mimi nimeanzisha kampuni hii, ninawajibika kulipia kodi, ninawajibika kulipia leseni kusudi mapato ya Wizara hii yaweze kuongezeka. Kwa hiyo, yalikuwa ni mambo ya ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa naomba nijikite kwenye jambo muhimu ambalo limenigusa nichangie ndani ya Wizara hii. Utakumbuka nilizungumza sana kwenye Wizara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye fungu la Ofisi ya Waziri Mkuu kwamba Mbarali sasa kule sikuona kitu chochote kimezungumzwa huku kwenye bajeti. Nimeangalia kwenye Kitabu cha Nne cha Maendeleo sijaona pesa zilizotengwa kutoka kwenye Wizara hii ni jinsi gani watawawezesha wananchi wa Mbarali ili waweze kuwa na maisha bora ya yale ambayo walikuwa nayo hapo zamani.

Ninasema hapa kwamba tumekumbwa na mambo mawili, kwamba ili tupitishe lile eneo la Ihefu kuna watu walivamia pale nakubali wafugaji, ukubwa wa eneo la hekta 80. Serikali ilihamia kule Mbarali wakati wanahamisha ile mifugo na Mheshimiwa Waziri ni shahidi yangu wakati ametembelea Mbarali, alikuta jinsi ng’ombe walivyokuwa wanakusanywa, wamekonda, wanakufa na aliona kwa masikitiko makubwa sana. Lakini wananchi walikubali kuondoka na sisi na mimi kama Mbunge nimeendelea kushawishi wananchi wale kwamba huko mnakokwenda ni kuzuri, kumetengwa maeneo na hakuna tatizo lakini achieni hili eneo. Lakini wengi hawakuweza kuondoka kwa wakati kwa sababu Serikali ilikuwa bado haijaamua ni wapi waende.

Sasa ilipifika wakati ule nakumbuka Kamati ya Manaibu Waziri ambayo ilikuja Mbarali ikiongozwa na Mhehimiwa Rita Mlaki walitumwa na Waziri Mkuu aliyepita

Mheshimiwa Edward N. Lowassa baada ya mimi na Mheshimiwa John Cheyo kuongea kwamba wananchi, wale wafugaji, wanapata shida sana ya kuhamisha ile mifugo hasa baada ya kutoka Ihefu na kuingia kwenye vijiji na lengo ni kuachia vyanzo vya maji tu. Tulikuwa bado hatujafikia lengo la kuongeza ile hifadhi.

Sasa ile timu ilipokuja ya Mawaziri na mimi nilitegemea jambo la kwenda kujikita pale ni kuangalia ni jinsi gani watawasaidia wale wafugaji wahame na njia zao za kupita, lakini cha ajabu na cha masikitiko taarifa ile ambayo na mimi angalau nilibahatika kupitia mahali ilikuwa imsute Mbunge zaidi kwamba mimi nawashawishi wale watu wasihame, ninawashawishi watu wasiuze mashamba, lakini kilichowapeleka ilikuwa ni kuangalia jinsi gani ile mifugo itaondoka. Lakini wakajikita kwenye jambo lingine ambalo siyo ambalo walikuwa wameagizwa kufanya.

Sasa hivi mimi imekuwa ikinipa shida kwamba Serikali inapoazimia jambo fulani likifanikiwa inasahau kabisa, kwamba kuna watu waliowahamisha pale wanaotakiwa wawatengenezee eneo zuri ili kuondoa zile hasira za mara kwa mara. Sasa hilo lilikuwa la mifugo ambalo bahati nzuri Mheshimiwa Rais kwa vyombo vyake aliona tatizo hilo akateua timu na mimi nikawepo, hilo namwachia Mheshimiwa Rais na maamuzi yake.

Lakini la pili ninalozungumza ni kuhamisha watu ambao hawakuwa ndani ya ile Ihefu, baada ya Serikali kuona kwamba lile eneo halitoshi sasa ilibidi vijiji vingine viongezwe ili kusudi kupanua ile hifadhi ya Ruaha.

Ninapozungumza hapa, hakuna chochote kinachozungumzwa huko, wale watu tulipita kuwahamasisha na Mheshimiwa Waziri anajua na Wizara tatu zilihusika pamoja na TAMISEMI, Wizara ya Elimu na Wizara ya Mifugo kwamba wazingatie waungane pamoja.

Sasa mimi nashindwa maana wameniachia Mbunge na wenzangu wa Mbarali tuongee na *TANAPA* sijaona tena yale magari yanayokuja Mbarali kama mwanzo, sijaona tena Mawaziri wanatembelea tena Mbarali kuangalia wale wananchi wamekaaje, *TANAPA* haingii ndani ya Bunge, ni nani ambaye anaweza akanijibu ndani ya Bunge?

Lakini vilevile nakosa nguvu ya kumlazimisha mtu wa *TANAPA*. Mimi nafikiri ile Taasisi ambapo imepewa tu nafasi ya kusimamia na kuwekeza baada ya Serikali kuondoa hizi kero zote za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapozungumza, wananchi wa Mbarali kwenye vijiji saba wamehama na shule zao ambazo zilikuwa zimejengwa kwa mfuko wa *MMEM* na nguvu zao zote wakati huo waliahidiwa kwamba huko mtakakohamia mtajengewa miundombinu kwa maana ya maji, Zahanati na shule ninyi kazi yenu baada ya kupewa fidia na viwanja mtakuta vimepimwa, barabara zimepasuliwa, siyo kitu ambacho kiko sasa. Wengine walihama tangu mwezi wa kumi na moja mwaka jana wamenyeshewa na mvua na wamekuta eneo halina chochote miundombinu yoyote kurudisha hali ya shule zote pamoja na Zahanati, itatugharimu karibu shilingi bilioni 2.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiongea na *TANAPA* wanasema hizo pesa hatuna kwenye bajeti, tumejitahidi tu kulipia fidia ambayo itafikia karibia shilingi bilioni 6.6 na mimi naungana nao kwa sababu vilevile na mimi ni Makamu Mwenyekiti wa Mashirika ya Umma, naelewa hali yao ilivyo nilifikiri bajeti hii sasa Wizara inawekewa.

Tumetayarisha michanganuo ya hapa *write up* yetu ya gharama zote tukapeleka Wizarani, TAMISEMI na sehemu zote muhimu nilijua leo bajeti hapa itasema chochote na sasa tuna miezi mitatu kwamba mwezi wa kumi na moja ukifika wananchi wale watakumbwa na mvua kwani itakuwa imeanza kunyesha, bado wataendelea kunyeshewa huko, wanafunzi wa shule za msingi, miezi mitatu hawajaingia darasani, wamekuwa wakijibanza tu na ninafikiri kwenye *TV* mmekuwa mnaona. Sasa Serikali inasemaje kuhusu hili? *(Makofi)*

Mheshimiw aNaibu Spika, napongeza kweli Ihefu kumeota vizuri na kwa sababu maji yanaendelea kujaa Mtera ninaamini mmesahau kwamba waliohama kule ni watu sio wanyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachomwomba Waziri wa Maliasili, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, amefika Mbarali ameiona hali; mahali mnaponiweka ni pabaya sana kuliko mnavyotegemea. Madiwani wangu hivi ninavyoongea, wamezunguka Wilayani kwenye Vijiji vyote ambavyo wamehama kwenda kufanya tathmini, wamekuta baadhi ya Wananchi wamedhulumiwa mashamba, *TANAPA* kwa kusuasua kidogo angalau wamejenga nyumba tano na madarasa na wanasema hawana uwezo wa kurudishia shule zote hasa zile za MMEM.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sijamwona Waziri wa Elimu akishtuka kwenye hili, sijamwona kuja kuangalia hali hii ikoje. Zahanati ambazo wenzetu watakuwa wanaendelea sisi tunaanza upya kwenye vijiji saba, sijamwona Waziri wa Afya akizungumzia hili kwamba, atatoa fedha kwa ajili ya kujenga hizo zahanati. Kwa hiyo, leo ninachoomba Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii anipe jibu ni juu ya hizi shilingi bilioni mbili atatoa au kutujengea. Tunachofurahia ni kwamba, Ihefu pamerudia hali yake, tunafurahia Mtera kwamba maji yamejaa, basi wananchi nao wapeni maisha bora ambayo walitegemea kuyapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwarudishie furaha yao, nakumbuka Mheshimiwa Nyalandu alisema, kwa nini tunawapa hasira wananchi, kila wakati wanakuwa wameikasirikia Serikali yao lakini wao lengo lao lilikuwa ni kuchangia tu kwamba tunaunga Azimio la Serikali, tunajua faida ya Hifadhi ya Taifa kwa Nyanda za Juu Kusini lakini sasa hapa tunahitaji Serikali itusaidie? Sasa sijui tutamfukuza nani katika Serikali hii, Mkuu wa Mkoa analalamika, tukija kwa Waziri wa Maliasili na Utalii naye alalamike, sijui twende tukampigie magoti Rais atuangalie kule?

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri Mheshimiwa Waziri ana majibu na naomba suala hili nisiliongee tena leo iwe mwisho, ninaporudi Mbarali nijue kabisa ni kitu gani

kitafanyika kule, kama ni TAMISEMI, Elimu, Afya na hii Maliasili na Utalii na Mifugo, basi waungane kwenye hizo bajeti ili wajue wanawasaidiaje Wananchi wa Mbarali hawa wa Vijiji saba na Vitongoji vingine ambavyo sijavitaja, basi wanapata zile ahadi ambazo Serikali imeahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, haitakuwa busara kufurahia Ihefu kumenawiri wakati watu wangu wanapata matatizo. Kwa hiyo, naliongea hili na naamini wanasikia; wananchi wangu wamekuwa maskini, ng'ombe wamekufa, hata si wale waliohamia na waliokuwepo, hali halisi ninayoizungumza wanaifahamu na je, hawa watu wanyeshewe mvua, hakuna maji, barabara, wala zahanati?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba, naiunga mkono hoja hii kwa kupitisha bajeti kwa yale yaliyoelekezwa humu, lakini kwa hilo naomba nipate jibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia Hotuba ya Maliasili na Utalii. Awali ya yote, napenda nimpongeze Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kwa hotuba yake nzuri. Vilevile napenda nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote, kwa kuandaa hotuba nzuri. *(Makofi)*

Kipekee, naomba niipongeze Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa kujali *gender*; Waziri wa Maliasili na Utalii ni mwanamke dada yangu Shamsa, Katibu Mkuu Mama Blandina ni mwanamke, Mkurugenzi wa Utalii ni mwanamke, Msemaji Mkuu wa Upinzani pia alikuwa ni mwanamke, nami kama mdau wa utalii sina pingamizi kabisa na hotuba yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu wa Sekta hii ya Utalii, naomba ninukuu Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambapo alisema: "Ukuaji wa Sekta ya Utalii ni muhimu sana katika jitihada zetu za kuongeza mauzo ya nje. Kwa kipindi cha mwaka 2007, mchango wa Sekta hiyo kwenye mauzo ya nje, ulifikia Dola za Marekani bilioni moja pointi sifuri nne, sawa na asilimia ishirini na nane pointi nane ya mauzo yetu ya nje. Sekta hii ndiyo iliyotoa mchango mkubwa katika mauzo ya nje, ikilinganishwa na Sekta nyingine zote. Kwa hiyo basi, katika Sekta hii lazima tuwe na utalii endelevu na wenye kujali mazingira."

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mlima Kilimanjaro, kutokana na Kitabu cha Hali ya Uchumi, Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro pekee imeliingizia Taifa Sh. 20,215,920,615, hizi ni fedha nyingi sana. Katika Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro, kuna njia nyingi kuanzia Rongai, Machame, Umbwe, Londorosi, Lemesho Glade, lakini napenda kumwomba Mheshimiwa Waziri katika ile njia ya Machame, wakati huu wa wageni wengi, njia ya Marangu tayari inayo *hut.* Kwa kuanzia tu ile njia ya Machame, tunaomba kwa ajili ya wapagazi, wajaribu kutengeneza mahema ya kulala wapagazi. Fedha zinapatikana nyingi sana na hii itaonyesha kwamba tunauza utalii ambao upo *unique* na ambao upo *uniform*. Sasa hivi *Tour Operators* wengi kila *Tour Operator* anapeleka wapagazi wake na mahema tofauti kule mlimani, kwa hiyo, haionekani vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakiweza kutengeneza mahema ya *temporary,* itasaidia kupunguza mahema mengi kule mlimani na pataonekana vizuri zaidi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, aliangalie hili kwa kuanzia tu Machame na mahema si ghali, pale Arusha wanatengeneza mahema; hema moja la kutosha *Porters* kumi halifiki shilingi milioni mbili. Kwa hiyo, nina hakika kabisa, Mheshimiwa Waziri akiliangalia hili, litasaidia sana katika Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo katika Mlima Kilimanjaro, kumekuwa na vyama vingi vya *porters*. Tumeona kwenye magazeti wanalalamika *Kilimanjaro Porters Association*. Vipo vyama vingi vya *Porters*, nashauri tusiwe na chama kimoja cha *Porters*, vile vyama vilivyopo pale Moshi vyote viruhusiwe lakini Wenyeviti waungane ili waweze kupeleka mapendekezo yao na maoni yao kwa *KINAPA*. Ukisema kwamba, kuwa na chama kimoja itakuwa ni *monopoly*; tumeona katika Mlima Meru sasa hivi kuna chama cha *Porters* wa Kimeru, *Porters* wengine wote hawaruhusiwi kupanda katika Mlima Meru, huu ni ubaguzi.

Sasa tukiruhusu hii katika Mlima Kilimanjaro tuseme kiwe ni chama kimoja tu, italeta matatizo kama ilivyo pale Meru. Meru mtu mwingine yeyote haruhusiwi kupanda, lakini Kilimanjaro wanapanda *Porters* wa Makabila yote, wawe Wapare, Wasambaa, kila mtu anapanda katika Mlima Kilimanjaro. Hatutaki ubaguzi wa *Mount* Meru uwepo na namwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili, kwa sababu linaleta matatizo sana kule Meru. Wale Wameru wanafanya ule mlima ni wao tu, ule mlima ni wa Watanzania wote na sisi pia kama *Tour Operators,* tunawapelekea wageni kule. Kwa hiyo, hawana sababu ya kufanya ubaguzi wowote kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake amesema, watanunua helikopta kwa ajili ya kuangalia ulinzi katika hifadhi zetu. Katika hotuba yangu mwaka uliopita, nilizungumzia kuhusu *rescue, rescue* katika Mlima Kilimanjaro si nzuri sana. Kama ile helikopta itaweza kutumika pia katika kusaidia wakati *emergency* zinapotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mheshimiwa Waziri aangalie katika Mlima Kilimanjaro wale watu wa *rescue* zile nyumba zao zimejengwa kwa bati na mlima Kilimanjaro kuna baridi. Nafikiri Mheshimiwa Waziri anajua kule baridi inafika hata mpaka *minus five*, halafu unakuta mtu wa *rescue* amelala kwenye nyumba ya bati, wanapata baridi sana. Halafu *emergency* ikitokea inabidi waende wakawa-*rescue* wale watu, kwa kweli hawawezi kwenda, utakuta wengine wameugua kwa sababu ya baridi na hili kwa hiyo unakuta ile *system* inakuwa haipo vizuri. Ningependa Mheshimiwa Waziri, aliangalie hilo pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niliulizia kuhusu barabara ya Old Moshi kwamba, itafunguliwa lini? Ile barabara ipo tu imekaa na watalii ni wengi, hata kama hamtaki watu kufika *Uhuru Peak*, na-*suggest* kwamba, ile barabara itumike kwa ajili ya

*acclimatization,* watu wakiwa pale mjini wanaweza kwenda pale kwa siku moja, wana-*acclimatize* halafu wanarudi ndiyo wanakuja kuanza kupanda mlima kwenye hizi *routes* nyingine. Isikae tu bure, inaweza kutumika na tukaliingizia Taifa fedha, nami nipo tayari kabisa kuongeza katika *package* yetu kama njia mojawapo ya kufanya *acclimatization*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri, alipokuwa anajibu swali namba 79 la Mheshimiwa Kimbita alisema, *pack fee* inayotokana na Mlima Kilimanjaro, wametenga milioni mia nne na sita na elfu hamsini kwa ajili ya Halmashauri inayozunguka mlima ule, watu wa Moshi wamenituma nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri, hizo fedha zimetumika kwa kufanyia nini? Wanaomba mchanganuo, maana yake hawajaona maendeleo yoyote yaliyotokana na fedha hizo. Tunaomba mtupe mchanganuo kwamba fedha zile zimetumikaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kuongelea *Northern Circuit*. Naungana kabisa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwamba, zile hoteli za *Sopa Lodges* lazima nao wawekewe kiwango cha kulipa zile *fees*. Hizi hoteli huwa zinajaza wakati wote, hata sasa hivi ukisema unapeleka *booking* ya mwaka kesho kwa ajili ya *season* inayokuja mwezi wa Saba, hoteli zote zipo *full booked*. Sasa kwa nini walipe fedha ndogo kiasi hicho, kwa nini wasiwe wanalipa wakati wanaingia pale kwenye *gate* kama wale wanavyofanya kwenye *mobile tented*? Kwa hiyo, napenda kumshauri Mheshimiwa Waziri kwamba, wawekewe kiwango maalum cha kulipa badala ya kulipa hiyo *fee* ndogo wanayolipa sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo ningependa kuupongeza Uongozi wa Ngorongoro *National Park* kwa kutoruhusu ujenzi wa hoteli nyingine zaidi kwenye ile *rim.* Hili ni jambo zuri na nafikiri Serengeti inabidi wafuate mfano wa Ngorongoro kwa kutoongeza hoteli kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho napenda kumshauri Mheshimiwa Waziri ni kama walivyofanya katika Mlima Kilimanjaro, kuhusu *Local Tour Operators* kupandisha watalii mlimani. Wafanye hivyo hivyo kwenye safari. Sioni kama kuna sababu yoyote, mgeni kuja Tanzania kuchukua gari na kuzunguka kwenye mbuga za wanyama eti amekuja kuwekeza, anawekeza nini? Nafikiri kama anataka kuwekeza aje ajenge hoteli na wakija kujenga hoteli wawe wabia na Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasipokuwa na ubia na Watanzania, itatuletea matatizo. Hata kwenye kitabu kitakatifu kinatueleza, lazima tujali maliasili zetu. Kwa ruhusa yako, naomba ninukuu katika Biblia, Kitabu cha Maombolezo, mlango wa tano, mstari wa kwanza mpaka wa pili unasema hivi: “Ewe Bwana, kumbuka yaliyotupata, utazame kuiona aibu yetu, urithi wetu umegeuka kuwa mali za wageni.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tusikubali kabisa urithi wetu uwe mali ya wageni. Naomba kabisa Mheshimiwa Waziri, wageni wanapokuja kuwekeza hapa, tuhakikishe Watanzania wana hisa katika mali wanazokuja kuwekeza. Tumeona katika vyombo vya habari, kuna mwekezaji ambaye amewekwa huko *Selous* anawanyanyasa watu weusi; ndiyo sisi ni weusi hatukatai, lakini hana sababu ya kutunyanyasa na mali

zetu. Kama tungekuwa na *shares* asingeweza kuongea chochote, kwa hiyo tuhakikishe tuna *shares* katika huo uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tuna utalii mwingi, sasa hivi watu wamekuwa wakiiongelea sana *Northern Circuit*. Tumekuwa tukiiuza Zanzibar sana lakini tunatakiwa tuendeleze sehemu nyingine kama Bagamoyo, sijakataa kuuza utalii wa Zanzibar, tunauuza sana lakini hoteli Zanzibar zimejaa sana. Sasa ni wakati wa kuangalia kuiendeleza Bagamoyo hata Mafia. Mheshimiwa Shah nampelekea wageni wengi sana, Mafia sasa hivi imeanza kupanuka. Kwa hiyo, ni lazima tuangalie ni jinsi gani ya kuweza kuendeleza Mafia na Bagamoyo. Ile Sadani *National Park*, Tanzania jamani tuna vitu *unique*. Mtu anakwenda kwenye *tour,* tembo wanakuja mpaka kwenye bahari ni wapi pengine utaona utalii wa namna hiyo? Kwa hiyo, inabidi tutafute njia ya kuuendeleza utalii huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwa haraka haraka, naomba niongelee kuhusu *Gombe National Park;* wale *Gorillas* ni wa kipekee ambao hawaonekani sehemu nyingine popote duniani ni Tanzania tu. Sisi tunawachaji dola hamsini, mahali kama Rwanda kwenda kuona familia ya *gorillas* wanachaji dola mia tano. Namwomba Mheshimiwa Waziri, aliangalie hili ili tuweze kuchaji *fees* ambazo zinalingana na wenzetu na Mji wa Kigoma uweze kuendelea na ule utalii uendelezwe kule. Kuna vitu vingi sana ambavyo tunaweza kuviendeleza kule na tukaweza kuliingizia mapato Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niipongeze Wizara kwa kuipatia *TTB* fedha za kuweza kwenda kufanya matangazo; ni jambo zuri lakini bado wanahitaji fedha nyingi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunakwenda kufanya maonyesho, haya Makampuni ya *TANAPA* na mengine, yamekuwa yakileta Wenyeviti kule kwenye maonyesho. Sijui wanawaleta hao Wenyeviti kufanya nini?

Ningeshauri watumike wataalam zaidi; tumeni wataalam kwenye haya maonyesho, kama wanataka kuwapa likizo, *holiday*, *motivation* hawa wazee wapeni *holiday* zao. Onyesheni kwenye akaunti zenu *then* watafurahi wapo *holiday,* lakini hakuna sababu ya kumleta mzee anakuja kukaa pale anateseka, anakaa kwenye maonyesho. Huwa nakwenda kwenye maonyesho huwa nawaona, wanakaa tu pale hakuna kitu wanachofanya. Naomba mtume wataalam kwenda kwenye haya maonyesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, namalizia kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi nzuri. Natumaini haya niliyosema watayafuatilia. Naomba kuishia hapa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Kwa hiyo, unaunga mkono hoja? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mkapa, atafuatiwa na Mheshimiwa Lwanji na Mheshimiwa Kimbita naye ajiandae.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii, nami niweze kusema machache katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Awali ya yote, ningependa niungane na wenzangu kwa kutoa pole kwa wafiwa katika ajali ya ndege ambayo imetokea pale Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake. Pamoja na kwamba, wamekaa muda mfupi katika Wizara hii lakini wameonyesha umahiri mkubwa kwamba, hiyo kazi wanaiweza. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nitoe pongezi pia kwa dada yangu, Che Blandina Nyoni, kwa kazi nzuri uliyoifanya ya kuandaa hotuba hii pamoja na watendaji wako wote.

**NAIBU SPIKA:** Sema Katibu Mkuu, maana yake utafikiri dada yako wa kule nyumbani kumbe Katibu Mkuu. *(Kicheko)*

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Katibu Mkuu Che Blandina Nyoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nichangie kama ifuatavyo: Kwa bahati mbaya kwangu utalii hakuna, kwangu kuna kero nyingi sana zinazohusiana na Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Kubwa katika yote, ndugu zangu Wapemba mtanisamehe ni tembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tembo wamekuwa ni kero kubwa sana Wilayani Nanyumbu. Wilaya ya Nanyumbu hatuna raha kwa sababu ya tembo. Tembo wamekuwa ni waharibifu wakubwa, wanaua wapiga kura wangu, ndovu hawa kwa kweli hatujui jinsi ya kuwafanya. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri, atusaidie sisi Wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tembo wanaua watu kwa mfano, nitatoa takwimu; mwaka jana wameuawa watu wawili siku moja. Mzee mmoja alikwenda shambani hakurudi na mama mmoja alikuwa amekwenda na mtoto wake mchanga huko, basi mama yule akafa yule mtoto akabaki na yu hai mpaka leo. Naona tembo aliposikia kelele za mtoto zinazidi akakimbia sababu ya kuogopa kichanga kile kidogo, lakini mama yake alimkanyaga kanyaga akafariki na hii ilikuwa katika Kijiji cha Mtawatawa katika Kata ya Nanyumbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi, mwaka huu mwezi wa Tatu, mama mmoja aliuawa katika Kijiji cha Ndechela Mitonga huko katika Kata ya Napacho. Kwa kweli tembo wanamaliza wapiga kura wangu. Sasa nafikiri katika hilo Daftari la Wapiga Kura, watasajiliwa tembo badala ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kwa uchungu sana, kwa sababu katika kila mikutano ninapokutana na wananchi, kero kubwa ni wanyama hawa waharibifu (ndovu). Kata za Masuguru, Chipuputa, Lumesule katika Vijiji vya Lukwika, Napacho, Mpwahiya na kwingine hawalimi kwani tembo hawa wanafanya uharibifu mkubwa sana. Natabiri kwamba, mwaka huu kutakuwa na njaa kubwa kwa sababu ya uharibifu mkubwa uliofanywa na hawa tembo. Naomba sana atusaidie angalau kuwapunguza hawa tembo, inasemekana wamezaliwa kwa wingi sana. Tunapakana na msitu mmoja wa uwindaji wa Lukwika, sasa nasikia hawa tembo kila siku asubuhi wanatoka Msumbiji wanavuka Mto Ruvuma jioni kama saa hizi wanarudi zao Msumbiji. idadi inaonyesha kwamba, bado ni wengi sana, tunahitaji kusaidiwa ili wapunguzwe hawa.

Kuna dada mmoja pale Afisa Wanyamapori, anaitwa Consolata, yeye ndiye kiboko cha hawa tembo, kwa kweli ana shabaha siku ambayo anatumwa akafanye doria, naona wakisikia harufu yake wale ndovu wanakimbia. Naomba sana Wizara yako, imfikirie huyu dada Consolata, angalau kumpa motisha au kumpandisha cheo kama inawezekana. Ni mwanamke lakini anajua sana kuwadhibiti hawa tembo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naomba ufute maneno haya kwamba ni mwanamke lakini, naomba ufute hayo maneno tafadhali, mwanamke lakini!

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefuta lakini nina maana kwamba, uwezo wake…

**NAIBU SPIKA:** Ni wa mwanaume?

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Ni mkubwa pamoja na kwamba ni mwanamama.

**NAIBU SPIKA:** Tafadhali hebu sema tu kwamba ni hodari.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Naibu Spika, anaimudu sana kazi yake. Nampa hongera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hawa ndovu vilevile kuna nyani, ngedere na tumbili wengi sana katika Wilaya ya Nanyumbu. Tungeomba Wizara ya Maliasili, itusaidie angalau nyavu kuweza kuwadhibiti hawa nyani na ngedere hasa katika Kata za Nandete, Maratani, Mkonona na Mikangaula ni wengi sana; wanaharibu mazao, wananchi wanashindwa jinsi ya kufanya kwa sababu hawana zana za kuwafukuzia au kuwaua.

Nadhani tukipatiwa hizo nyavu na Wizara ya Maliasili na Utalii, tukasambaza katika maeneo haya, tunaweza kudhibiti hawa wanyama waharibifu na pengine wakulima wetu wanaweza kurudisha mazao kutoka mashambani kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ningependa kuieleza Wizara kwamba, mahusiano kati ya hawa wafanyakazi wa msitu wa uwindaji wa Lukwika na wananchi wanaozunguka msitu huo li si mazuri. Maafisa hawa wamekuwa wakiwanyanyasa wananchi, wanafanya misako ya mara kwa mara, ambayo si ya kibinadamu, vitisho, mara nyingine huwa panatokea ugomvi kati yao na wananchi hasa sehemu za Mpombe, Chimika na Masuguru. Katika sehemu hizi wanawatisha sana wananchi, wanafanya misako ambayo haistahili. Unapovunja mahusiano na wananchi, hata wao kuulinda ule msitu inakuwa ni shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile hawanufaiki na wanyama walio katika msitu ule. Wao wanawaangalia tu, naomba Wizara ifanye mpango angalau mara moja moja, wanyama wanaouawa wapatiwe hawa wananchi, sio bure kwa kuwauzia. Ni mara chache tu nimeona tembo wakiua watu ndipo wanauawa na ndiyo wanauza hiyo nyama lakini si wote wanaotumia hiyo nyama ya tembo. Naomba hawa wanyama wengine ambao wanatumiwa na watu wengi wauawe wakati mwingine ili kuwapatia wananchi angalau kwa gharama ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Nanyumbu tuna tatizo la gari ya doria, hatuna gari la doria. Naomba Wizara itusaidie gari moja la kufanyia doria, si lazima liwe jipya, angalau Mheshimiwa Waziri atafute kule Wizarani kwake au sehemu nyingine yoyote, atusaidie gari moja ili angalau tukisikia haya matukio ya watu kuuawa na tembo au tembo kuharibu mazao, basi Afisa Maliasili aweze kwenda mara moja na kuweza kuidhibiti hali hiyo kabla haijawa mbaya zaidi. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, atusaidie gari la doria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utalii, Mkoa wa Mtwara kwa kweli tumesahauliwa sana. Watu wanasema usilolijua ni kama usiku wa giza. Sisi tuna fukwe nzuri sana katika Mikoa ya Mtwara na Lindi, tuna sehemu ambazo ni vivutio vya kale kwa mfano Mikindani. Ukifika pale utakuta nyumba za kale, historia iko pale, kulikuwa na biashara ya utumwa lakini historia ile inakufa hivi hivi, Wizara haitaki hata kuitupia macho sehemu ile. Idara hizo za utalii hazitaki kutangaza fukwe za Mtwara na Lindi na sehemu zile za historia za Kilwa, pamoja na Mtwara pale Mikindani. Nawaomba waje Mikindani waone historia jinsi ilivyojengeka kama ilivyo kwa Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninalotaka kulizungumzia ni la urinaji wa nyuki sijui wengine wanaita ufugaji lakini mimi naita urinaji. Kwetu Wilayani Nanyumbu, kuna warinaji wa asali wengi sana lakini elimu hii haiwafikii, zana wanazotumia ni duni, mizinga yao ni ile ya kizamani na si ya kisasa. Pamoja na hayo, wananyanyaswa sana hasa unapofikia wakati wa kurina asali. Wanauza kwa usiri kwa kuogopa Maafisa Maliasili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kwa sababu hakuna elimu yoyote inayowafikia, wafanye nini, waende wapi, kama kuna mambo ya leseni wakakate vipi. Asali ni nyingi sana Wilayani Nanyumbu, ukifika kwenye Kijiji cha Muungano pale Maratani, asali ni nyingi lakini wananchi wanaogopa wapeleke wapi au wafanye nini kwa sababu ya vitisho vya Maafisa Maliasili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na matatizo haya yote, namwomba Mheshimiwa Waziri au Naibu wake, watutembelee Wilayani Nanyumbu. Mambo mengi watajionea kule, kama ni hizi kero watazikuta kule, naomba waje watusaidie angalau kukutana na wananchi ili waweze kuwamalizia kiu yao, wawaone na pia wafikishe matatizo yao kwao. Nikiambiwa nichague kati yao nani, ningesema Mheshimiwa Mwangunga tufuatane wote. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si kwamba ndugu yangu Maige simtaki hapana, lakini nafikiri ningependa sana Mheshimiwa Mwangunga tufuatane wote, akaone tabu za kule kama kulala sehemu finyu basi ni hiyo hiyo, asiogope, naomba aje tusaidiane kutatua kero za wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Unaamini kabisa mama ana huruma. Mheshimiwa Lwanji, atafuatiwa na Mheshimiwa Kimbita na Mheshimiwa Mwenegoha ajiandae pia.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa bahati mbaya, sitaunga mkono hoja hii. Nampenda sana ndugu yangu, mdogo wangu, Mheshimiwa Ezekiel Maige lakini atanisamehe. Labda nitafikiria kufanya hivyo, baadae niunganishe kwa ndugu yangu aliyeketi sasa hivi kwamba, nitamhitaji Mheshimiwa Waziri, tufuatane kwa wiki moja kuanzia tarehe 1 - 7 Septemba, 2008 akajionee matatizo ya maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mteja na mdau mkubwa wa Wizara hii na sitaacha kuzungumza matatizo ya Wizara hii mpaka nimeondoka Bungeni, kwa sababu Mbuga za Akiba Rungwa, Kizigo, Mhesa na Chaya ziko jimboni kwangu na ndiyo tunaojionea matatizo makubwa. Nitaomba iwe hivyo kwamba, tufuatane na Mheshimiwa Waziri, tukaone hali halisi. Nitamwomba Mheshimiwa Waziri mwenyewe wala siyo Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeliomba pia wanieleze kwa nini mpaka leo Wizara hii haijaja na utaratibu wa kuunda Bodi ya Asali? Hili zao ni muhimu sana lakini mpaka leo linafanywa kama vile ni zao tu la mchezo. Kenya na Uganda wana Bodi ya Asali, wana Baraza la Asali, lakini hapa nchini hatuna ni kama chakula cha watoto tu. Ni ajabu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia anihakikishie kama watakuja na sera mpya ya kuwajali binadamu wanaoishi maeneo hayo. Maana kuna *feelings* kwamba wanyama wanaonekana kama vile wanahifadhiwa vizuri zaidi kuliko binadamu. Sasa sera hii ni ya wapi maana ina mnuko wa ukoloni ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia anihakikishie kama atatenga fedha za kutosha kwa ajili ya doria, risasi, posho za watumishi, usafiri na kuongeza idadi ya wafanyakazi wa idara hiyo katika maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ina Sera gani juu ya uvunaji wa mbao kwenye mapori haya? Kuna mgodi gani ulioko ndani ya Mbuga ya Akiba ya Muhesi, maana kuna mgodi bubu unaendelea mle ndani na sidhani kama Serikali ina habari hiyo. Ningependa kujua hatma ya Bwawa la Rungwa, nikipata majibu hayo basi kesho nadhani itakuwa ahueni kidogo. Yote haya yana *revolve* kwenye rasilimali. Rasilimali zetu zinakwenda kuleta maendeleo sehemu nyingine, sisi tunaachwa hivi hivi.

Amilcar Cabral yule mwanaharakati aliyepigia vita vya *Guinea Bissau* alisema kwamba, watu hawapigani kwa sababu ya mawazo au hoja, watu wanapigana kwa sababu ya rasilimali. Maana Wareno walipokuwa wanashindwa hivyo vita, wakataka wa-*negotiate* yeye akakataa kutoka msituni, wakamwambia kwa nini unakataa kutoka? Akasema hapana wanihakikishie kwanza rasilimali, Ken Sarowiwa alikufa kwa sababu ya kugombea mafuta ya kwao. Yanauzwa mafuta yanakwenda ku-*beef up bank accounts Uswiss*, *bank account* za majenerali wanaotoka Kaskazini. Sasa hakuwa na sababu ya kuchanganya maneno alisema wazi kwamba, mafuta haya kwanza ya-*develop* hapa ndiyo yaende sehemu nyingine. Lakini sisi tumeachwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lile kuna makampuni karibu kumi yanawinda pale. *Hunting blocks 13* kuna *Tanganyika Game Trackers Safaris*, *Winget Windrose Safaris*, *Foa Adventure Safaris*, *Miombo Hunting Safaris*, *Marera hunting Safaris*, *Robin Hurt Safaris*, *Mwanauta Hunting Safaris* na inakuja kampuni moja inaitwa *Namagoya Hunting Safaris*. Hakuna kinachokuwa *ploughed back* pale, mbali ya juhudi za huu Mfuko wa Wanyamapori kutusaidia bwawa la Rungwa, hakuna kitu zaidi. Hawa *they are paying*, mpaka wafuatwe na mara nyingine mpaka Mbunge awafuatilie, sasa wanataka na mimi niingie majaribuni. Maana unapowafuatia watu wanaweza kukuandikia *cheque* wakasema nyamaza. Huo ndiyo ukweli. Kwa hiyo, siyo kazi yangu mimi. Kwa nini hakuna sheria inayowabana hawa watu, wanawaachia eti waamue wenyewe katika muda muafaka? Why? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba iwekwe sheria ya kuwabana hawa watu kulipa mrabaha. *Just 20% they are failing to pay this. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbuga za Akiba za Rungwa/Kizigo na Mhesi, zina kilomita za mraba 13000, sawa na Mkoa wa Kilimanjaro. Kinachofanyika mle ndani hakuna anayejua; mbao zile na asali zimeachwa kwa walanguzi. Wanyama wengine wanachukuliwa. Kuna wakati Loliondo wanyama walikuwa wanachukuliwa na kule tuna kiwanja cha ndege. Mambo hayo yanafanyika ni mbali. Toka Uhuru sidhani kama kuna Waziri wa Maliasili aliyewahi kulala Rungwa au kufika Rungwa hakuna. Mheshimiwa Diallo aliishia Manyoni tu, lakini toka Hasnu Makame hakuna hata aliyefika wanasubiri ripoti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa ukoloni kulikuwa kuna kibao Itigi pale kilikuwa kinaandikwa hivi, nadhani wengine Mama Batenga aliuliza siku moja, kimeandikwa hivi; *you are now entering uncivilized world please buy food and refreshments before departure.* Unatoka Itigi kwenda Mbeya, tumeachiwa hiyo *legacy* kwamba sisi *we are uncivilized*, hatuna tofauti na *bushmen* wa Kalahari. *Gods must be crazy* yule bwana alikuwa anakimbia sana kwenye ile filamu yeye ni kuongoza misafara ya watalii anaachiwa makopo ya nyama na soda basi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningeliomba *legacy* hii itoke. Ninaomba sana hatuna barabara, hatuna shule za kutosha, hatuna zahanati, tunategemea fadhila za *missionaries* utafikiri miaka ya zamani, hata wale wanashangaa sana. Wametujengea hospitali nzuri pale Mgandu St. Vincent, *St. Gasper* Itigi, lakini barabara tunashindwa, tunataka wao tena watujengee barabara wakati mali lukuki tunazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia azma yangu kwamba, mgawanyo wa *recourses* huu tupewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumza sana kuhusu matatizo ya eneo hili, toka mwaka juzi, mwaka jana mwishoni wakaniona labda huyu bwana ni zumbukuku au vipi. Unajua asubuhi huwa tunapofoleni pale kwa ajili ya *breakfast,* Waheshimiwa Wabunge wengi wanapenda sana supu ya utumbo, kwa sababu inaweka joto halafu na ni *roughage* nzuri, lakini wanapenda kula. Ukiambiwa ondoka hapa unazungumza utumbo hapo sasa, ukiambiwa wewe bwana unazungumza utumbo *is a different thing* unaona hapa. Sasa tunakula utumbo ule asubuhi pale wote Wabunge wawili, watatu, tukifika hapa mwingine unaambiwa kwamba, wewe unazungumza la maana wewe bwana unazungumza utumbo tu, maana habari ya simba, tembo, nimeizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina barua hapa kutoka ofisi ya chama, sasa hivi ni suala la siasa maana simba na tembo imekuwa ni siasa. Kutoka kwa Katibu wa Chama wa Wilaya inakwenda kwa Mkurugenzi inasema, maamuzi ya Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya ya Manyoni. Tafadhali husika, Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Wilaya katika kikao chake maalum kilichoketi tarehe 28 Juni, pamoja na mambo mengine, kilizungumzia kwa kina suala la wanyama waharibifu, tembo wamekuwa wakila mazao ya wananchi yaliyoko mashambani na yale yaliyovunwa. Yale yaliyovunwa huwa tunaweka nyuma ya nyumba wanafika mpaka huko.

Simba wamekuwa tishio kwa kula watu. Sasa hivi wameshaonekana maeneo ya Mkwese, Ipande na Mwenyekiti wa CCM tawi hilo ametafunwa mguu amelazwa St. Gasper kwa ajili ya matibabu. Watu wengine walioliwa na simba Kitaraka, Doroto na mpakani mwa Singida Vijijini, Singida wameliwa watu 14 katika muda mfupi sana. Labda siku moja simba huyu akosee aingie humu Bungeni ndio mtasikia. Hii ni barua labda ndiyo kilio kitasikika. Hii ni kutokana na mipaka; mipaka ile iliyokuwepo awali kwa sababu ya uchoyo wa hela na kwa sababu ya kukosa uzalendo wale wafanyakazi wamesogeza mipaka mpaka ukingoni mwa vijijini, watu waende wapi?

Kwa hiyo, hiki kilio tunachohitaji rasilimali zetu tupewe. *We need a sort of democratic capitalism* kwamba na sisi kila mtu walau apate chochote. Sasa isiwe *capitalism* ya mtu mmoja tajiri wa kupindukia na kabla ya kufa anaachia urithi wake mbwa na siyo binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *rates* kwa mfano, simba akiuawa, anauzwa dola 2500, tembo dola 15,000 mpaka 20,000 hiyo ni milioni 15 mpaka 20, pundamilia dola 1200, nyati dola 1400, nyumbu dola 650, pofu dola 1500. Sasa unaambiwa anayeuawa na simba anapewa kifuta jasho cha shilingi 200,000; huyu simba yeye akifa dola 2500 lakini binadamu shilingi 200,000. Hekta moja ni sawa na ekari mbili na nusu; eti mnalipa kifuta jasho cha shilingi 100,000; kweli hizi ni sera za wapi? Hatuwezi kuwa na Sera za namna hiyo za kuwabagua wananchi wetu sisi wenyewe.

Bwana mmoja Lianga alifanya kazi za Serikali za kuchangisha michango ya sekondari anarudi kuwasilisha michango, alikuwa mjasirimali mzuri amefungua duka, familia yake inamtegemea, yule bwana alikamatwa na simba akatafunwa akabakizwa kichwa, familia yake tunamlipa shilingi 200,000. Mimi nadhani angepewa thamani ya tembo mmoja; milioni 15, milioni 20. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba waje na Sera zinazotetea binadamu. Mbuga hizi za akiba mahusiano ni mabaya kati ya wafanyakazi pamoja na wananchi wa maeneo hayo. Kwa sababu hawawajali wananchi hata kidogo, halafu wanawaambia kwamba, *lets co-operate* hata Tume ya Haki za Binadamu imetembelea mwaka jana maeneo yale wamekuta kilio ni hicho hicho, wananchi wanaambiwa tushirikiane. Hata Mahtma Gandhi alisema; *if co-operation is a duty I hold that non co-operation also under certain conditions is equally a duty*. Wana haki kabisa ya kukataa kwa sababu hawanufaiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nahitimisha kwa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyosema juzi kwamba, tusikubali watu wachache watumie fedha zetu kiujanja, tuwabaini na kuwadhibiti. Hii ipo ukurasa wa 88, fungu la 126 na ndiyo hapo kuna wajanja wengi katika Wizara hii. Pakacha linavuja hapo sana, pamoja na kwamba, tumeambiwa ndiyo Sekta iliyoingiza fedha nyingi sana nchini lakini ukweli ni kwamba, pakacha linavuja. Ningeliomba ndugu zetu hawa wahakikishe *resources* hizi zinatusaidia sote hususan maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimezungumza kwa hisia kali siyo kawaida yangu, lakini nadhani *message* imefika, wenzetu watuangalie na watuonee huruma. Nawashukuru sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, naamini wamesikia uchungu wako mkubwa.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi jioni hii. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutufikisha hapa na kutujali uzima tulionao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwape pole sana Wizara nzima ya Maliasili na Utalii, kwa msiba mkubwa walioupata kutokana na ajali ya ndege, ambapo tulipotelewa na wataalam wetu. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Waziri, kwa kipindi kifupi amekaa hapo Wizarani kwa kushirikiana na Naibu Waziri, pamoja na Katibu Mkuu wameweza kutuletea hotuba ambayo tumeisoma na inaanza kutupa mwanga na mwelekeo, nawapongeza pamoja na watendaji wengine wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri, yapo mambo mengine ambayo tunajiuliza sisi wengine siku nyingi kidogo, lakini sasa hatua zimeanza kuchukuliwa. Tuliyokuwa tumesikia kutoka kwenye hotuba ya mwaka jana ya Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, kuziweka hoteli zetu kwenye madaraja. Kwa sababu hata wageni wa nje, wanakuja hapa wenye uwezo mbalimbali. Mwingine anataka kujua atalala kwenye hoteli yenye daraja gani. Sasa hatukuwa na hali hiyo hapa nchini. Kwa hiyo, nawapongeza kwa kuanza hilo zoezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nashukuru kwamba, wanajenga Chuo cha Utalii sasa hivi. Nchi za wenzetu jirani wanatuzidi katika mambo ya utalii, kwa sababu ya mambo ya kisomo. Wenzetu wale wanapita kwenye vyuo, tunavyo vyuo ndiyo, lakini hicho chuo wanachokijenga, ninatumaini kitakuwa kishawishi kikubwa zaidi na tutaweza kutoa wataalam wengi zaidi, ambapo wakihudumia wageni wetu, wageni wetu watakuwa wanajisikia kwamba, wanahudumiwa *professionally*. Kwa hiyo, ninawapongeza na ninawashukuru kwa kuanzisha hicho Chuo cha Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenzangu alizungumzia kuhusu zile *dollar* 450,000 zilizopelekwa kwenye Balozi zetu. Mimi ningeomba zitumike, bado ni kidogo; ninasema ni kidogo kwa sababu hatujautangaza utalii wetu vya kutosha na njia mojawapo tuliyokuwanayo ni katika Balozi zetu. Ningeomba Balozi zetu ziwe na vitengo maalum vya kutangaza utalii ambao Mwenyezi Mungu ametujalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitembea katika baadhi ya nchi ukitaja Tanzania, anakuuliza huko ni wapi, Kenya hivi au Afrika ya Kusini. Sasa hivi tumeanza kufahamika fahamika kutokana na Mikutano mikubwa, kwa mfano, mkutano mkubwa wa Sullivan uliofanyika Arusha. Jitahada anazozifanya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete ni kubwa sana kuitangaza nchi yetu, tunaanza kufahamika vizuri na hizo taarifa kwenye Vyombo vya Habari zinafanya Tanzania tunaendelea kuwepo kwenye ramani ya dunia kwa kufahamika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nizidi kuomba kwamba, Wizara isichelewe ipeleke fedha kwa wingi zaidi katika Balozi zetu ili vianzishwe Vitengo Maalum kwa maana ya kuutangaza utalii au vivutio tulivyonavyo hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanya hivyo, ningependekeza kuanzishwe Mfuko wa Utalii. Huo Mfuko wa Utalii sijui kama upo, natumaini haupo, lakini

ukianzishwa Mfuko wa Utalii utatusaidia sana. Hapa kila Mheshimiwa Mbunge, amezungumzia vyanzo mbalimbali au vivutio mbalimbali vilivyopo katika Majimbo yetu. Sasa huo Mfuko wa Utalii ungetusaidia sana tuweze kupeleka zile taarifa katika hicho chombo nao wangetushauri kuhusu hivyo vivutio tulivyonavyo na ili kuweka mikakati ya kuanza kuvitangaza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hoja yake, aniambie kama Mfuko wa Utalii upo au haupo na kama haupo; je, anakubaliana na mimi kuuanzisha Mfuko wa Utalii?

Mheshimiwa Naibu Spika, kidogo tunapata tatizo, tunajiuliza Tanzania tatizo liko wapi? Tumejaliwa vitu vingi mno, lakini tunashindwa kuvitumia inavyofaa au inavyopasa, tumejaliwa madini kwa wingi sana, hali nzuri ya ardhi, bahati mbaya ardhi nyingine ndiyo hiyo tumeanza kulima jetrofa badala ya kulima mazao ya chakula.

Mhseshimiwa Naibu Spika, lakini tukija kwenye mambo ya utalii, tuna vivutio vingi sana, vingine ni urithi wa dunia sasa hivi, lakini hali za wananchi wetu ni duni sana. Sasa ukijiuliza kwa nini tunakuwa maskini; jibu linakuwa ni vigumu sana kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya wageni wanafika hapa nchini wakitembea kidogo wanajiuliza, hivi kwa nini ninyi ni maskini na shida iko wapi? Kuna baadhi ya wageni wanafika hapa nchini kwetu kwa *briefcase*, baada ya muda mfupi ni matajiri wa kupindukia katika nyanja zote. Matajiri wakubwa mno wa kupindukia, lakini alikuja na *briefcase* tu na kichwa chake wakati sisi Watanzania tupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningeomba kwa ujumla wetu, Watanzania tuwe na uwezo wa ku-*create* mambo, lakini na pale tunapo-*create* mambo tupate *support* kutoka kwenye Idara zinazohusika, tupeane msukumo, wazo saa nyingine ukilipeleka Mwafrika kwa Mtanzania mwenzako, inawezekana likaonekana labda halijawa timilifu. Lakini mgeni akija na wazo lake hapo hapo anaanza kuchuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi ningeomba kwamba tujitahidi, tuvitumie vitu vyote hivi vizuri ambavyo Mwenyezi Mungu, ametujalia ili tuweze kuwaokoa wananchi wetu. Tusipofanya hivyo, tutakuja kujilaumu na tutakuja kuishia mahali pabaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, utalii umezungumziwa wa aina nyingi sana. Sasa nikirudi kule kwangu Mkoani Kilimanjaro, nikianza pale Jimboni kwangu Hai, tunavyo vivutio vingi vya utalii. Tunataka tuanze kujipanga sisi wenyewe, kuweka utaratibu mzuri wa kuanza kuvitangaza vile vivutio ili tuombe na ushirikiano kupitia Wizara na ili tuweze kupatia utaalam uliopo pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya tambarare tunayo sehemu inaitwa Chemka, Chemka ni maji yanayotoka ardhini tu yakiwa na uvuguvugu. Wenzetu kule Ulaya

wanatumia hata lile tope, ukijipakaa wanasema *healing* ya mambo ya *romatism*, sisi tumekaa tu na kile kivutio pale hatujakitumia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo maeneo mbalimbali, ukija nyanda za juu huku ambako yalikuwa mahandaki ya zamani ya wakati wa vita vya wenyewe kwa wenyewe, ambayo pia tunaweza kuyatumia kama vivutio vya utalii kule vya Nseny Ngira, ukienda huko Ng'uni kuna mapango mengi tu. Kwa jumla ni kwamba, tunavyo vivutio vingi na mimi ninachukulia hivi vilivyopo ndani ya Wilaya yangu kwamba, kila Mheshimiwa Mbunge hapa anavyo vivutio. Vitu vingi tu vipo katika nchi yetu, ambavyo tungeweza kuvitumia kwa maana ya utalii ambavyo vitakuja kutusaidia hii tunayosema, *Cultural Tourism*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Kilimanjaro tunayo ile dhahabu yetu, ni ule Mlima tu na ninamwomba Mheshimiwa Waziri na wale Watendaji pale Wizarani, wasinichoke ninapozungumzia Mlima Kilimanjaro, ndiyo dhahabu tuliyojaliwa na Mwenyezi Mungu. Hatuna dhahabu nyingine pale Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kahama, Geita kule wanayo dhahabu na almasi na vitu vingine. Kilimanjaro dhahabu yetu ni Mlima Kilimanjaro jamani na ninaomba ieleweke hivyo. Sasa ule Mlima Kilimanjaro wale ambao wanafahamu mambo ya utalii na wageni wanaokuja wanasema, bado hatujautumia vizuri. Bado kuna uwezekano wa kuendelea kuutumia ule Mlima Kilimanjaro kama Taifa, tukaendelea kupata kipato, kama wananchi wanaozunguka ule Mlima Kilimanjaro wakaendelea kuwa na maisha mazuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara nyingi au *route* za kupanda ule Mlima Kilimanjaro siyo nyingi sana sasa hivi, lakini bado zipo nyingi ambazo zinaweza kutumika na kusaidia katika kuongeza kipato cha nchi yetu na kuinua hali za wale wananchi wanaozunguka ule Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru rafiki yangu, Mheshimiwa Naibu Waziri Ezekiel Maige, nilipouliza swali langu Namba 79 tulitofautiana kiasi pale, lakini baadaye tulikuja kuwekana sawa na ninaomba yale tuliyoyazungumza yatekelezwe yawe mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mlima Kilimanjaro tukiweza kuutumia vizuri unaweza kuchangia mpaka *one third* ya bajeti ya nchi yetu. Wenzetu Afrika Kusini wanasema njoo Johannesburg ukauone Mlima Kilimanjaro, wenzetu Kenya wanasema njoo Nairobi uuone Mlima Kilimanjaro. Sasa sisi tungeweza kusema njoo kwetu Tanzania uushike Mlima Kilimanjaro, siyo kuuona au kuuangalia. Sisi ni kwamba unafika kwenye Mlima wenyewe, *contact yourself on the land of the Kilimanjaro Tanzania.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuna tatizo linalokuja mahali hapa; kuna utaratibu ambao nimeelimishwa kupitia Wizarani kutokana na kile kinachoweza kwenda kwenye zile jamii zinazouzunguka ule Mlima Kilimanjaro. Mambo ya Ujirani Mwema nimeelewa

vizuri, lakini ningeomba Wizara ikae vizuri; Mheshimiwa Waziri na Wataalam wake, kumbe kile kinachopatikana kwenda kwenye ile jamii cha ujirani mwema ni kidogo kutokana na ile Bajeti ya *KINAPA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna taarifa kwamba, kule Japan wenzetu ili waweze kupata nyama nzuri ya ng'ombe, yule ng'ombe kabla hajachinjwa anapigiwa muziki hivi, *to get a tender meat* ni kumbembeleza yule ng'ombe. Sisi wafugaji ukitaka upate maziwa mengi na mazuri, unamlisha yule ng'ombe unampa na pumba ili akuachie yale maziwa yawe mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama sisi pale Mlima Kilimanjaro wanavuna tu, kinachorudi kwenye ile jamii ni kidogo *peanut.* Bahati mbaya yule ng'ombe anaweza akashtuka akatingisha ndoo kwa mguu na yale maziwa akayamwaga. Sasa mimi ningeomba tusije tukafika huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba hapa ni kile kinachoenda *TANAPA* kwa maana ya ujirani mwema. Sasa hivi Wizara ikae ijipange vizuri ni suala hilo hilo la ujirani mwema, lakini kiongezwe na kiende moja kwa moja kwenye zile Halmashauri au Wilaya zinazozunguka ule Mlima Kilimanjaro ili tuweze kuwaambia wananchi wetu hilo darasa wanaloliona hapo, lile daraja wanaloliona pale ni mapato yanayotokana na Mlima wetu Kilimanjaro. Moto ukizuka Wananchi wa Kilimanjaro ndio wanaokwenda kuuzima kwa kushirikiana na wale watu waliopo pale wa Wanyamapori. Matatizo yote yanayotokea; mmomonyoko mkubwa wa ardhi kutokana labda na mvua zikinyesha ni Wananchi wa Kilimanjaro ndio wanaoathirika na *erosion* na mambo mengi yanayotokana au madhara kwa upande mwingine wa hali ya hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Waziri, hili suala alizingatie kwa kushirikiana na wataalam wake, kile kinachoenda kwenye ujirani mwema, mambo ya *co-operate social responsibility* naomba kile kiasi kiongezwe ili kiweze kuwafikia wale wananchi na kipelekwe moja kwa moja kwenye Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ule utaratibu uliopo sasa hivi ni mgumu kidogo na ni vigumu sana kuwaeleza wananchi kwamba, hiki ndicho kilichopatikana kutokana na mapato ya Mlima Kilimanjaro. Sawa sawa na mahali pengine, wenzetu pale kwenye uwindaji nako wanapewa. Kwa hiyo na sisi tungeomba kile kiasi kiweze kuwafikia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mlima huo wa Kilimanjaro, mojawapo ni njia mpya ambazo tunatarajia zifunguliwe, lakini kuna njia moja ya kutoka kwa Sadala kupitia Masama Mula kuelekea Nure, hii njia ni ya siku nyingi sana, imekuwa ikitumika tangu enzi za babu zetu. Kuna mahali huko ndani ya Mlima palikuwa panafanyika soko panaitwa Kisingireni. Nilizungumza hapa mara ya mwisho, kuna jani ukilishika mvua inanyesha watu wakacheka, lakini karibuni muweze kushuhudia hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ningeomba tuendelee kuutumia ule Mlima Kilimanjaro vizuri zaidi; *Cultural Tourism*, tunaweza tukawa na *None Summit Tourism of Mount* Kilimanjaro, watu kwenda kufurahia tu hali ile ya uoto wa asili inawezekana sana. Taifa likapata na wale wananchi wanaozunguka ule Mlima Kilimanjaro nao kwa njia moja au nyingine, wakaendelea kufaidika ili waendelee kuwa na moyo mzuri wa kuutunza ule Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru Naibu Waziri, lile zoezi ambalo walikuwa wameongeza ile mipaka, alinithibitishia kwamba, lilisitishwa na mazungumzo yanaendelea kufanyika, kufanya tathmini na ili tuweze kuwa na ujirani mwema zaidi. Ningeomba yale maeneo yasiendelee kuongezwa kwa sababu Kilimanjaro tunao uhaba mkubwa wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba niishie hapo kwa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuna kila hali na sababu ya kuibua vivutio vingi vya utalii ndani ya Majimbo yetu. Sisi wenyewe tuweke taratibu nzuri za kuvisimamia kiasi kwamba, tukiomba ushirikiano kutoka Wizarani, wananchi wetu wazidi kunufaika na hivi vitu vyote ambavyo Mwenyezi Mungu ametujalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe wale wataalam basi uzalendo uwe ni muhimu zaidi, waikumbuke nchi yetu na waogope historia ya kuja kuwahukumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na nazidi kuwashukuru sana Wananchi wangu wa kule Hai. Nitaendelea kuwawakilisha vizuri, kuwatumikia kwa uaminifu na uadilifu wa hali ya juu na nizidi kuomba hii Wizara ituangalie ili huyo ng’ombe asije akapiga teke yale maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fuya Kimbita ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, atafuatiwa na Mheshimiwa Kaika Telele na Mheshimiwa Diana Chilolo ajiandae.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie kidogo tu. Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunifikisha hapa na kuweza kupata nafasi hii.

Kwanza, nataka nianze kwa kuwapa pole Wizara kwa kufiwa na wenzao ambao ni wafanyakazi hodari katika ajali ya ndege; poleni sana.

Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii. Tatu, shukrani zangu zinakwenda kwa *TANAPA*, wametusaidia sana wametujengea Kituo cha Afya cha Gomela – Kisaki, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Vilevile nawashukuru *GTZ* kwa niaba ya Ujerumani na *Selous Conservation Programme*, ambao wametusaidia nao katika zahanati pale Kisaki Stesheni na wametusaidia sana katika mambo mengi tu, tunashirikiana nao vizuri sana.

Baada ya kushukuru huko nina swali nataka niulize; ndani ya *Selous* kunafanyika utafiti mkubwa sana kila wakati unapata wataalam wanakwenda kufanya utafiti, lakini unaona wanaingia tu na kutoka mpaka sasa hatujui wanafanya utafiti kitu gani? Nchi hii inafaidika vipi na utafiti ule au wanabeba utafiti ule na kwenda nao nyumbani kwao, hili tungependa tuelezwe? *(Makofi)*

Pamoja na hilo ndani ya *Selous* pale hasa Matambwe, pana kiwanja cha ndege na mara nyingine ndege zinakwama katika kiwanja kile. Ningeomba Wizara watie lami kile kiwanja, kwa sababu watalii wakati wa masika wanashindwa kupita huku kwenye njia kutoka Morogoro kwenda Kisaki. Kwa hiyo, wangeweza kuwa wanatua pale. Ni rahisi kwa watu wengine wazee wanaendesha muda mrefu sana kutoka Morogoro mpaka Kisaki ni kilomita 194 kwa barabara mbaya kama hizi zetu, tunawavunja moyo watalii kwenda kule. Kwa hiyo, ingekuwa vizuri kama wangeweza kuruka kwenda Matambwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nataka niingie kwenye matatizo kuhusu kero za wananchi. Kwanza, uvunaji wa misitu holela halafu tunapakaziwa Waluguru. Watu wanakuja na vibali kutoka Wizarani, Mkoani, lakini huku sisi ambao tunatunza misitu ile haturuhusiwi hata kuwauliza. Mimi natoka Kata ya Selembala, Tarafa ya Mvuha, Jimbo la Morogoro Kusini, nimezuia sio kwa niaba ya Serikali, kwa niaba yetu sisi wenyewe nimezuia mtu yeyote kuja kuvuna mpingo. Kuna msitu wa mpingo kule mimi nimezaliwa nimeukuta. Mtu mmoja alikuja amevuna malori matatu, bahati mbaya wakati mimi nilikuwa nakwenda kule nilikutana naye. Sisi ni wawindaji, nilichofanya ni kupiga ukelele tu mwizi wa mali, zilitoka gobole zaidi ya mia kuzuia mali ile na tulitaka atueleze amepata kibali wapi cha kuvuna mpingo. Tulimwambia shusha mali yote hapa ukamlete aliyekupa kibali mpaka kesho hajarudi.

Kwa hiyo, tulijua ni mwizi tu. Bila ya kuendelea, tumeona mradi imevunjwa mali hii ni mali ya Wana-Selembala tukauza tukajenga sekondari. Hivi vibali vya kupatikana, watu wanaleta tu vibali vyao vya miti, mbao na miti mingine mikubwa mikubwa, Milima ya Uluguru ile yote inamalizwa sio na Waluguru inakuja inafyekwa na watu waliopata vibali hatujui vinatoka wapi! Tafadhali sana, tunaomba tushirikiane uvunaji wa misitu lazima tushirikiane. Watu wasije tu kuvuna misitu kwa sababu wanaiona, wasione vinaelea vimeundwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nilitaka kuzungumzia *open hunting area* ya Msitu wa Mkurazi. Kuanzia Julai 1 mpaka Desemba 31 katika msitu ule ukipita usiku ukipona bahati yako; ni bunduki zinatoka Dar es Salaam kila mahali wanyama wanawindwa kama vile wapo kwenye vita. Ukiuliza wanasema hii *open area* tunawinda hapa mzee tumeruhusiwa na kweli wana leseni za kuwinda. Lakini leseni nyingine inatoka wapi; inatoka Kisarawe, inatoka Dar es Salaam, mimi nikasema mambo gani haya?

Hebu tunaomba tujue ile *open area* ya Msitu wa Mkurazi ipo katikati ya Vijiji vya Ngerengere, Tununguo, Selembala na Mkurazi kwenyewe; *control* yake ikoje? Wanyama wanawindwa kama vile ni kisasi, kupona kwao ni kuvuka Mto Ruvu kuingia *Selous.* Sasa sisi hatujui hii maana yake nini na tumeomba pale pawe mahali pa *reserve*, kwa sababu ya utalii wa kupiga picha. Kila tunapoomba, tunaambiwa hapana hii ni *open hunting area*, sasa nani anaamua, mnatusaidiaje kuwatunza wanyama hawa? Hili naomba jibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni gumu kabisa linahusu vijiji 22 vinavyozunguka *Selous.* Ukianzia Magogoni, Mvuha, Dutumi, Mngazi, Dakawa, Kisaki huko kote kuna vijiji hivyo vinalinda *Selous.* Wanaopewa nafasi ya kuwinda hizi *hunting blocks* wanakuja na karatasi wakisema mimi nimepata hiyo *hunting block*. Matokeo yake, thamani ya sisi wananchi ambao tunakaa kwenye kulinda hawa wanyama ni ndogo kwa sababu hatuhusiki na hao wanaokuja. Bahati nzuri, nimezungumza na Mheshimiwa Waziri, naomba niwaambie wananchi wa vijiji vile 22 na chama chao cha Jukumu kwamba, Mheshimiwa Waziri, amekubali kuja na mimi mguu kwa mguu tuzungumze na wananchi wale na tuone jinsi gani malalamiko yenu yanaweza kumalizwa na Wizara. Kwa hiyo, sina haja ya kuyataja hapa kwa sababu Waziri amekubali kuja. Tulishazungumza kabla ya hotuba hii, basi nina hakika atakuja kwangu kwanza baadaye atafuata pengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwangu utalii hautangazwi sana, Kaskazini ya *Selous* bado utalii haujatangazwa sana na hii ni sababu ya hali halisi ya ugumu wa njia. Watu walikuwa ni vigumu sana kufika Kisaki, kuna mabonde na madaraja mengi sana Morogoro mnajua tuna mito mingi sana, kwa hiyo, tunatangaza polepole. Naishukuru Wizara inajitahidi sana, lakini kuna kitu kimoja, sasa hivi kule watalii wanakifuata Kisaki kuna *hot water spring* panaitwa Majimoto. Wanakuja, sisi tumeizoea ile lakini wao wanakuja pale wengi tu wazee wanakoga, najua maana yake nini wao wanatumia ile kama dawa lakini wanakuja pale wanaondoka tu. Pana mahali unakaa unaangalia wanyama wakisafiri kutoka Mikumi kuingia *Selous* na kutoka *Selous* kwenda Mikumi, pale Kisaki; *Selous* na Mikumi zimekutana, lakini huwezi kuona mahali popote inatajwa, wala huwezi kuona tunashughulikia habari hii, wanaona kitu cha kawaida tu labda hawataki tu basi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanyama wa *Selous* wamezoea kuangalia watu badala ya watu kuwaangalia wanyama. Kwa sababu kuna amani, hawapigwi mle ndani ya *Selous*, unaweza ukapita ukapishana na tembo tu ili mradi wewe humsumbui. Sasa wanakuja wanageuza pori lile wengine kupiga picha wanyama bila ya ruhusa. Wanapiga picha hawa wanyama, maana yake nawauliza wale watu jamani mmepata kibali cha kupiga picha, kibali cha nini sisi tumeingia huku.

Pili, kwa sababu tuko mbali sana na Makao Makuu yetu ya Wilaya, yapo kilomita 194 Morogoro Mjini mpaka ukiingia huko, lakini sasa limezuka tatizo moja hili ndilo nataka nilizungumzie hasa simba. Kijiji cha Dutumi kimeingiwa na woga wa simba wa ajabu sana, simba wala watu. Hivi ninavyozungumza, saa hizi Dutumi wamekwishaingia

kwenye nyumba zao kulala, hakuna nafasi ya kutembea simba wanatawala. Wamekwisha kula watu wanne katika muda mfupi huu wa kiangazi, simba hawa wanatawala kuanzia Mvuha, Dutumi, Mngazi, Bwakila mpaka Kisaki. Tunaomba msaada haraka sana, kutawaliwa na mnyama wa porini ni kitu kibaya sana. Kuna dharura ambazo huwezi kuzifanya kwa sababu nje pana samba, hujui anawinda saa ngapi na anamwinda nani. Tunaomba msaada sana tena wa haraka sana. Tunacho chama pale kinaitwa Jukumu cha *WMA* lakini tatizo pamoja kwamba, wanazo bunduki, risasi ni vigumu kupata wale watu. Ama tuletewe Bwana Nyama au wapewe wale vijana risasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ni Mto Ruvu. Mto Ruvu na Mto Mvuha vinakutana. Mito miwili hii ina mamba sana. Mamba ni wengi sana, tunaomba mtoe kibali wavunwe kwa sababu kesi za kuliwa watu na mamba ni nyingi mno. Bahati mbaya alikuja Bwana Nyama mmoja pale, Afisa wanyamapori kupiga mamba alikuja na risasi kumi, tulikuwa na matumaini kwamba angalau atawapiga wawili; yule ni tofauti na huyu wa Mheshimiwa Mkapa, yule wangu ilikuwa kila akipiga anapiga porini, risasi kumi amepoteza hata mamba mmoja hakumpata.

**NAIBU SPIKA:** Alikuwa mwanamume?

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mwanamume huyo mama, huyo mwanamume ambaye hana shabaha, bahati nzuri niseme nilikuwepo. Mimi ni muwindaji, ninazo bunduki zangu na huyu mamba alikuwa anashambulia watu kweli kweli. Kwa hiyo, nikamwomba ruhusa kwamba mimi sina kibali cha kupiga sasa wewe Afisa Wanyamapori uko hapa niruhusu nipige, unahitaji risasi moja tu ya 458 kupiga mamba anapinduka.

Sasa yule mjomba amepiga kumi watu wanashangaa kabisa huyu ni afisa huyu! Sasa sisi tumesema labda amesahau siku nyingi, tuleteeni maafisa wenye shabaha kama yule mama wa Mheshimiwa Mkapa kule, kwa sababu kupiga mamba mara nyingine kunatiwa woga au samba, lazima umkabili ndio umpige huwezi kumwagizia. Naomba sana, narudia; Wizara naomba sana mtuletee haraka kabisa tatizo la simba mla watu Dutumi, yupo Dutumi anatoka *Selous* anaingia kwenye Kijiji cha Dutumi ndiyo atembee, anaunguruma saa moja tu jioni. Na hili sio mchezo ni tishio kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maliasili na Utalii, kama ambavyo imewasilishwa katika Bunge hili. Awali ya yote, napenda pia nitumie nafasi hii, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Wataalam wake wote wa Wizara na Mashirika ambayo yapo chini ya Wizara hii ya Maliasili na Utalii, kwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri kuandaa bajeti hii na hatimaye kufika mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Vilevile niungane na wenzangu kutoa rambirambi kwa Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara, kwa Maafisa Waandamizi waliofariki katika ajali ya ndege hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tishio la kutoweka kwa wanyamapori duniani, inategemea binadamu mwenyewe, lakini binadamu huyo huyo anaweza akawa mhifadhi mzuri akawahifadhi wanyama wakaendelea kuwepo duniani. Sisi tunaokaa katika maeneo ya wanyamapori, tatizo letu kubwa na tishio letu kubwa kwa wanyamapori ni watu wanaoitwa Wasomali. Watu hawa ni hatari sana kwa wanyamapori, kwa watalii na kwa kila kitu. Watu pekee ambao wanaweza wakakabiliana na hawa Wasomali na naomba kwa sababu nimesikia kilio katika maeneo mengi ya simba wala watu, kwa ndugu yangu Mkapa hapa, kwa ndugu Lwanji huko karibu kila mahali. Tufike mahali, vyombo vinavyohusika waajiri Watanzania wenye asili ya Kimasai, Wakurya wa kule Tarime na ndugu zangu Wahehe, hawa ni majasiri sana wakipita maeneo yale simba wataingia kwenye mashimo wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotakiwa hapa ni kuwapa tu mafunzo yanayotakiwa ya kiaskari ukakamavu, lakini ujasiri makabila hayo wanayo. Ukiangalia sana Watanzania wa jamii ya Kimasai, wamekuwa ni wahifadhi wa muda mrefu sana. Ukiangalia maeneo ambayo wanyamapori wanapatikana sasa hivi ni maeneo ambayo kabila hilo limewahi kukaa au linaendelea kukaa hadi sasa. Kule Serengeti, baadaye imekuja kuwa hifadhi maarufu ya Taifa, yalikuwa ni maeneo kwa kweli yaliyokaliwa na jamii hii lakini Wakoloni walifanya kazi kubwa sana ya *negotiation* ya miaka zaidi 13, kuwashawishi waweze kuondoka na kwenda maeneo ya Ngorongoro. Ilifanyika hivyo na tupo Ngorongoro hadi sasa ni maeneo yetu tumepewa badala ya Serengeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, wahifadhi wa siku hizi mimi nawashangaa sana, wanapojaribu kutenga mifugo na wanyamapori. Mifugo na wanyamapori kwa kweli hawana mgogoro wanaelewana vizuri tu. Tunakutana huko kwenye nyasi na mifugo yetu jioni tunarejea nyumbani tunakutana tena kesho, hakuna matatizo. Kutokana labda na taratibu za uhifadhi wa siku hizi, basi wanyamapori na mifugo wanaelekea kutengwa. Nawapongeza watu wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa kuwa na hili wazo la kununua helikopta ambayo inaweza kudhibiti suala zima la ujangili katika maeneo ya wanyamapori. Vilevile ikasaidia kudhibiti wizi wa mifugo kutoka kwa watani zetu Wasukuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie maeneo ya uhifadhi wa ardhi oevu, yaani *Wetlands Lake Natron. Lake Natron* umaarufu wake ni wale *lesser flamingo*. Zaidi ya *lesser flamingo, Lake Natron* haina umaarufu wowote. Ziwa hili halijatusaidia sana kimapato na badala yake, linawasaidia sana wenzetu wa nchi jirani pale Kenya. Nilishazungumza wakati uliopita, nikichangia Wizara hii hii kwamba, kuna *Lodge* moja kubwa nzuri ipo upande wa Kenya wanaiita *Shombole Lodge* na mapato yao makubwa yanatokana na Ziwa hili. Sisi Watanzania vijiji vyangu vya Pininyi, Moniki, Engalisero na kule kwa ndugu yangu, Mheshimiwa Lekule, hatunufaiki chochote na ziwa hili. Hata wanaposema kwamba, tutajenga kiwanda, binafsi sikubaliani nao napinga hiyo hali moja kwa moja, pamoja na kwamba naambiwa itawaajiri watu; kwa nini wewe hutaki watu

wako waajiriwe? Kama ni Watanzania wenzangu waliokwenda shule, hiyo ni sawa sawa, lakini kama ni ndugu zangu Wamasai ambao elimu ni kidogo wataishia kuwa walinzi, haitusaidii nafuu tukaendelea kuangalia Ziwa hili liendelee kutunufaisha kiutalii badala ya kiwanda ambacho kinakusudiwa kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Programu ya Ujirani Mwema inayoendeshwa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, lakini ningesema kwamba, hiyo Programu ni nzuri sana. Wameelekeza nguvu sana kwa upande wa Karatu na hii ni kwa sababu ya *Northern Island Forest Reserve*, ambayo watu wabaya wakiingia ndani ya msitu ule ni rahisi kuingia Hifadhi ya Ngorongoro na kuingia kwenye *crater* na kutuletea balaa kwa wanyamapori.

Sasa nilikuwa nataka niwaombe kwamba, huu ujirani mwema waupanue waelekee maeneo ya Malambo, Piyaya, sehemu za Esilalei, Arash, Masusu, Engaresevo sehemu za Pininyi, waweze kusaidia Miradi ya Wananchi katika maeneo yale. Kwa sababu watu wabaya na wanyamapori wanaweza wakatoka pia mbali na sio lazima watoke karibu na maeneo yale. Wasaidie Miradi ya Wananchi kama kujenga shule, wanafanya hivyo lakini kubwa zaidi wajenge mabwawa kwa ajili ya wanyamapori na kwa ajili ya mifugo mbugani; hii itawasaidia sana kuona Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro inakuwa na faida kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Oldonyosambu imetajwa katika ukurasa wa 20 wa hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri, nimefurahi kwamba, wametenga shilingi bilioni 1.1 katika mwaka huu wa fedha kwa ajili ya miundombinu ya barabara, shule za msingi, zahanati, kituo cha polisi na kuweka maji; wamefanya vizuri. Huu ni mwaka kama wa tatu au wa nne, fedha zinatengwa lakini kazi inakwenda kwa kasi ndogo sana. Ningependa kuwaomba waongeze kasi, kwa sababu sasa hili limezungumzwa Bungeni, katika bajeti ijayo watupe taarifa kwamba, miundombinu hii yote imekamilika katika eneo lile.

Hawa ni wale watu ambao wamehamishwa au wamekwenda kwa hiari yao wenyewe kutoka Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, kwa sababu ni eneo dogo kwenda katika eneo la Oldonyosambu ambalo wametafutiwa na Serikali. Tutajenga kituo kikubwa cha Polisi kwa sababu ni *corridor* kubwa ya kwenda nchi ya Kenya na mambo yasiyo mazuri yanaweza yakapitishwa katika *corridor* hiyo. Kwa hiyo, tunahitaji Kituo cha Polisi kianze kujengwa haraka kadiri inavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, utalii wa ndani; Watanzania bado hatujachangamka sana katika kufanya utalii wa ndani. Mimi sijui hasa ni kwa nini, labda *rates* za kuingia maeneo ya wanyamapori zipo juu lakini kwa Ngorongoro ni shilingi 1,500, lakini umaskini wa Watanzania labda unawakwamisha. Nawapongeza, juzi nilikuwa kwenye Maonyesho ya Sabasaba huko Dar es Salaam, banda lile la Wizara ya Maliasili na Utalii wamepata watu wengi, wamevunja rekodi kabisa. Hii inaonyesha kwamba, wananchi wana kiu ya kufanya utalii wa ndani, lakini kutokana na viwango; maeneo yetu hatujawahamasisha vya kutosha, hatujawaeleza taratibu nzima za kwenda kwenye mbuga wanasita. Nitumie nafasi hii, niwaalike Mamlaka Hifadhi ya Ngorongoro kwa kweli sio

gharama kiasi hicho na Watanzania waweze kujenga utamaduni wa kutembea. Unaongeza maisha yako, ukitoka kwenye eneo la *pressure* ya kazi kila siku ukaenda maeneo mengine kupumzika, unakuwa kijana zaidi miaka kumi *younger* kuliko ungeendelea kukaa mahali pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Makampuni ya Kitalii yaliyoko Ngorongoro na hasa sehemu za Loliondo zaidi ya 17. Makampuni yote yaliingia kwa kufanya mikataba na vijiji na wanalipa kitu kidogo kwa vijiji lakini sijui ni kiasi gani wanalipa kwa Taifa hili kupitia Wizara hii. Nilikuwa nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri kwanza, nimpongeze sana kwa sababu mara tu baada ya kuteuliwa katika maeneo machache sana ambayo amefika ni Wilaya ya Ngorongoro, ambayo ni viongozi wachache sana wanafika Makao Makuu ya Wilaya. Nampongeza sana na hili tulimweleza na akatuambia kwamba, hakuna mtu atakayesumbuliwa katika eneo lake; si Makampuni haya wala si wenyeji ilimradi tukae chini tuweze kutengeneza utaratibu wa namna ya kuishi pamoja na kusaidiana kimapato katika eneo hilo. Namwomba sasa amsaidie Mheshimiwa *DC* ameanza kuwachambua kwa kufanya utafiti wa Makampuni haya ili kujua ni akina nani wana leseni halali na wanalipa ushuru halali kwa Serikali na kwa hiyo wana uhalali wa kuendelea kukaa huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kidogo lango la Ngorongoro. Lango hili wanaliita *Lodiwale Gate;* ni eneo la kuingia na kutoka katika Hifadhi ya Ngorongoro. Wanaingia watu na wanaingiza magari ndani ya Ngorongoro na kwenda Loliondo, Musoma na Mwanza, lakini pia kutoka kuja Arusha na maeneo mengine. Sasa kuna *entry fees* za kuingia humu. *Entry fees* ni kati ya shilingi 20,000 au 25,000 kwa magari madogo ni 10,000. Magari ya kwenda Loliondo ambako ni Wilaya hiyo hiyo, sioni kwa nini waendelee kuyatoza ushuru wa magari yale kwa sababu ni mabasi ya kupeleka watu na kupeleka bidhaa za madukani na kwenye soko.

Sasa ukiendelea kuwatoza hawa, basi maana yake bidhaa zinapanda kule madukani na katika soko na maisha ya wananchi yanakuwa ni gharama kubwa zaidi. Kwa hiyo, ningependa kwa sababu ni mabasi machache na malori machache hayazidi 12, haiwezi kuathiri bajeti ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, naomba ushuru huo ufutwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka wakati fulani tulipandisha ushuru kwa sababu magari yanayoingia yanatuharibia barabara. Magari ya kwenda Musoma, fuso la tani saba lakini linabeba mzigo wa tani kumi linatuharibia barabara, kwa hiyo tukapandisha ku-*discourage* hiyo.

Zilipigwa kelele sana na ni kelele za haki kwa Wabunge wa Musoma, Mwanza kwamba vitu vimepanda bei. Kwa hiyo, tukashusha tukaja 50,000 tukashusha zaidi na sasa 25,000. Naomba kwa maana ya mabasi haya na malori yanayopeleka bidhaa Loliondo na Sale ndani ya Wilaya hiyo hiyo, hawa wafutiwe moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho hoteli zinazojengwa katika Hifadhi ya Ngorongoro, nashukuru kwamba, kwa *realm* ya Ngorongoro hakuna hoteli tena za kuendelea kujengwa. Kwa maeneo mengine, Mamlaka Hifadhi ya Ngorongoro imeidhinisha hoteli na *lodges* katika maeneo fulani fulani. Lakini hayo yanakwenda kwa kasi zaidi kuliko sisi tunavyotaka kujenga shule za sekondari, kwa mfano, tunapata matatizo makubwa sana. Mara hii *EIA* ichukue muda mrefu, tunatenga fedha kila mwaka zinarudi hii *EIA* haijakamilika. Sasa hivi nalishukuru Baraza la Mazingira la Taifa wametuelewa na sasa tunaweza kuendelea, lakini wametuchelewesha muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii ili na mimi niweze kutoa kilio changu kwa niaba ya Watanzania na hususan Wanasingida kupitia Bajeti hii ya Maliasili na Utalii. Kabla sijaingia kwenye kilio naomba nianze na pongezi. *(Makofi)*

Kwanza nimpongeze Mheshimiwa William Ngeleja, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Adam Malima, pamoja na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri waliyoifanya jana kwa kutupatia umeme. Tumepata umeme Ihanja, Sepuka na Mgongo. Natoa pongezi hizi kwa niaba yangu mwenyewe na kwa niaba ya Wabunge wa Majimbo na wananchi wa maeneo haya na Mkoa wa Singida kwa ujumla. Nawapongeza sana na nawatakia utekelezaji mwema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo sasa niingie kwenye Wizara ambayo tunaijadili leo. Nianze kwa kumpongeza dada yangu na rafiki yangu, Waziri, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Naibu Waziri mwanangu Mheshimiwa Ezekiel Maige, Katibu Mkuu rafiki yangu Blandina Nyoni na watendaji wote walioshiriki katika kuandaa Bajeti hii. Kwa kweli Bajeti ni nzuri. Imeainisha maeneo yote na jinsi watakavyoitekeleza, nawatakia utekelezaji mwema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo naingia kwenye matatizo, naanza na Simba wanaokula watu Singida. Singida tuna kilio, kilio wala si kidogo ni kikubwa. Kaka yangu Mheshimiwa Paul Lwanji amesema sijui huyo simba aje humu humu ndani ya Bunge. Sasa mimi nasema, sijui mimi na mdogo wangu Mheshimiwa Martha Mlata tulie humu humu ndani ndiyo muone Wanasingida tunaathirika, tunakwisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni afadhali binadamu augue afe umzike unaona hivi hivi kiwili wili chake. Msiba wa kuliwa na Simba maiti haionekani. Maiti hizo zinatambulika kwa kupitia nguo alizovaa. Miili huwa imeshaliwa, hakuna nyama wala nini. Mnataka tuseme nini ili Serikali itusikie. Wanasingida tunakwisha, simba wametishia maisha ya binadamu, sasa hivi watu kusafiri kwa miguu, kwa baiskeli au

pikipiki wanashindwa, kwenda shambani wanashindwa. Ndugu zangu Serikali ya Wilaya na Mkoa zimejitahidi mpaka watu binafsi wamejitolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, yupo kijana wetu anaitwa Ndovu, mtoto wa Marehemu Chifu Senge. Bahati nzuri Chifu huyu alikuwa anafuga simba zamani. Kwa hiyo, tukamwomba labda atatusaidia, kajitolea baba wa watu lakini mpaka sasa hivi juhudi hizi hazijazaa matunda. Sasa nakileta kilio kwa Serikali, tupeni msaada, tuungeni mkono. Watendaji wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu, hawana vitendea kazi. Hivi ulisikia simba wanasakwa na watendaji wa vijiji, watendaji wa kata au maafisa tarafa wanaoenda kwa miguu hawana silaha?

Mheshimiwa Naibu Spika, tupeni silaha, tupeni risasi, tupeni gari lizunguke kote tarafa zote ambazo zimeingiliwa na simba hawa na sio hiyo tu. Tunaomba Askari Wanyamapori, Manyoni Wilaya nzima kuna askari mmoja tena kazeeka karibu anastaafu. Wilaya ya Singida haina kabisa. Tunaomba tupewe Askari Wanyamapori haraka ili kunusuru maisha ya binadamu. Tarafa ya Itigi tupate mmoja, Konko tupate mmoja, Sepuka tupate mmoja, Ikungi tupate mmoja na Ihanja tupate askari mmoja. Ninaomba sana tukipata hawa askari watatusaidia jamani. Haya ni maafa lazima tushirikiane jamani. Wizara lazima muingilie kati hakuna mjanja kwa hili na hili ni tatizo na ni maafa tuyape kipaumbele kama maafa mengine mnavyofanya. Kwa nini Wanasingida tupige kelele humu ndani kila siku?

Mheshimiwa Naibu Spika, alishasema Mheshimiwa Mohamed Missanga siku moja hapa, haya mwenzangu Mheshimiwa Paul Lwanji kapiga kelele humu ndani, yaani imekuwa kama wimbo wa Taifa, Singida kwa nini? Namalizia hapo ninaomba sana sana tuletewe Askari Wanyamapori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo nizungumzie kuhusu kifuta jasho. Ndugu zangu ni kweli simba, ndovu wanaua watu, wanaharibu mashamba yetu na tunashukuru Serikali imetizama hili, kidogo imeongeza. Eti binadamu anapewa kifuta jasho shilingi laki mbili na mazao lakini moja. Hivi kwa nini gharama ya shamba na mazao yaliyoharibiwa na ndovu yasifanyiwe tathimini yameharibiwa kiasi gani ili fidia hiyo itoke ilingane na gharama. Vifuta jasho vinasaidia nini kwa mtu aliyeathirika kwa shamba zima la ekari kumi limekwenda?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba vifuta jasho vilingane na uharibifu. Binadamu kafa, tegemeo la familia, baba mwenye nyumba kafa leo unapeleka rambirambi laki mbili unaipa familia. Mke kaacha na familia ya watoto sita, laki mbili itawafikisha wapi? Nguvu kazi ya familia imekwenda, tunaomba jambo hili litazamwe upya. Halina maslahi na watu. Halimfuti machozi mtu yeyote aliyepatwa na maafa haya. Tuangalie upya, tutafakari upya kama ni shamba mazao yameliwa iangaliwe shamba hilo limeliwa kiasi gani ili fidia ilingane na gharama hiyo na binadamu vivyo hivyo. Angalau tutoe kiwango ambacho familia hiyo itajisukumasuka wakati inamlilia marehemu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo niongelee juu ya asilimia ya mapori ya uwindaji. Tunashukuru kwamba Serikali inatoa asilimia 25 kwa ajili ya mapori ya uwindaji. Lakini vile vile nishukuru Idara ya Wanyamapori siku hizi inaainisha, kwa mwaka huu ni wanyama wangapi watawindwa na ni wa aina gani na ni wa gharama gani. Hivyo basi tunaomba orodha hiyo inayoainishwa na Maafisa Wanyapori wa Wizara yako tuletewe kwenye Halmashauri zetu za Wilaya ili tujue kiwango tunachopewa kinalingana na asilimia 25 ya wanyama waliovunwa? Tuna wasiwasi Hazina inatuzunguka, pesa tunazopewa hazilingani na asilimia 25. Wanyama wengi wanaovunwa wanagharama kubwa ili tufahamu takwimu hizo na kwenye Halmashauri zetu zifike. Tutapiga hesabu wenyewe, ili tujue asilimia 25 yetu ilitakiwa iwe shilingi ngapi, kama tumepunjwa tudai na zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongee kuhusu mbung'o. Hifadhi yetu ya Wanyama iliyoko kule Rungwa, Muhesi, Chaya na maeneo mengine kuna mbung'o. Hivi Wizara inajua hilo? Kama inajua imetafiti nini? Mbung'o hawa wanaathiri wanyama hao na binadamu? Tunaomba utafiti ufanyike na watafute tiba ya kutokomeza mbung'o anaweza akamalizwa tu ili wanyama wetu wakae kwa amani na wawindaji wanakokwenda kule wafanye kazi zao bila wasiwasi kwa sababu wadudu hawa wanaathiri maisha ya wanyama pamoja na binadamu wanaenda kuwinda huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ha hilo niongelee suala la asali. Katika Mikoa inayovuna asali kwa wingi ni pamoja na Singida, Manyoni hapa tuna asali nzuri sana. Asali ya nyuki wakubwa na nyuki wadogo, lakini wananchi wanahangaika, wanavuna asali nyingi ya kutosha soko lipo wapi? Tutafutieni soko, wananchi wanahitaji soko asali wanarundika madebe ndani ya nyumba yanafanya kazi gani? Tunaomba soko lipatikane ili hawa wanaofanya kazi ya kurina asali wapate manufaa na asali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo sasa nizungumzie magogo au mbao zinazokamatwa. Tunafahamu kwamba kuna magogo na mbao zinazokamatwa na Serikali. Lakini mbao hizi baada ya kukamatwa wanauziwa watu binafsi tu. Mimi naiomba Serikali, mbao hizi na magogo haya yanayokamatwa wauziwe wanavijiji na wananchi wanaoendelea na miradi ya maendeleo. Mbao hizi zijenge shule, zijenge zahanati na vituo vya afya pamoja na sekondari zetu tena wapewe bure kuliko kuwauzia wananchi wengine ambao wanabiashara zao tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naona kengele inakazana sasa na mimi naomba nikazane. Naomba nizungumzie kuhusu mipaka ya mapori ya uwindaji na ameongelea mwenzangu pale. Mipaka hii inahatarisha maisha ya wananchi kwa sababu ipo jirani sana na makazi ya watu kiasi kwamba inatishia maisha ya watu.

Naomba Wizara ifanye utafiti upya, iweke mipaka upya kama kuwahamisha hawa wananchi basi wahamishwe na wafidiwe ili tuwasaidie wasije wakaathirika na wanyama hawa wakali. Kwa kweli makazi yameingia karibu kabisa na mapori ya uwindaji. Katika suala nililolizungumzia kuhusu wanyama hawa wanaohatarisha maisha ya binadamu naomba Sheria itungwe ambayo itaweza kuainisha binadamu anayeliwa na simba au mnyama anafidiwa kiasi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niongelee vivutio vya utalii. Nafahamu wazi kwamba kuna vivutio vingi, kuna mbuga za wanyama na maeneo mengine mengi. Lakini naiomba Wizara haijainisha vya kutosha vivutio viko vingi sana. Hata Njombe Naibu Spika ninahakika una vivutio, na Singida vivutio tunavyo. Naiomba Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii ifanye utafiti upya na iainishe vivutio vya watalii na Singida vipo viainishwe. Kuna kipindi nilichangia hapa nikasema kwamba *center* ya Tanzania ni Singida na ni kivutio tosha. Wajerumani walishaweka alama, waleteni watalii waone. Singida, Manyoni kwa Mheshimiwa Kepteni John Chiligati, Kata ya Iseke kuna mwamba una sanamu ya Nabii Issa, njooni muone, waleteni watalii waone. Hata Iramba kuna Mlima wa Senkenke ni kivutio tosha waleteni watalii. Naomba mfanye utafiti upya ili vivutio vya utalii viongezeke. Msiendelee kuwapeleka maeneo hayo hayo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kuhusu mikakati ya kuvutia watalii. Katika kuvutia watalii ni pamoja na hoteli. Mikoa mingi haina hoteli, hivi Serikali ikiagiza tu kwa Wakuu wa Mikoa kwamba kila Mkoa sasa tunataka zijengwe hoteli tano, mbona mambo mengine mkiagiza yanafanyika? Mmeagiza shule za msingi tumejenga na za sekondari tumejenga. Agizeni na hoteli za kitalii zijengwe. Nina hakika Mikoa itatafuta Wawekezaji, watakuja kujenga na sisi tutapata vivutio vya kuwaletea watalii katika Mikoa yetu. Mgonjwa wakati mwingine unamlazimisha dawa ili apone; na sisi tuleteeni dawa. Kutuletea dawa ni pamoja na kutulazimisha kutengeneza au kujenga hoteli za kitalii ili watalii wanapokuja kwetu waweze kupata mahali pa kulala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba niongelee suala la posho, najua nitakera watu lakini muwe na amani kabisa. Posho za Wajumbe wa Bodi mbona kubwa sana? *(Makofi)*

Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *POC*, tunakagua hesabu za Mashirika ya Umma, posho mbona wanapata kubwa sana? Kwa nini Wajumbe wa Bodi walipane posho kubwa, hivi Serikali hii imepata uchumi mkubwa kiasi gani? Nchi maskini kama Tanzania unampa Mjumbe wa Bodi siku moja shilingi milioni moja wakati tunachangisha wananchi fedha za kujenga zahanati, vituo vya afya, shule na miradi mbalimbali ya maendeleo? *(Makofi)*

Naomba posho za Wajumbe wa Bodi za Mashirika ya Umma zitazamwe upya. Ziko Bodi nyingi tu *TANAPA*, Ngorongoro na nyingine zitazamwe upya. Tungeweza kujilipa hivyo kama uchumi wetu ungekuwa umeshainuka, uchumi wetu bado kabisa. Tusijipe fedha nyingi namna hiyo wakati Watanzania wanahangaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya naunga mkono hoja hii mia kwa mia nikitegemea kwamba hoja zangu zitajibiwa na Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana; na mimi pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili ya nafasi hii lakini pia kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Singida napenda kutoa pole nyingi sana kwa Wizara kwa msiba uliotokea kwa watendaji wenu. Sisi tunasema Bwana alitoa na Bwana ametwa jina lake

na libarikiwe. Lakini pia nitoe pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pomoja na watendaji wote kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya kuendeleza Wizara hii. Lakini nimpongeze Katibu Mkuu dada yangu Blandina Nyoni amekuwa ni mwanamke aliyejifunga mkanda kuhakikisha Wizara hii inasonga mbele, Mungu akubariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda nizungumzie kidogo kuhusu Mkoa wa Singoda katika sekta hii ya utalii. Wenzangu wameshazungumza lakini pia nami naomba nizungumze kwa kuweka mkazo kuhusu suala la wanyama waharibifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli suala hili limekuwa ni wimbo mwaka hadi mwaka kwa sababu kila mwaka Wabunge wa maeneo hayo wamekuwa wakileta kilio hicho hapa Bungeni kuililia Wizara lakini hakuna hatua madhubuti zinazochukuliwa. Hivyo naiomba sana Wizara hii ituangalie kwa jicho la huruma. Naomba Wabunge wote waungane nami kwa majonzi makubwa kwa kufikiria umekaa pale nyumbani wewe, mkeo na watoto wako halafu anakuja anachukuliwa mwanao, mkeo au wewe mwenye na simba. *(Makofi)*

Vile vile kulikuwa na vijana walikuwa wamepakiana kwenye baiskeli maeneo ya Isuna Mkiwa wametoka shule mwenzake akachukuliwa nyuma ya baiskeli na akashuhudia mwenzake akitafunwa na simba. Kwa kweli ni uchungu mkubwa sana. Tunaomba Wizara hii mtufikirie na mtuokoe. Wizara imekuwa na majibu ya kawaida sana kwa Wizara kusema kwamba watu wamefuata maeneo ya wanyama hawa. Lakini si kweli kwa sababu wanyama ndiyo wanaoingia kwenye makazi ya watu hawa. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara isiendelee kujibu kwamba watu wanafuata wanyama hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wenzangu wamezungumzia kuhusu fidia, ni kweli fidia imekuwa ni kama dharau au kebehi ya familia hizi ambazo zimekuwa zikiondokewa na wapendwa wao kwa uchungu mkubwa sana. Ninaiomba Wizara ilifikirie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la vijiji ambavyo viko pembezoni mwa hifadhi za wanyama hawa. Kuna kiwango cha fedha ambazo huwa zinatolewa kila mwaka. Lakini fedha hizi zimekuwa zikitolewa si kwa wakati muafaka na pia kidogo kidogo. Hivyo naiomba sana Wizara iliangalie suala hili ili hizo fedha zije kwa wakati na pia zije zikiwa zimekamilika na ikiwezekana *percent* hiyo iongezwe. *(Makofi)*

Naomba pia kuialika Wizara kutembelea pia Mkoa wa Singida kuja kuainisha vivutio ambavyo viko katika Mkoa wa Singida. Tuna vivutio vingi sana, tuna *Game Reserve* ambayo ipo Rungwa, tuna Mkesi pamoja na Kizinga. Lakini pia tuna mapango mazuri sana na michoro ambayo ipo Ndukuti na Mkarama na pia kuna Maboma ya Wajerumani kule, hivyo naiomba sana Wizara hii itilie mkazo ili kuisaidia Mkoa wa Singida katika hali ya kuinua uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nizungumzie suala la utangazaji wa utalii. Mimi naomba nizungumzie mwaka huu kulizinduliwa maonyesho ambayo yalikuwa

yakitangaza utalii wa Tanzania kule London, Uingereza. Kulikuwa kuna mabango ambayo yaliwekwa *Heathrow underground* pamoja na kwenye mabasi yanayozunguka katika mji ule. Kwa kweli imekuwa ni kivutio kikubwa sana na ninaamini ongezeko la utalii limetokana na matangazo haya. Lakini niliambiwa kwamba yatakuwa ni ya muda mfupi. *(Makofi)*

Naomba Wizara hii isikatishe matangazo haya angalau kwa mwaka iwe inafanya kwa kipindi kama ilivyofanya sasa ili kuongeza idadi ya watalii lakini iangalie ni muda gani ambao unaweza ukawa muafaka kwa ajili ya matangazo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitakuwa sio mwingi wa fadhila kama sitaweza kulizungumza suala hili hapa Bungeni na Wabunge wakaelewa pamoja na Wizara hii. Mwezi wa nne kulikuwa na mbio za *London Marathon.* Walikuwa vijana sita wa kimasai wakiongozwa na kapteni wao aliyejitambulisha kwa jina Isaya, kijana wa kimasai. Vijana hawa walifika Uingereza kuanzia *Kilimanjaro Internationa Airport* wakiwa wamevaa nguo zao za kimasai, mikuki pamoja na ngao zao. Walikuwa walivyo, ilikuwa ni kivutio kikubwa sana. Hata walipofika London kabla hawajafika ilitangazwa kwenye vyombo vyote vya habari ikiwemo *BBC.* Wageni wote na wenyeji wa London waliwasubiri kwa hamu sana na vijana hao walikuwa wakionyeshwa kwenye *TV* za *BBC* na nyingine zilizoko kule pamoja magazeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, walivutia sana na waliweza kuitangaza Tanzania hasa katika sekta hii ya utalii. Sote tunatambua kwamba kutangaza utalii ni gharama kubwa sana lakini vijana hawa ambao walikuwa wamefadhiliwa na Kampuni ya *Green Force* pamoja na *Britain Tanzania Society*. Hawa walifika kule kwa gharama zao wenyewe na waliweza kutangaza utalii huo pasipo kutumia senti hata moja ya Serikali. *(Makofi)*

Mimi nawaona vijana hawa ni mashujaa kwa sababu kila walipopita ilikuwa ni kivutio kikubwa sana. Hivyo naiomba Wizara hii ya Maliasili na Utalii iweze kuwatambua vijana hawa na kuwapongeza, na Mheshimiwa Naibu Spika ukiona ni vyema vijana hawa wafike hapa ili tupate kuwapongeza na tupate maelezo zaidi. Kijana huyu Isaya alikuwa akiongea Kiingereza japokuwa ni Mmasai aliyeishia darasa la pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la uwekezaji. Sera ya nchi yetu imekuwa ni ya uwekezaji. Mheshimiwa Rais wa nchi yetu amekuwa akizunguka kwenye Mataifa mbalimbali akiitangaza Tanzania na kuomba wawekezaji waweze kufika nchini ili waweze kuwekeza. Mimi naiomba sana Wizara hii pamoja na Watanzania wote tuilinde vizuri sera hii ili wawekezaji wanapofika nchini kwa sababu inakuza uchumi wa nchi yetu. Tutumie vizuri nafasi hii ambayo wawekezaji hawa wameweza kujitolea kufika hapa Tanzania na kuwekeza kwa ajili ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, yale makubaliano ambayo tunayaweka tusiyakiuke na pale yanapokuwa yamekiukwa basi tuchukuliane kwa upendo ili tuweze kurekebishana vizuri kwa sababu tunapokwenda kinyume na jinsi ambavyo tumeweka hakika kwamba

wawekezaji hawa ni wafanyabiashara wanazungumza na wafanyabiashara wengine tusije tukatangaza nchi yetu kinyume na jinsi tulivyotarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia suala la kiwanda cha magadi. Nasikitika sana Wizara ya Maliasili na Utalii inataka kuwafukuza ndege wa *Flamingo* waliopo katika Ziwa Natron kwa sababu wao wanataka kujenga kiwanda cha magadi pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndege hawa wamekuwa kwa muda mrefu pale na kivutio kikubwa, ndege wote wanaotoka katika pande zote za Afrika hata nje ya Afrika wamekuwa wakifika pale kwamba ndiyo mazalio yao. Ile chumvi chumvi iliyoko katika maji yale ile ndiyo chakula chao. Sasa mimi nauliza kujenga kile kiwanda pale Wizara haioni kwamba tayari inawafukuza wale ndege na kutokomea kabisa katika nchi yetu ambao wamekuwa ni kivutio kikubwa na wamekuwa wakiliingizia Taifa hili pato kubwa. Ni faida gani ambayo tunaweza tukaipata kwa sababu kiwanda unaweza ukajenga chumvi ikaisha pale, tukabaki na jengo na ndege wakawa wameondoka hawaoni kwamba itakuwa ni hasara kubwa na katu hatutaweza kuwarudisha ndege hao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sitakuwa na mengi zaidi lakini naomba haya yote ambayo nimeyazungumza nipatiwe majibu ili tuweze kwenda pamoja. *Otherwise* naishukuru sana Wizara hii na kuipongeza naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Kuhusu utaratibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 64.

Mheshimiwa Naibu Spika, inaonekana Wabunge wengi katika hoja hii wameongelea sana kuhusu kiwanda cha magadi kule Ziwa Natron. Laiti wenzetu wange-*refer* kwamba kiwanda kinajengwa kilometa ngapi kutoka Ziwa Natron, taarifa nilizonazo ni kwamba kiwanda kinajengwa kilometa 30 kutoka Ziwa Natron. Sasa hoja na picha ambayo inatolewa hapa kwa wananchi wa Tanzania na walioko nje ya Tanzania ni kana kwamba kiwanda kinajengwa kwenye Ziwa Natron. Lakini pia Watanzania tusiwe rahisi sana na kununua ajenda za jirani zetu kwa sababu ajenda hii si ya Watanzania. Ajenda hii ni ya jirani zetu na hawataki hata siku moja kusikia kwamba kiwanda kinajengwa hata kam ni kilometa 30 kutoka Ziwa Natron na hakina athari yoyote.

Kwa hiyo, upotoshaji huu pengine si mzuri sana. Pengine ukiongelea kuhusu kiwanda hiki useme pia hakijengwi kwenye mwambao wa Ziwa, ni kilometa karibu 30 ili angalau hata wale wenye dhamira nzuri na nchi yetu waweze kuelewa. Muda wote

nimesikia kana kwamba kiwanda kitajengwa kwenye mwambao wa Ziwa Natron ambapo si kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Kifungu ulichosoma ni kirefu kinasema; "(i) bila ya kuathiri ibara ya 100 ya Katiba inayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge" kina mambo mengi, ...hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli, hatazungumzia jambo ambalo haliko kwenye mjadala, hatazungumzia jambo lililoko Mahakamani, hatamtaja Rais, hatasema mwenendo wa Rais, hatasema vibaya au lugha ya matusi, hatatumia lugha ya matusi au nini. Sasa sidhani haya yote waliyozungumza yanawahusu. Kwa hiyo, mimi nilitegemea kwamba baada ya wao kuzungumza basi Waziri analipata hilo na atalijibu vizuri. Lakini tunashukuru kwa taarifa ila nafikiri maelezo mazuri itabidi Waziri mtoa hoja itabidi atoe. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Guido Sigonda. *(Makofi)*

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii nikiwa kama mzungumzaji wa mwisho katika kikao chetu cha leo. Lakini vile vile naomba niungane na wenzangu kwa pongezi zote za uhodari ambazo zimetolewa kwa Wizara hii hasa kwa viongozi vile vile pamoja na rambirambi. Mimi nipo pamoja na wao nisingependa nikarudia zile pongezi ambazo wenzangu wamezitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni-*declare interest* zangu kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maliasili na Utalii kwa hiyo, sikuwa na haja yoyote ya kusimama na kuanza kuzungumza kwa sababu yale yote maoni ambayo yametolewa na Kamati na mimi nilihusika.

Lakini baada ya kupitia hiki kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri nimeshawishika kwamba angalau nizungumze kwa sababu kuna mambo muhimu kabisa yaliyozungumzwa katika hotuba hii hayakuweza hata kidogo kugusia Wilaya ya Chunya na hasa Jimbo langu la Songwe. Ndicho kilichonishawishi kwamba nisimame, nizungumze. Maana yake ni kwamba nawaomba wajumbe wenzangu wasidhani kwamba pengine nimekiuka ule utaratibu ambao upo, lakini ni kutokana na hii hali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze ukurasa wa 7 mpaka wa 8 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri ambayo inazungumzia ulinzi wa maisha ya watu na mali. Wenzangu wamezungumza sana kuhusu hali ambayo inajitokeza katika maeneo yao, lakini mimi naomba nizungumzie la kwangu kwa uchungu kabisa linalotokana na hali inayosababisha vifo vinavyotokana na mamba katika eneo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, toka mwaka 2006, nimekuwa nikiomba Wizara pamoja na Serikali kwamba wajaribu kutafuta mbinu na namna ya kupunguza mamba katika eneo langu, eneo la Ziwa Rukwa. Nimeahidiwa hapa mwaka 2006 kwamba kuna kota ambayo ilikuwa imetolewa ya mamba 49, mwaka 2007 nimeahidiwa kwamba kuna kota nyingine

imetolewa, lakini mpaka hivi sasa ninavyozungumza ni mamba watano ndio ambao wameuwawa katika eneo langu. Sasa nakuja najiuliza hivi, hii kota ya mamba 1,500 mimi kwangu walikuwa wamepangiwa mamba watano? Maana inanipeleka mahali ambako kwa kweli hata sielewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu la kushangaza zaidi ni kwamba walikuja wakanishauri, Serikali ilinishauri kwamba katika kifuta jasho au kifuta machozi kwa wale walioathirika. Kuna wengine waliuawa, lakini wakaacha familia zao, kuna wengine walishambuliwa na ni vilema. Lakini mpaka hivi sasa hiyo ahadi ya kifuta machozi haijatekelezeka. Bado najiuliza kuna nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu la kusikitisha zaidi, mimi tarehe 13 Mei, nilikuwa na kikao cha wananchi katika eneo langu ambalo linazunguka lile Ziwa Rukwa upande wa Kusini mwa Ziwa. Alisimama mama mmoja akaulizia hili hili, akalalamika, hivi namna gani Serikali inatuonaje sisi ambao tunamalizwa na mamba! Mimi kwa sababu tayari nilikuwa na majibu ya Wizara, nililijibu kwamba Serikali inashughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekwenda kwenye mkutano mwingine wa hadhara, mama huyu alikuwepo, aliniambia hapana, naomba utueleze maana hapa tuko wengi sasa, utueleze hili tatizo la mamba litaisha lini? Nilijitahidi kumjibu kama Wizara ilivyokuwa inanielekeza. Naomba niseme kwamba huyu mama ni dada yangu mimi, dada mkubwa. Tarehe 16 wakati mimi nafanya mipango ya kuja huku, yule mama wakati anakwenda kuchota maji aliliwa na mamba!

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli hili ni jambo dogo, lakini kwa sasa naomba nipate maelezo lini watakuja, lini watajitahidi angalau kupunguza hawa mamba walioko katika eneo langu?

Mheshimiwa Naibu Spika, niende katika suala la utalii na hasa zaidi uwezeshaji na utangazaji wa vivutio vya malikale. Nimekuwa kila wakati ninapochangia kuhusu suala hili la utalii, huwa najitahidi sana kuelezea vivutio vilivyoko katika Wilaya ya Chunya na nikawaomba kwamba viongozi wa Wizara hii angalau waje wajaribu ku-*establish* hayo maeneo ambayo nayazungumza. Lakini ni miaka miwili na nusu sasa hivi tangu nimeingia, hakuna hata kiongozi yeyote ambaye amekuja. Naomba tu niwakumbushe kwamba vivutio vya malikale katika Jimbo la Songwe na Wilaya ya Chunya viko vingi sana. Nitatoa mifano michache tu, tunaweza tukawa na utalii wa utamaduni kwa kupitia Mlima Kwimba. Katika Mlima Kwimba kuna mapango ambayo kwa kweli yanavutia sana yaliyokuwa yanatumiwa na wazee wetu wa zamani. Pango moja ambalo linavutia zaidi ni lile pango la matambiko. Hivi tukijaribu kulieleza vizuri jinsi wananchi wa kule wanavyolitumia hili pango, hivi kweli haliwezi likawa kivuto cha utalii. Kwa sababu mimi nimejaribu kupita katika nchi zinazothamini maeneo kama hayo, yanawaingizia fedha nyingi sana. Lakini, kwa nini sisi tusithamini kitu kama hicho? Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri ameeleza yeye mwenyewe kwamba katika mipango yake kuna hiyo *cultural tourism*, nina imani kwamba na huku kwangu tajaribu kuja kuangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mlima mmoja, huo mlima *Chief* wetu nafikiri alikuwa wa pili, aliuona huo mlima umekaa vizuri kama kiti, kwa hiyo, akaamua kwamba mimi nataka niung'oe huu mlima niupeleke sehemu ile ambayo iko karibu na mimi. Huo Mlima ni Mlima Mwene na upo mpaka hivi sasa. Hivi kweli tukiwa na maelezo mazuri ya jinsi yule Mwene alivyo na alijaribu kuwashawishi wananchi wauchimbe ule mlima na lile eneo lipo, sehemu ambazo zilijaribiwa kuchimbwa ili kusudi aung'oe ule Mlima aupeleke huko. Sasa tukipata maelezo kweli mazuri, hayawezi yakawa ni kivutio kimojawapo!

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vile vile pango lingine ambalo machifu wetu wa zamani katika eneo hilo walikuwa wanalitumia kama ni sehemu ya kutolea hukumu ya kifo kwa mtu ambaye amekosa. Lile pango bado lipo. Tukilitengenezea maelezo mazuri kabisa, nafikiri lile pango linaweza likawa ni moja ya vivutio vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna jiwe ambalo lilikuwa linatumika na wazee wetu wa zamani wakati wanakwenda kupigana vita kwa ajili ya kunolea zile silaha zao kama mapanga, mikuki. Lile jiwe bado lipo na kwa sababu kilugha, kunoa tunaita *kupala* kwa hiyo lile jiwe limeitwa Kapalala kwa sababu ni mahali ambako walikuwa wananolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitafuta maelezo kwa kitu kama hiki, hivi kweli hakiwezi kikawa kivutio? Naomba kabisa tujitahidi tujaribu tu ili kusudi kuona, kuna maeneo mengi sana ambayo ni ya vivutio. Tuna fukwe. Kwa hiyo, naomba tu Wizara ijaribu kukubaliana na mimi kwamba waje wajaribu ku-*establish* maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwindaji wa kitalii, katika Jimbo langu tunayo kampuni moja tu ya *Dan Mac Ram Safari* ambayo ndiyo inashughulika na uwindaji wa kitalii. Naomba nielezee hapa na wananchi wa Jimbo hilo wanielewe kwamba hii kampuni kwa kweli inatusaidia sana kutokana na ile asilimia ambayo inatokana na uwindaji. Wametujengea shule, wametujengea zahanati na wanaendelea vile vile kutusaidia katika mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini eneo ambalo mwindaji huyu amepewa ni eneo kubwa sana. Wapo wananchi wazalendo ambao wamelitaka lile eneo angalau katika yale maeneo ambayo bado hayajaingiliwa, basi na wao wapate hiyo nafasi ili wawekeze katika suala la uwindaji wa kitalii. Mimi namuomba tu Waziri kwamba nikishamaliza hapa, nitajitahidi kumpa majina ya wale ambao wako tayari na ni wazalendo na wana uwezo wa kutimiza masharti yote ambayo yanahitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapanya katika eneo letu kwa kweli ni kitu ambacho kinasumbua sana kwa wakulima. Nashukuru Wizara kwamba imeonyesha kwamba kuna utafiti ambao unafanyika kwa ajili ya kuangamiza hayo mapanya. Lakini nasikia kwamba kuna mahali katika Tanzania hii, panya ni chakula! Sasa Wizara haiwezi ikashawishi hayo maeneo yakaja kwetu wakawinda hao panya! Halafu vile vile nasikia siku hizi kwamba panya anafanya kazi ya upelelezi, ya uchunguzi, hivi hao ndugu zetu ambao wana teknolojia hiyo, hawawezi wakaruhusiwa wakaja Jimboni kwangu

wakafanya hiyo kazi kwa ajili ya kuwachukua ili waende wakafanye kazi hiyo? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, maana naona kama kuna dakika mbili zimebakia. Naomba nizungmzie kidogo sana kuhusu misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, misitu katika eneo langu sijui kama kweli unaelewa kwamba inamalizika kwa kiwango ambacho sidhani kama tunaweza tukaja…hata kama tukiwa na mpango wa kupanda miti, sijadhani kama tunaweza. Kuna vibali sijui vinatokea wapi vya kuja kukata miti upande wa Jimbo la Songwe.

Mimi nilikuwa sijajua jinsi mkaa unavyochomwa, nimekwenda kuonyeshwa sehemu ya kuchomea mkaa ni nyumba kama ghorofa. Nikaanza kuuliza hivi hili ghorofa limechukua miti mingapi? Kweli inasikitisha sana. Namuomba Mkurugenzi wa Misitu atembelee Jimboni kwangu ili kusudi aje aangalie na aone ni jinsi gani anaweze kutusaidia katika suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada kuzungumza hayo, wenzangu wengi wameshayazungumza na mimi nina tabia ya kutorudia rudia. Naomba tu niseme kwamba naomba yale maelezo yapatikane ya jinsi gani nitasaidiwa mimi kuhusu mamba. Nilikuwa nimesita kwamba nisiunge mkono, lakini kwa kweli nitakuwa siitendei haki Serikali. Naunga mkono hoja! *(Makofi)*

**NAIBU SPKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona muda wa kuahirisha shughuli zetu umefika. Nina wachangiaji kesho kama 15. Kwa maana ya kesho, ni kwamba tunaweza tukawafika sana sana wachangiaji nane kama hakutakuwa na shughuli zingine maana *order paper* hatujapata. Kwa hiyo, tena hao wengine watakaokuwa wamebakia, itakuwa bahati mbaya. Lakini, nawashukuru kwa sababu asubuhi walikuwa hawapo watu hao wote. Lakini baadae wamejitokeza. Tumewahamasisha, wamejitokeza, sasa tunasema wako wengi. Basi ndio wakati unavyokuwa kwa sababu hatuna muda mwingi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nawashukuru sana kwa siku ya leo, tumeendesha mambo yetu vizuri na nategemea Wizara wataendelea kuyatafakari hayo yaliyozungumzwa kusudi kesho wawe na sehemu ndogo zaidi ya kutafakari kwa yale yatakayotokea kesho. Vinginevyo, naomba kuahirisha shukughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 11 Julai, 2008 saa tatu asubuhi)*